ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg Yahya Khamis Hamad	**Kny: Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Tano – Tarehe 24 Januari, 2012

Kikao Kitaanza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mohmoud Muhammed Mussa) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 64

Fedha za TASAF

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:-
Mhe. Mwenyekiti namuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Katika kipindi cha miaka kumi (10) iliyopita Benki ya Dunia ilisaidia Tanzania fedha za kusukuma mbele maendeleo ya Tanzania yaani TASAF. Fedha hizo zilizotengwa kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilisaidia sana juhudi za wananchi kujiletea maendeleo hasa katika Sekta za Elimu, Afya na Maji. Pia zilisaidia kuleta umoja na mshikamano katika jamii, hata hivyo baada ya kumaliza awamu ya pili ya mradi huo yaani TASAF II kumekuwa kimya kikubwa na kuwafanya wananchi kutokujua kinachoendelea.

(a) Serikali imefanya tathmini ya mradi huo kwa TASAF II na kubaini faida na hasara zake.

(b) Hivi Serikali imeshafanya mazungumzo na Benki ya Dunia kuhusu mradi huo kuendelea awamu ya tatu ili kuwapunguzia hali ngumu ya maisha.

(c) Kati ya Mikoa mitano (5) ya Zanzibar ni Mkoa upi umepata fedha nyingi za TASAF II.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Raisi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Makamo wa Pili wa Rais, kabla ya kumkjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 64 lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, TASAF II bado inaendelea na utekelezaji wa miradi kupitia mpango wa uhakika wa chakula, lakini mpango huu unatekelezwa katika baadhi ya Shehia tu, zilizochaguliwa na Wizara ya Kilimo na maliasili kupitia Mpango wa Taifa wa Uhakika wa Chakula. Miradi inayotekelezwa ni ya kilimo cha umwagiliaji, mazingira, mifugo, miradi ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, miradi ya uvuvi na kutoa elimu kwa wajasiri mali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Raisi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, Makamo Makuu ya TASAF Dar-es-Salaam kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa kutumia mshauri muelekezi, wamefanya tathmini ya miradi ya TASAF II Unguja na Pemba, ili kuangalia faida na changamoto zilizojitokeza. Tarifa ya tathmini hiyo inaonesha kwamba kuna mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi hiyo Unguja na Pemba.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Jamuhuri wa Muungao wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar imefanya mazungumzo na Benki ya Dunia kuhusu utekelezaji wa TASAF awamu ya tatu. Hivi sasa Kamati maalum ya wataalamu kutoka Zanzibar na Tanzania Bara wanaendelea na maandalizi ya awamu ya tatu na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwezi wa Aprili mwaka huu 2012.

(c) Mhe. Mwenyekiti, kwa wastan Mikoa yote ya Zanzibar imepata fedha zinazolingana. Hii inatokana na utaratibu uliowekwa katika ugawaji wa fedha za TASAF II. Utaratibu huo huwahusisha wahusika wengi wakiwemo wana Shehia wenyewe, Kamati mbali mbali za Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Kwa jumla kazi za upelekaji fedha za utekelezaji wa miradi inafanyika kwa kuzingatia mahitaji ya miradi husika na mashirikiano ya wadau wote, mambo ambayo huleta uwiyano katika miradi hiyo.

Nam. 102

Uingizwaji wa Dawa za Kulevya

Mhe. Rufai Said Rufai – Aliuliza:-

Namuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Inaonekana kwamba Zanzibar inaendelea kupoteza vijana wake ambao ndio nguvu kazi ya Taifa letu kutokana na madhara ya dawa za kulevya. Kwa kuwa Zanzibar si wazalishaji wa dawa hizi bila shaka zinaingizwa kutoka nje na njia mbili kuu zinazohusika na upitishaji wa dawa hizo ni Bandarini na Viwanja vya Ndege.

Je, Wizara yako imejiandaa vipi kuwa na vyombo vya kisasa ili kupambana na uingizwaji huu haramu wa dawa za kulevya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu :-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, napenda sana kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba jukumu la kupambana na uingizwaji wa dawa za kulevya nchini linatekelezwa na Jeshi la Polisi katika kitengo cha Udhibiti wa dawa za kulevya Zanzibar, chini ya Wizara ya Mambo ya ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Tume ya Taifa ya Udhibiti wa dawa za kulevya imepewa jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli zote za mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwenyekiti suala lake Nam. 102 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi, ni lazima nikiri kwamba vijana ni nguvu kazi ya Taifa na ndio ambao kwa kiasi kikubwa wanaendelea kupotea kutokana na athari ya matumizi ya dawa za kulevya Duniani kote ikiwemo Zanzibar. Miongoni mwa harakati za Jeshi la Polisi katika kukabiliana na uingizwaji wa dawa haramu za kulevya ni pamoja na:-

a) Kufungwa kwa choo maalum katika Uwanja wa ndege ambacho kitasaidia katika ugunduzi kwa watuhumiwa wanaoingiza dawa za kulevya nchini kwa njia ya kuzimeza.
b) Kuimarisha ulinzi katika sehemu ya uwanja wa ndege jambo ambalo limesaidia katika kuibua ukamataji hivi

karibuni wa kilo saba (7) za kokeni katika kiwanja cha Ndege cha Zanzibar zikitokea nchini Brazil. Aidha jumla ya mito kumi na moja (11) iliweza kukamatwa katika Bandari ya Malindi Unguja ambayo ilikuwa na vifurushi vya bangi mia mbili na sabiini na saba (277)vyenye uzito wa kilo kumi na tatu na nusu.

c) Kitengo cha Polisi cha Udhibiti wa dawa za kulevya kuendelea kujenga mashirikiano ya karibu na taasisi nyengine zilizo katika utekelezaji wa sheria ikiwemo Mahkama, Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka, TRA n.k

d) Jeshi la Polisi limekuwa na mashirikiano ya karibu sana na Taasisi ya kimataifa ya Jeshi la Polisi INTERPOL yenye Makao Makuu nchini Ufaransa katika kubadilishana taarifa za washukiwa wa dawa za kulevya, kutoka nchi mbalimbali. Hatua ambayo imekua ikisaidia katika kuwabaini washukiwa hao.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote hayo naomba nikiri kwamba mapambano dhidi ya dawa za kulevya ni changamoto kubwa Duniani kote ikiwemo katika Visiwa vyetu vya Zanzibar, kutokana na kuwepo Bandari nyingi zisizo rasmi ambazo huufanya ulinzi kuwa mgumu. Hivi karibuni Jeshi la Polisi Zanzibar limepata msaada wa boti mbili (2) mpya za kisasa kutoka Ubalozi wa Marekani ambazo zitasaidia kufanya doria ndani ya Visiwa vyetu. Aidha wahusika wakuu wa dawa za kulevya duniani kote wamekua mstari wa mbele katika kubuni mbinu mbalimbali za kudhoofisha jitihada za mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Mashirikiano ya dhati yanahitajika kwa taasisi na vyombo vya dola vilivyo katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya pamoja na jamii kwa ujumla.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini nitakuwa na suala moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri Zanzibar inaingiza wageni kutoka nchi mbali mbali siku hadi siku. Je, hatuoni kwamba ipo haja ya kufanya uchunguzi wa ziada ili kuangalia tatizo hili, pengine miongoni mwa wageni inakuwa ni sababu ya kuingiza haya madawa ya kulevya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hasa kutokana na shughuli za utalii ambayo nchi yetu imejikita sana. Zanzabar inapokea idadi kubwa ya wageni. Kwa sababu hiyo basi ndio maana katika Uwanja wa Ndege Zanzibar pamoja na Bandarini kuna kikosi maalum cha kupambana na udhibiti wa dawa za kulevya kwa maanja ya kufanya uchunguzi huo.

Vile vile kwa kushirikiana na mataifa mengine na kushirikiana na *Interpol* ndipo tunapobadilishana taarifa kwamba labda katika wageni hao watakaoshuka leo kuna mmoja ameanzia safari kutoka Itali akapita Brazil huwa wanapata taarifa kwamba sasa huyo mtilieni mashaka na mchunguzeni. Hicho ndicho kinachotokea kwa hivyo hilo linaeleweka na linafanyiwa kazi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza. Kwa kuwa uso umeubwa na haya na wenzetu wa Kenya walipogundua kwamba biashara hii inamatatizo ya kupata ushahidi kamili waliwaita wale ambao. ni *big suspect* katika mtandao ule na kuzungumza nao kibinaadamu, waisaidie nchi kutokana na madhara makubwa ya madawa haya ya kulevya. Je, wizara yake imechukua hatua gani ya kufanya utafiti kuhusiana na suala hili huko Kenya waliliandaa vipi na kuweza kulitekeleza hapa Zanzibar, ili hawa wafanyabiashara ambao ushahidi kamili haupatikani, wakazungumzanao kwa lugha ya kibinaadamu ili wakaweza kuachana na biashara hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba rai iliyotumika Kwenya na sisi pengine ingeweza kutusaidia. Lakini mbali ya jitihada zote za ofisi yangu, pamoja na jeshi la Polisi la kuwaomba wananchi kama wanawafahamu yaani ambao yeye amewaita *suspect* basi watupe taarifa kwa ajili ya kuwafatilia, lakini hadi hivi sasa hatujapokea majina yoyote kutwambia kwamba ndani ya nchi yetu hawa ndio wanaoshukiwa ili tukaweza kufanya mazungumzo na wao. Kwa hivyo kama Mhe. Mwakilishi anazo taarifa hizo za watu ambao wanashukiwa sisi tutakuwa karibu kushirikiana naye ili tusaidiane katika kutatua tatizo hili.

Mhe. Nassor Ali Salum: Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na kuipongeza serikali kwa kuweza kupata kifaa hicho.

Mhe. Mwenyekiti, pale Uwanja wa Ndege palikuwa na mbwa ambaye alikuwa anasaidia sana kuchunguza au kujua masuala haya ya madawa ya kulevya. Kwa taarifa zilizokuwepo kwamba mbwa yule amefariki. Je, taarifa hii ni kweli na kama ni kweli serikali ina mpango gani kupata mbwa mpya ambaye anasaidia kujua matatizo haya au kujua uchunguzi huu wa madawa ya kulevya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, taarifa aliyoitoa ni kweli kwamba mbwa yule ambaye alikuwa anasaidia katika kunusa madawa ambayo yalikuwa Air Port amefariki, hiyo taarifa ni ya kweli na ni sasahihi kabisa. Katika changamoto moja wapo inayokabili jeshi la polisi kwa hivi sasa ni kwa kukosekana mbwa huyo.

Lakini hivi sasa jeshi la Polisi imo katika hatua za haraka sana kuhakikisha wanampata mbwa kama huyo. Nilipoongea na jeshi la Polisi kwa kuweza kumnunua kutoka South Africa bei yake ni

kubwa sana. Lakini hapa hapa visiwani tunao mbwa ambao *quality* yao wanasema ni lazima awe ni mbwa ambaye ni mpole hawezi kuvamia, kazi yake yeye ni kunusa tu harufu. Kwa hivyo hapa wapo na wanauzwa kwa bei ya laki 4, wapo katika jitihada ya kumnunua ili waweze kum – *train* ili aweze kufanya kazi hiyo.

Nam. 118

Mafunzo kwa Madereva wa Viongozi

Mhe. Mohammed Said Mohammed - Aliuliza:-

Kwa kuwa madereva wengi wa serikali wanaowandeshea viongozi (VIP) wamekosa taaluma ya kuendesha viongozi. Je, serikali ina mpango gani wa kuwapeleka madereva hao katika Chuo cha Usafirishaji ili kujifunza taratibu za uendeshaji wa viongozi.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake namba 118 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba wapo baadhi ya madereva ambao taaluma zao hazijafikia kiwango cha juu cha kuwaendesha viongozi (VIP) na wanahitaji kuendelezwa kila mara waendane na wakati na magari ya kisasa wanayotumia.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa kuona haja hiyo ya kuwaendeleza zaidi madereva, kupitia Idara yetu ya Mafunzo na Maendeleo ya Watumishi na Chuo cha Utawala wa Umma kwa pamoja inaandaa mafunzo ya muda mfupi kwa madereva wote wa Viongozi.

Mafunzo haya yatendeshwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Taifa ya Usafirishaji Dar-es-Salaam (NIT). Kila muajiri atatakiwa kumgharamia mtumishi wake katika kushiriki mafunzo hayo kama itakavyooneshwa katika toleo maalum la wizara ambalo litatolewa hivi karibuni.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri umekiri kuwa madereva wengi wanaowaendesha viongozi wa juu hawana taaluma hiyo, na wizara yako imejipanga kuwapeleka kuwapeleka katika Chuo cha NIT. Je, serikali inafikiria vipi kuanzisha mtaala huo au chuo hicho kwa kushirikiana na NIT hapa Zanzibar.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikijibu suala mama nilisema kwamba Wizara yangu tayari imeandaa mtaala kupitia Idara yetu ya Mafunzo kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma na hivi karibuni tutatoa toleo ili kuelekeza ni kwa jinsi gani madereva watatakiwa kushiriki katika mafunzo hayo.

Nam. 66

Ajira za Walimu

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:-

Katika Bajeti ya mwaka huu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iliahidi kuwaajiri vijana wote waliosomea Uwalimu wa kuanza na wale wa Diploma na baadae cheti, hata hivyo hadi hivi sasa kuna vijana wengi hasa wa kike ambao hawajaajiriwa ingawa wengine wamemeliza mafunzo yao tangu mwaka 2007.

(a) Je, Mhe. Waziri unaweza kulifahamisha Baraza hili tukufu ni vijana wangapi ambao wameshasomea ualimu na hawajaajiriwa hadi leo.

(b) Je, Serikali bado ina lengo la kuwaajiri vijana hao katika mwaka huu wa fedha.

(c) Kwa vile Serikali bado haijaweza kuwaajiri vijana wengi waliosomea ualimu, hivi kuna haja ya kuendelea kuwasomesha vijana wetu kada ya ualimu.

Mhe.Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa idhini yao na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Namba 66 lenye sehemu (a) na (b) na (c) . Kwanza Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa maelezo ya utangulizi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa katika bajeti yake ya mwaka 2011/2012, wizara imeahidi kuajiri walimu waliomaliza mafunzo mbali mbali ya ualimu. Wizara inakusudia kuajiri katika hatu ya kwanza vijana waliohitimu mafunzo ya Shahada ya ualimu kwa ajili ya kufundisha katika skuli za sekondari hasa skuli mpya 16, na baadaye wataajiriwa wahitimu wa stashahada ya ualimu na kufuatiwa na waliohitimu mafunzo ya cheti cha ualimu. Wizara imeshapokea maombi kwa vijana wanaohitaji ajira na taratibu za kuomba kibali cha ajira tumeshazikamilisha na mara tu ruhusa itakapotolewa wizara yangu itaanza taratibu za uajiri.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Hadi sasa wapo jumla ya vijana 4,305 waliomba kazi ya ualimu miongoni wa 235 wamemaliza shahada, 2,234 Stashahada na 1,834 weny vyeti vya ualimu.

b) Wizara inakusudia kuajiri walimu 100 kwa mujibu wa nafasi za ajira zilizotengwa katika Bajeti yetu.

c) Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya ualimu kwa zile fani za masomo ambazo bado tunao upungufu mkubwa hasa mafunzo ya ualimu ngazi ya shahada na stashahada kwa masomo ya Hesabati, Sayansi, na somo la Kiingereza. Mafunzo ya cheti cha ualimu, hivi sasa yamesitishwa kutokana na kupungua kwa mahitaji isipokuwa mafunzo ya cheti cha elimu mjumuisho ambayo mahitaji isipokuwa mafunzo ya cheti cha elimu mjumuisho ambayo mahitaji ya walimu wa fani hiyo bado ni makubwa.

Mhe. Mwanaidi Kassim Juma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza suala dogo la nyongeza.

Ni kwa nini kwa sasa hawaajiri walimu wa dini na kiarabu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake la nyongeza. Ni kweli kwa sasa hatuajiri walimu wa dini na kiarabu kwa sababu mahitaji yao maskulini hatuna, tuna walimu wengi wa dini na kiarabu ambao wapo katika maskuli. Lakini kuna walimu wengi wa dini na kiarabu ambao tumewaajiri wapo kwenye masomo. Mhe. Mwenyekiti, kwas asa tunajaribu kuzungumza na walimu wetu kuwa licha ya kuchukua masomo ya dini na kiarabu lakini waweze kuchukua na masomo mengine kwa sababu mahitaji ya walimu wa dini na kiarabu hivi sasa hatuna. Sasa ikiwa wana na

masomo mengine ya ziada inakuwa ni rahisi kuweza kusaidia wizara yetu. Nakushukuru.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi naomba kuuliza suala dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kuna taarifa kwamba pamoja na kwamba umetaja kuna vijana 4,305 wameshasomea na wapo tu hawajaajiriwa,

(a) Lakini kuna taarifa kwamba ajira za vijana hawa zinafanywa kwa kujuana. Je, taarifa hii ni kweli.

(b) Na kama ni kweli huoni kwamba kuajiri katika misingi hiyo si kuwabagua Wazanzibari.

(c) Je, isingekuwa vyema pindi ambapo mkaajiri rasmi hawa vijana makaweza kubagua kwamba nafasi hizi zinahitajika Pemba na nafasi hizi zinahitajika Unguja kusudi kuweza kujua uwiyano baina ya wale watakaoajiriwa Pemba na watakaoajirwa Unguja kwa sababu kuna wakati watu wanatoka Pemba wanakuja kuchukua nafasi za Unguja au wanatoka Unguja kwenda kuchukua nafas za Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumjibu Mhe. Saleh suala lake la nyongeza.

Mhe. Mwenyekitik, si kweli kuwa Wizara yake inaajiri kwa upendeleo au kwa kujuana. Kwanza nataka ifahamike kuwa suala la ajira kwa sasa lipo katika Tume ya Utumishi Serikalini. Sisi kama Wizara ya Elimu tunapeleka maombi yetu katika Tume ya Utumishi kuwambia kama tunahitaji walimu kadhaa kwa ajili ya ajira. Baada ya hapo tume ya Utumishi hutangazia ajira hizo. Kwa

mfano hivi karibuni tu Tume ya Utumishi imetangaza uwajiri wa Shahada na diploma ya sayansi na walimu na walimu wetu tayari wameomba.

Suala la uwiyano kati ya Unguja na Pemba. Mhe. Mwenyekiti, mimi nashangaa kwa sababu Unguja na Pemba ni Zanzibar sasa tukianza kusema kwamba hizi ni nafasi za Wapemba na hizi ni nafasi za Unguja, kesho na keshokutwa tutakuja kusema hizi ni za mjini, hizi ni za Magharibi, tutaanza kubaguwana sisi wenyewe. Mara nyingi Wizara ya Elimu tunatizama pale ambapo pana mahitaji maalum. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ya suala la nyongeza. Mimi nataka niongezee majibu ya nyongeza katika suala zima la ajira kufanywa kwa kuelewana.

Nataka nimuhakikishie Mhe. Saleh kwamba suala hilo sasa hivi halipo na ndio maana Tume ya Utumishi Serikalini baada ya kupokea mahitaji ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wiki iliyopita ilitangaza rasmi nafas za ajira kwa walimu kwa ngazi ya diploma na digirii ya kwanza wale wa diploma kwa masomo ya sayansi na digirii ya kwanza kwa masomo ya Arti ya Sayansi. Sasa nataka nimuhakikishie kwamba hilo suala halipo.

Mhe. Mwenyekiti, na suala la kujua mahitaji ya hali halisi ya mskuli yetu. Moja kati ya masharti ya kupokea maombi ya Wizara yoyote au taasisi yoyote ya serikali ni kutaka walete uchambuzi wa mahitaji halisi. Ulikuwepo utaratibu wa watu kuomba ajira bila ya kuleta uchambuzi wa nafasi zinazohitajika. Sasa hivi masharti yetu ni kwamba kuajiri watu 300 mtuwambie, watu 300 hawa unawapeleka wapi na wapi na hali halisi ya mahitaji katika skuli zinazohusika zikoje ndipo tuweze kutoa kibali cha uajiri. Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema hayo ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c).

a) Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa walimu wetu ambao wamemaliza shahada ya kwanza walisoma kupitia mfuko wa mikopo wa Zanzibar. Kwa kuwa walimu hao wamemaliza tangu 2007 hadi leo hii hajaajiriwa Mhe. Waziri haoni kwamba wizara yake inachangia kudumaza mfuko huu kwa sababu bila ya ajira hakuna atakayerejesha mkopo.

b) Katika Baraza lilopita Mhe. Waziri alitwambia kwamba wameomba kuajiriwa walimu 800 leo anatwambia 1000, mimi naomba atwambie ni 800 au 1000.

c) Kwa kuwa Wazanzibari wanahitaji walimu na kwa kuwa serikali haijaajiri walimu na kwa kuwa wizara yake ilitwambia kwamba katika walimu 800 walioomba wameajiriwa walimu 60 tu. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba serikali hii haijaweka kipaumbele kama ni elimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nianze swali lako la (b) kwamba ni kweli kwenye bajeti yetu tuliomba walimu 800 na tukasema hapa kama tutaajiri walimu 800. Lakini kuna skuli zetu hizi mpya ambazo karibuni tunatarajia kuzifungua ambazo hizi peke yake zina mahitaji ya walimu 500. Kwa hivyo, tukaomba kupitia Tume ya Utumishi kuwa watusaidie kuajiri walimu hawa, hivyo badala ya 800 wao wakatuongezea tena 200 ikawa ni walimu 1000. Kwa hivyo, sasa tutaajiri walimu 1000 badala ya 800 kwa haya mahitaji ambayo yameongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa wanafunzi wetu wanaokwenda kuchukua mkopo ambao ni *degree* ya kwanza, wamechukua mkopo huo lakini nataka niseme kama kusomesha ni suala moja na ajira ni suala jengine. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu ni jukumu letu kusomesha na ukishasomesha ikiwa hukuajiriwa na serikali basi utaajiriwa na sekta binafsi. Lakini jambo la muhimu ni elimu kwanza, ajira itakuja baadae. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika uajiri nimeona kuwa vijana walioomba kuajiriwa ni vijana waliomaliza elimu ya *degree* na stashahada ambao ni wa sayansi wale wa *art* bado hawajaajiriwa.

a) Je, hawa walimu wenye sifa kama hizo lakini wamesomea art wao wameekwa katika sehemu gani.
b) Mhe. Mwenyekiti, tunao vijana waliosomea ualimu wa cheti ambao hawatajwi kabisa, tuseme nini adhma ya wizara kwa vijana hawa ambao nahisi ajira yao ni kama haiko tena.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ijapokuwa kanuni yetu inataka masuala matatu lakini kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nne la Mhe. Mwakilishi nadhani nitalijibu kwa maslahi ya wananchi wanaotusikiliza.

Mhe. Mwenyekiti, kama unakumbuka wakati tunasoma bajeti yetu tulisema kama tutaajiri walimu wote ambao tumewasomesha, lakini tutakwenda hatua kwa hatua. Walimu wa art pia tunawahitaji, lakini hivi sasa mahitaji makubwa ambayo ni ukosefu mkubwa ndani ya maskuli yetu ni hawa walimu wa *degree* ya sayansi na ya *art*. Lakini ni walimu wa diploma ya sayansi kwa hivyo namuomba Mhe. Mwakilishi awe

mstahamilivu na ajira itafuata hatua baada ya hatua. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

d) Hadi sasa wapo jumla ya vijana 4,305 waliomba kazi ya ualimu miongoni wa 235 wamemaliza shahada, 2,234 Stashahada na 1,834 weny vyeti vya ualimu**.**

e) Wizara inakusudia kuajiri walimu 100 kwa mujibu wa nafasi za ajira zilizotengwa katika Bajeti yetu**.**

f) Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya ualimu kwa zile fani za masomo ambazo bado tunao upungufu mkubwa hasa mafunzo ya ualimu ngazi ya shahada na stashahada kwa masomo ya Hesabati, Sayansi, na somo la Kiingereza. Mafunzo ya cheti cha ualimu, hivi sasa yamesitishwa kutokana na kupungua kwa mahitaji isipokuwa mafunzo ya cheti cha elimu mjumuisho ambayo mahitaji isipokuwa mafunzo ya cheti cha elimu mjumuisho ambayo mahitaji ya walimu wa fani hiyo bado ni makubwa.

Nam. 13

Msukumo kwa Idara ya Ushirika

Mhe. Salma Mussa Bilali - Aliuliza:-

Katika kutoa msukumo kwa Idara ya Ushirika ili iweze kufikia malengo na kupunguza tatizo sugu la usafiri, Mradi wa *ASSP* umeipatia gari mbili (2) Idara hiyo kwa ajili ya huduma zake za usajili na usimamizi ndani ya Vyama vya Ushirika. Gari hizo ni maalum kwa ajili ya shughuli hizo kwa Afisi ya Unguja na Pemba. Gari ya Pemba badala ya kutumika kwa shughuli iliyokusudiwa, kwa muda sasa imekuwa ikifanyakazi ya kumhudumia Afisa Mdhamini.

Je, Mhe. Waziri, Wizara inalifahamu suala hilo. Kama inalifahamu ina mpango gani wa kurekebisha kasoro hiyo ili gari hizo zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Mradi wa *ASSP* na *MANCEMP* umeipatia gari mbili (2) Idara ya Ushirika kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa shughuli zake za usajili, ufuatiliaji na usimamizi wa vyama vya Ushirika kwa Ofisi za Unguja na Pemba.

Ni kweli kuwa gari la Idara ya Ushirika Pemba, pamoja na kutumika kwa shughuli za kazi za usajili na ufuatiliaji wa vyama, pia linamuhudumia Afisa Mdhamini. Hali hii imesababishwa na ukweli kuwa wizara ni mpya na haina vitendea kazi vya kutosha, ikiwemo magari. Gari iliyopo kwa sasa kwa upande wa Pemba ni moja tu, yaani hiyo ya Idara ya Ushirika. Hali hii kwa kiasi fulani inaathiri utendaji wa kazi, ikiwemo pale inapotokea wizara kuwa na shughuli zaidi ya moja ya kutekeleza na zote zikiwa zinahitaji huduma ya usafiri.

Mhe. Spika, hata hivyo, wizara itaandaa utaratibu mzuri zaidi ili kuhakikisha kuwa kazi hazizoroti na kuwa gari hiyo inapatikana na kutumiwa kwa shughuli za usajili, ukaguzi, ufuatiliaji wa vyama vya ushirika. Aidha, naiomba Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika mwaka ujao wa fedha iongezee bajeti wizara yangu ili iweze kupata gari kwa ufuatiliaji wa shughuli zake Unguja na Pemba, na hivyo kupunguza baadhi ya hizo changamoto zinazoathiri utendaji kazi.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri imeelezwa kwamba kazi za ushirika ni kazi za *field* na ili tuwe na vyama imara inabidi vyama lazima vilelewe vizuri, visajiliwe, vifanyiwe *auditing* ili viweze kuwa vyama madhubuti na viwe endelevu. Mhe. Mwenyekiti, katika utafiti unaoendelea imeonekana kwamba ni vyama vingi vimekufa vimebakia kidogo, hii nadhani inasababishwa na tatizo hilo hilo la usafiri.

Je, Mhe. Waziri tunaomba utueleze utachukua hatua gani za haraka haraka ili Afisa Mdhamini angalau kwa muda apatiwe gari yake ili gari ya ushirika iendelee kubakia katika Ofisi ya Ushirika na iweze kufanya kazi zake kwa ajili ya kufanikisha shughuli za ushirika huko kisiwani Pemba.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na uhaba wa gari tuliokuwa nao huko Pemba na matatizo waliyokuwa nayo. Lakini kuna mashirikiano mazuri kati ya Ofisi yetu na Ofisi nyengine za Maafisa Wadhamini katika idara nyengine inapotokea haja basi huwa tunafanya hivyo, hata pale waziri anapofanya ziara kwenda Pemba kwa mfano inabidi atumie gari ya Afisa Mdhamini ambayo ni ya ushirika. Lakini pia hiyo haidhoroteshi kazi nyengine kwa sababu huwa tunaazima gari katika maeneo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba pamoja na yote hayo ambayo yanatendeka kazi zetu zinakwenda kama kawaida na *speed* ya kufanya kazi inakwenda, ingawa sio katika hali ambayo tungeitarajia kutokana na matatizo hayo, lakini tunajitahidi ili kazi zisidhorote na inshaallah tunatarajia katika kipindi kijacho basi mambo yetu yatakuwa mazuri na masuala haya Mhe. Mwakilishi atakuja kupunguza kwa kiasi kikubwa kipindi hicho.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niulize swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mhe. Mwakilishi kwa kulizindua Baraza kwamba gari ya kazi inatumika kwa shughuli nyengine. Kwa kuwa kazi za ushirika ni kazi zinazofufuliwa na kwa kuwa wakubwa wengi hupenda gari mpya. Je, haoni sababu kubwa ya hii gari kupewa Afisa Mdhamini huu upya wake.

b) Ni kwa kiwango gani angetueleza yeye kutokuwepo gari kumeathiri shughuli za ushirika ufuatiliaji kwani si kweli kwamba ilivyokuwa gari ni moja tu na ufuatiliaji ni gari hiyo hiyo na Afisa Mdhamini gari hiyo hiyo kwamba hapana taathira yoyote au hakuna utendaji wa kazi unaofanywa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kazi hazijadhorota kwa sababu nimesema nilipojibu swali mama kwamba tuna utaratibu wa kushirikiana na Ofisi za kule Pemba za sekta nyengine.

Lakini pia kuna vipando ambavyo tumepeleka vespa kwa kurahisisha hilo, pia kama hayo hayatoshi hivi sasa tumeimarisha kwa kuteuwa Maafisa wa Vyama vya Ushirika katika kila Wilaya ili kufuatilia kwa umakini zaidi.

Kwa hivyo, shughuli hazidhoroti kazi zinakwenda na inshaallah tuvute subra tunatarajia matatizo ya usafiri yatapungua hivi karibuni. Ni mapema mno kuyasema lakini kwa kweli kuna kila dalili za kufanikisha suala hilo la usafiri Unguja na Pemba.

Nam. 52

Huduma ya Dharura Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Ussi Jecha Simai - Aliuliza:-

Ni utaratibu wa kawaida duniani kwenye hospitali kubwa na hasa hospitali za rufaa kuwepo huduma ya dharura au ya haraka (*Emergency Service*), ili kuwasaidia kwa haraka wagonjwa ambao wako kwenye hali mbaya (*Critical Stage*) au wale wanaopata ajali. Kwa kawaida huduma hiyo huwa ni ya masaa 24. Inashangaza kwamba Hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja haina huduma hiyo muhimu.

(a) Mhe. Waziri, kwa nini wizara yako haijaweka huduma hiyo muhimu mpaka sasa katika karne ya 21.

(b) Kwa kuwa tumechelewa sana kuanzisha huduma hiyo, na kwakuwa huduma hiyo inahitajika sana kunusuru maisha ya watu wetu, ni lini wizara yako itaanzisha huduma hiyo.

(c) Kwa kuwa kwa sasa huduma hiyo haipo, na kwakuwa yapo mahitaji ya huduma ya dharura, wizara yako itaweka utaratibu gani wa kuwashughulikia kwa haraka wagonjwa wanaohitaji huduma ya haraka hasa wa ajali.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52, lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilikuwa naomba nitoe maelezo kidogo kwamba katika maswali kumeulizwa na kuna maneno ambayo hayakusemwa sawa nimesema nisahihishe hilo kwanza halafu nitoe maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna neno limetumika linaitwa *emergency services* lililo sahihi ni *emergency care*, neno jengine ni *critical stage* lililo sahihi ni *critical condition*. Hivyo ndivyo tunavyotumia maneno haya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nitoe maelezo yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti Hospitali ya Mnazi Mmoja imejengwa karibu karne moja iliyopita wakati wakazi wa nchi hii walikuwa 300,000. Ni ukweli uliowazi idadi ya wananchi imeongezeka kufika million 1.2 lakini ongezeko hili haliendi sambasamba na ukubwa wa hospitali yetu na muundo wake wa kutoa huduma za dharura. Mhe Mwenyekiti, sasa naomba kumjibu Mhe Mwakilishi swali lake (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

(a) + (b) Kwa kutambua kuwa huduma za dharura ni muhimu katika hospitali kubwa kama Mnazi Mmoja, wizara tayari imeshaanza maandalizi ya awali ya kukikarabati kiwanda cha zamani cha madawa ili sehemu ya jengo hilo liweze kutumika kwa huduma za dharura. Michoro ya ukarabati huo ipo tayari na ni matarajio yetu mwanzoni mwa nusu ya kwanza ya mwaka 2012 tenda za ujenzi huo zitatolewa.

(b) Mhe. Mwenyekiti, huduma za dharura zimekuwa zikitolewa kupitia idara ya wagonjwa wa nje kwa hivi sasa wakati tunajaribu kutatua hizo changamoto nilizozieleza hapo awali. Pia kwa kushirikiana na washirika wetu wa maendeleo, mwezi wa julai 2011, wafanyakazi 25 walipatiwa elimu ya nadharia na vitendo kuhusu ajali na huduma za haraka (*accident and emergency*) walifundishwa na wataalamu kutoka Uturuki kwa muda wa siku kumi. Aidha, wafanyakazi wengine 30 walipata mafunzo ya huduma ya kwanza kwa mgonjwa aliyeumia (*primary trauma care*) waliofudishwa na wataalamu kutoka Afrika Kusini, na kati ya hao 8 walipata mafunzo

zaidi ya kufundisha wengine (*Training of Trainer au TOT*) ambapo wataweza kuendelea na mafunzo hayo kwa kuwafundisha wengine. Mhe. Mwenyekiti, haya yote ni kudhibitisha kwamba huduma za dharura ni kipaumbele cha wizara yangu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri huduma hizo zinakwenda sambamba na huduma za *ICU*. Je, kukosekana kwa huduma hizo huoni kama tutaishusha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo inategemea kuwa ndio Hospitali ya Rufaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, *ICU* haitumiki tu kwa ajili ya *emergency* wala *emergency* si lazima itumie *ICU* inategemea hali halisi, kuna wengi tu wanaopata ajali wakaishia mapokezi wakenda zao na wengine wakapitia *theater* wakenda wodini wakenda zao na wengine wakaishia *ICU*. Kwa hivyo, *ICU* tumeshazungumza vya kutosha sasa sifikiri kama hilo tena lina mantiki kulitia hapa eti kwa sababu ya *emergency* na *ICU*. Mhe. Mwenyekiti, tumesema *ICU* itajenga na *emergency* itajenga kila kimoja kitajengwa lakini sio leo wakati utakapofika vitajengwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b)

a) Kwa kuwa majibu mengi yameshatolewa hapa kuhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja napenda Mhe. Naibu Waziri atuekee wazi suala la kuwa ni sahihi kuilenga Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ni hospitali ya rufaa. Kwa sababu leo katika majibu yake amejichanganya amesema ni hospitali iliyojengwa muda mrefu tokea watu 300,000 mpaka sasa watu milioni 1.2 haina nafasi za kutosha. Je, bado ni sahihi kuilenga Hospitali ya

Mnazi Mmoja pamoja na yote yaliyopo kwamba bado ni hospitali ya rufaa au kama swali lilivyoulizwa juzi kwamba patafutwe pahali pengine pakujengwa hospitali ya rufaa.

b) Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya muda wa miaka mitano katika kipindi kilichopita suala moja nilikuwa nikilizungumza sana ni kupatiwa *ICU* moja katika hospitali yoyote kule Pemba. Lakini tokea mwaka 2011 na leo tuko 2012 nimenyamaza kimya kwa kuwa hapa penye mama hapana. Je, ni lini nitaruhusiwa kuomba *ICU* kule Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, bado napenda kusema kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio itakayokuwa ni hospitali ya rufaa, kwa sababu hospitali ya rufaa si lazima hayo yote tunayoyafikiria yaweko pale, pale patakuwa na *specialize training*, patakuwa na *specialize wode* kwa ajili ya mambo ambayo yametakiwa yawepo pale. Mhe. Mwenyekiti, mambo mengine yatafanywa katika hospitali za kawaida. Kwa hivyo, hospitali ya rufaa ina mambo yake ya kuwa rufaa, na moja katika hospitali ya rufaa mambo yake ni kuwa na *ICU* na pia kuwa na *emergency care* na ndio maana tunasema kiwanda cha madawa kitakarabatiwa kuwe na sehemu ambapo *emergency care* na *ICU* iko pale. Mhe. Mwenyekiti, hakutokuwa na *ICU* moja katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, kutakuwa na *ICU* tofauti kulingana na mahitaji tofauti kwa ajili ya kuwa hospitali ya rufaa.

Mhe. Mwenyekiti, swali la pili nafikiri umeshajijibu mwenyewe kama hospitali mama haijapata *ICU* seuze ya Pemba.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika swali lake la msingi Mhe. Mwakilishi

alitia hofu kwenye suala zima la *emergency services* katika mahospitali yetu hasa Mnazi Mmoja.

Kwa kuwa suala hili linaenda sambamba sana na madaktari ambao wanaingia katika utaratibu wa kozi, na madaktari hawa hulipwa shilingi 2000 kila wanapoitwa. Je, haoni kwamba huduma hii ya *emergency* inaathiriwa sana na malipo ya madaktari kwa sababu unamtoa daktari kwenye wito wa dharura, lakini unamlipa shilingi 2000 tena za malimbikizo haoni kwamba ni sababu tosha hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kama anavyosema kwamba madaktari wetu ambao wanakuja kwa ajili ya kutoa *emergency care* wanatakiwa kulipwa shilingi 2000 kwa mwezi na hizo zinapatikana kila baada ya miezi 3, sidhani kama ni sahihi sijui taarifa hizo kazitoa wapi. Mimi ninavyojua kiwango cha chini kabisa ni shilingi 5000, labda kuwe kuna mabadiliko mengine na viwango vinalingana na taaluma ya daktari. Lini zinapatikana inategemea kupatikana kwa pesa hizo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja sisemi kwamba wanapewa kila mwezi. Kama pesa hazikutosha zilizopo kwa hiyo wanaambiwa mwezi huu hazipo, pengine na mwezi ujao zinakuwa hazipo hivyo zikipatikana wanalipwa kama *areas*.

Nam. 119

Taaluma ya Katiba

Mhe. Subeit Khamis Faki (Kny: Mhe. Mohammed Said Mohammed) - Aliuliza:-

Kwa kuwa inafahamika kwamba ni idadi ndogo ya Wazanzibari wanaojuwa kusoma Katiba ya nchi hii. Wakati zoezi la kutoa maoni juu ya marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano linakaribia.

(a) Je, ni asilimia ngapi ya Wazanzibari wanaoweza kusoma na kuzielewa Katiba za nchi yao.

(b) Kama ni asilimia ndogo, Je, idadi hiyo itatosha kujenga uhalali wa kutoa maoni ya mabadiliko ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe.Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 119(a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, kimsingi Wizara ya Katiba na Sheria haina twakimu sahihi ya idadi ya Wazanzibari wanaoweza kusoma na kuzielewa Katiba za nchi yao. Katika kuhakikisha kuwa Wanzanzibari wengi wanaelewa Katiba, Wizara kwa kushirikiana na Wanasheria wa Serikali pamoja na Jumuia za kisheria imekuwa ikishiriki kwenye vipindi mbali mbali vya redio na televisheni vinavyozungumzia elemu juu ya Katiba na Sheria nyengine mbalimbali za nchi.

   Hivyo kutokana na jitahada hizo zinachukuliwa na wizara tunaamini kuwa Wazanzibari wengi wanaovifuatilia vipindi hivyo watafaidika na taaluma inayotolewa kupitia vipindi hivyo.

b) Kama nilivyojibu awali kwamba Wizara ya Katiba na Sheria haina twakwimu sahihi ya Wazanzibar wanaoweza kusoma na kuelewa Katiba, hivyo jukumu letu sote kuhakikisha kuwa tunatoa elimu ya kutosha na kuwatayarisha vizuri Wazanzibari kuweza kujiandaa kutoa maoni yao kwa Tume ya Katiba. Wizara kama ambavyo imekuwa ikishirikiana na jumuia hizo katika kuandaa na kuweka utaratibu utakaohakikisha kila Mzanzibari anapata

elimu itakayomuwezesha kushiriki vyema katika kutoa maoni juu ya Katiba mpya ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara yangu imejitahidi kutafuta Katiba ya Jamhuri ya Muungano ili iweze kuzigawa kwa wananchi kwa kuanzia tumeshapata Katiba 500 na hivi sasa tuna mpango mwengine wa kupata angalau Katiba 1000 ili tuweze kuzigawa mwahala mbali mbali katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ni kuwa hivi sasa wizara yetu inajiandaa na vijarida mbali mbali vya kueleimisha Wanzanzibari kuhusu mambo muhimu yaliyomo katika Katiba hiyo ya Jamuhuri ya Muungano. Vipeperushi hivi ambavyo vitakuwa kwa lugha nyepesi vitawasaidia sasa Wanzanzibari katika kuielewa Katiba hiyo, na hivyo kuwaweka katika nafasi nzuri ya kutowa mawazo yao ya vipi Katiba mpya iwe katika Katiba hiyo ya Jamhuri ya Muungano. Vipeperushi hivi ambavyo vitakuwa kwa lugha nyepesi vitawasaidia sana Wazanzibari katika kuelewa katiba hiyo na hivyo kuwaweka katika nafasi nzuri ya kutoa mawazo yao ya vipi katiba mpya iwe.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini napenda kumuuliza kuwa, hivi karibuni tulipata taarifa ya kwamba wenzetu Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kupitia Mwenyekiti wa Chama aliwapa shilingi milioni moja kwa ajili ya kuweza kupita majimboni mwao kuwahamasisha wananchi kwa ajili ya katiba.

Sasa kwa sababu Mhe. Waziri amesema Waheshimiwa Wawakilishi wapite katika majimbo yao na kama kupita katika majimbo hayo basi lazima gari zetu tutie mafuta kwa ajili ya suala hili. Sasa kupitia wizara yake atatusaidiaje Waheshimiwa Wawakilishi ili kuwafikia wananchi wetu na kuwaelimisha zaidi kuhusiana na katiba hii.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haina mpango wa kutoa fedha kwa kuwapa wawakilishi kujaza magari yao mafuta kupita katika majimbo. Hilo ni jukumu la kila mwakilishi aliye na nia ya kuwasaidia wananchi wake katika jimbo. Kwa hivyo, hili ni jukumu lao na si la wizara yangu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia fursa hii naomba niulize swali la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amesema hapa kwamba wizara yake imejipanga kutafuta katiba kwa ajili ya kuzigawa na ametwambia kwamba amepata nakala 500 na anatafuta nakala nyengine 1000. Lakini tulipata taarifa rasmi kupitia vyombo vya habari na hata katika Bunge la Jamhuri ya Muungano waliwahi kutangaza kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano imechapisha au inakusudia kuchapisha nakala milioni moja za Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kuzigawa. Sijui Mhe. Waziri anaweza kutueleza kwamba wamewasiliana ili Zanzibar nayo ipate mgao wake wa katiba hizo kwa ajili ya Wazanzibari.

(b) Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia katika kusaidia wananchi ili kuweza kuelewa yanayotaka kuchangiwa na hasa yale mambo ambayo yanagusa maslahi ya Zanzibar. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ana mipango gani ya kuchukua utaratibu kama ule alioufanya wakati wa mjadala wa Mswada wa Sheria wa Mabadiliko ya Katiba, ambapo alifanya kazi nzuri sana naomba nimpongeze na wizara yake ya kuwakusanya watu wenye ujuzi mbali mbali na kwa pamoja wakaongoza kutoa maoni yale ambayo yameisaidia Zanzibar pakubwa.

Sasa sijui katika hatua hii ya pili wizara yake imejipanga vipi kuona inachukua hatua kama ile ili kuwa na timu ambayo itakuwa inaandaa muongozo na kwa wale wananchi ambao uelewa wao ni mdogo waweze kujua ni maeneo gani hasa ambayo yana umuhimu kwa Zanzibar na kuweza kuyachangia ili kupata msimamo wa aina moja kutoka upande wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba tumeshapata nakla 500 za katiba na kwamba kuna mpango wa kupata nakla nyengine 1000. Hizi ni nakla ambazo tumezipata katika Wizara ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na tulizungumza na waziri mwenzangu wa Katiba na Sheria hiki ni kiporo ambacho kilikuwepo zamani, tunajua na tulizungumza kwamba ziko nakla milioni moja ambazo zinachapishwa.

Nilisema hapa kwamba tutapata nakla nyengine baadae ni kutokana na hiyo, siwezi kusema sasa hivi kwamba ngapi tutapata, lakini zile ambazo zilikuweko ndio tulipata hizi 500 na 1000 ziko njiani na zikimaliza hizo nyengine kuchapishwa naamini na sisi tutapata kwa mujibu wa makubaliano yetu tuliyozungumza. Kwa hivyo, naomba tusiwe na wasi wasi nakla za kutosha tutazipata ili kusaidia hili.

La pili Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, katika kujiandaa na masuala haya hivi karibuni wizarani kwangu tuliwaita baadhi ya wadau na tukazungumza nao na tukawapa miongozo fulani ya kufanya. Lakini napenda tujue kwamba suala hili ni la wananchi wenyewe si la serikali, wananchi ndio wanaopaswa kutoa maoni. Kwa hivyo, si vizuri serikali kuingilia moja kwa moja itakuwa kama ni maoni wanayopewa wananchi na serikali, tunachotaka ni kwamba wananchi watoe maoni yao ili yaweze kuzingatiwa.

Tumeshakutana na baadhi ya viongozi mbali mbali ili kuwapa ule utaratibu mzima wa shughuli hii vipi ifanywe na miongozo hiyo tutaendelea kutoa mara kwa mara.

Nam. 71

Kuungiwa Umeme Majumbani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Ingawa wananchi wamekuwa wakijigharamia wenyewe kuvuta umeme majumbani mwao, lakini kupata umeme huo imekuwa ni kero na ghilba kubwa.

Je, ni lini hasa kikwazo cha kupatiwa huduma hii ya msingi kitaondoka.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli wananchi wamekuwa wakijigharamia wenyewe kuvuta umeme. Njia hii ni ya kawaida kwa mashirika yote ya umeme Tanzania, yule yeyote anayehitaji kuungiwa umeme inampasa agharamie.

Mhe. Mwenyekiti, katika kujibu swali la msingi ni kwamba, hakuna kikwazo chochote kwa mwananchi yeyote anayetaka kuungiwa umeme ilihali ya kuwa afuate masharti yaliyowekwa na Shirika la Umeme.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa lengo la serikali ni kufikisha huduma ya umeme vijijini kunufaisha wananchi, Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto imetembelea *SACCOS* moja ya Mkipimiliki iliyoko Jimbo la Mtambwe, ni wananchi waliyoonesha juhudi zao kwa nguvu zote na hivi sasa tayari wameshalipia umeme huo kwa muda mrefu hawajapata huduma hiyo.

Je, kutokuwafikishia umeme kwa wakati huoni Mhe. Naibu WAziri ni kuwadhalilisha wananchi wale au kuwaonea, na ifikapo Febuari 2 kuna wahusika watakuja kukagua maendeleo ya kikundi kile na naamini hii taarifa utakuwa huna, lakini kutokana na utendaji wako naamini muda mfupi matatizo hayo yatatuka.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika jibu mama kwamba huwa tunachelewa kuwaunganishia watu umeme kutokana na matatizo mbali mbali ambayo yanatukabili hususan uchelewaji wa vifaa. Vifaa vyetu huwa tunategemea kutoka Afrika ya Kusini na sehemu nyengine, vinapochelewa vifaa hivyo huwa inatupasa kuchelewa kwa kufanywa kazi za uunganishaji umeme katika sehemu zinazohusika. Lakini wizara yangu kupitia Shirika la Umeme itajitahidi kuyashughulikia masuala hayo na mimi mwenyewe tukijaaliwa nitalifuatilia suala hilo kikamilifu na nitakwenda Pemba kwenye hicho kijiji kwa kulisisitizia suala hilo lifanikiwe haraka iwezekanavyo.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniruhusu nami kuuliza swali dogo la nyongeza. Nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini hivi sasa shirika tunajua ni shirika binafsi linalojiendesha wenyewe na gharama za umeme zinakuwa ni kubwa sana. Lakini juu ya hayo bado shirika liko mbioni na halijafikia lengo la kuwapelekea wananchi umeme

ambao ni nishati moja muhimu sana. Kwa hivyo, wananchi wanachangia gharama za kufikishia umeme katika eneo lile na mara nyingi umeme ni gharama zaidi ya shilingi milioni 20 pengine na kuendelea.

Je, haoni kwamba hivi sasa upo umuhimu wa shirika kuingia ubia na wale watu ambao wanafikisha huduma ile ili baadae wakawarejeshea faida yao au gharama zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia wizara yangu lengo ni kuwasambazia huduma ya umeme wananchi wake wote. Katika kulizingatia hilo, shirika langu la umeme kwa sasa mteja yeyote ambaye anahitaji kuunganishiwa umeme laini isiyopungua ya nguzo nne basi nguzo mbili tutamsaidia sisi shirika ili tu kufanikisha shughuli hiyo. Kwa hivyo, lengo letu ni kuboresha na kuwasaidia wananchi kwa mujibu wa sheria inavyostahiki.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri atakubaliana nami kuwa viko baadhi ya vijiji havijafaidika na huduma hii ya umeme kikiwemo Kijiji cha Kangani Kuukuu cha Muuka. Kwa kuwa ombi lao hili wameshalileta kwako je, ni lini utawakamilishia lengo lao la kupata huduma hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kuna baadhi ya vijiji vyengine bado huduma ya umeme haijafika. Lakini kama nilivyozungumza lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kusambaza umeme katika vijiji vyote. Kwa hivyo, hicho kijiji ambacho hakijafika umeme basi nakuomba Mhe. Mwakilishi tushirikiane, nipe taarifa, nikumbushe na tukijaaliwa huduma hiyo itafika.

Nam. 58

Upatikanaji na Utoaji Leseni za Udereva

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:

Sheria ya Usalama Barabarani imewataka watu wanaotaka leseni za udereva wa vyombo vya moto vya barabarani kupata mafunzo kwenye Vyuo au skuli za Udereva (*Driving Schools*) kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu na dereva huyo hupatiwa cheti cha Udereva.

Kwa kuwa baadhi ya vijana hupatiwa leseni baada ya kumaliza mafunzo hayo wakiwa na umri mdogo (chini ya miaka 18).

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako ina mpango gani katika kukabiliana na suala hili.

(b) Mhe. Waziri ni madereva wangapi kwa Zanzibar wanazo leseni za kuendeshea vyombo vya moto lakini hawakupitia Skuli za Udereva.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ili kukabiliana na suala hilo wizara yangu kabla ya kumpatia mtu leseni ya udereva mwanafunzi (*learner*) analazimika kuleta mambo yafuatayo:-

i) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa

ii) Kitambulisho kinachokubalika

iii) Cheti kinachothibitisha kuwa afya yake inamruhusu kuendesha chombo cha moto kinachotumia barabara kutoka katika hospitali ya serikali inayokubalika.

iv) Picha mbili za Passipoti

v) Barua kutoka katika skuli ya udereva au cheti cha kumaliza skuli ya udereva kwa wale waliosoma nje ya Zanzíbar. Zaidi ya hayo anafanyiwa mitihani ya Nadharia na Vitendo na akifaulu zaidi ya alama 70 (70%) anakabidhiwa cheti cha umahiri ambacho ndicho uthibitisho wa kumpatia leseni. Aidha, deriva mwenye umri wa miaka 16 anaruhusiwa kuendesha chombo cha Maringa mawili kisichozidi mwendo wa 50km/h na uwezo wa silinda (50cc), kwa maana ya moped na pasola.

(b) Zanzíbar inayo jumla ya maderera 45,265 na kati ya hao watu 22,674 hawakupita skuli za udereva kwa sababu walikuwa na leseni kabla ya kuanzishwa utaratibu huo mpya wa kwenda katika vyuo vya mafunzo.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, pamojana majibu mazuri ya Mhe. Naibu waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri ana mpango gani kwa maderera wa zamani ambao upatikanaji wa leseni zao ulikuwa nje ya sheria Nam. 7 ya mwaka 2003.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Samahani Mhe. Mwenyekiti, naomba arudie tena swali lake lijalisikia.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Waziri ana mpango gani kwa wale maderera wa zamani ambao upatikanaji wao wa leseni ulikuwa nje ya sheria Nam. 7 ya mwaka 2003.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, katika jibu (b) tumeeleza kwamba Zanzíbar kwa ujumla ina maderera 45,265, kati ya hawa maderera 22,674 walikuwa katika kundi hilo ambalo amelisema kabla ya sheria hii mpya, baada ya kuja sheria hii mpya tumewabadilishia leseni zao wameingia katika mkumbo huu. Lakini jumla yao ndio hiyo idadi ya 22,674.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri wa wizara nzito ya Miundombinu na Mawasiliano swali la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Kwa sababu hawa aliowataja ambao hawakutimiza masharti ya sifa ya sheria hiyo ya mwaka 2003 wapo na wengine wanaendesha vyombo vya usafiri ambavyo vinapakia abiria na pengine ndio sababu ya kuhatarisha hata usalama wao. Wizara ina mpango gani wa kuona kwamba inafanya uhakiki na wale ambao hawana sifa za kuendelea kuwa maderera wanyang'anywe leseni zao.

(b) Kwa maderera ambao wamekuwa wakiendesha gari za abiria hapa kwetu maarufu daladala, katika nchi za wenzetu uzoefu unaonesha kwamba maderera wanaoendesha gari za abiria Mbale ya mafunzo ya kawaida wanapatiwa mafunzo maalum na baadae wanafanyiwa uhakiki kupitia mafunzo ya vitendo ili kuonekana kwamba wanaweza kupewa dhamana ya kupakia abiria na hivyo kukabidhiwa usalama wa maisha yao.

Je, kwa Zanzíbar wizara imejipanga vipi kuanzisha utaratibu kama huu. Kwa sababu tunaona madereva wengi wanaoendesha daladala ni vijana wadogo wengine unaona wametawaliwa zaidi na uzembe kuliko kujali maisha ya wale wanaowaendesha.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kati ya lile kundi ambalo walikuwa wakimiliki leseni kabla ya sheria yetu mpya ya mwaka 2003 utaratibu uliotumika ni kwamba tulizihakiki. Kabla ya hapo mfumo wa kupata leseni uko wazi, kilichoongezeka hapa ni namna ya kwenda na mafunzo ya skuli, lakini kabla ya hapo wasimamizi wetu katika kitengo kile cha utoaji wa leseni walikuwa watu wanawapeleka *try* wakijiridhisha kwamba mafunzo haya ya vitendo ameridhika ndipo utaratibu wa kupata leseni anakabidhiwa.

Aidha, nakubaliana naye kama kutakuwa kuna madereva ambao wanaonesha kutokuendana na umahiri na usalama. Wizara yangu kwa kupitia kitengo chetu hicho kitaendelea kufanya uhakika na ikithibitika basi tunaweza tukachukua hatua za kuwanyang'anya. Utaratibu wa kumnyang'anya leseni tumepewa mamlaka hayo kwa mujibu wa sheria hii mpya ya Nam. 7 ya mwaka 2003. kwa hivyo, hakuna tatizo na tutaendelea kufanya hivyo kwani katika kufanya hivyo tutakuwa tunatekeleza utaratibu ambao tumepewa kwa mujibu wa sheria yetu hii.

Jibu (b) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi kuhusu maderera wetu wa daladala. Lakini napenda nimthibitishie kwamba, pamoja na kupata leseni hizo utaratibu wa kupata leseni ya daladala inazingatia kwanza umri na uzoefu, pamoja na kwamba utakuwa umemaliza skuli lakini kama hujapata uzoefu wa miaka mitatu huwezi kuruhusiwa kupata leseni ya kuendesha gari ya abiria kwa maana ya daladala na gari za abiria.

Hivyo namthibitishia kwamba utaratibu huo unaotumika huko katika nchi nyengine ndio utaratibu unaotumika kwetu, kwani baada ya kumaliza mafunzo lazima tupate pikindi cha miaka mitatu ya kujenga uzoefu ili uweze kupata leseni na kuendesha gari.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuulisa swali dogo la nyongeza. Pamoja na mafanikio mazuri ya wizara hii ya miundombinu ya kuanzisha vyuo vya mafunzo ya udereva ambapo ni pamoja na kuwapatia mavazi mazuri makonda na maderera wetu. Naomba kujua mafunzo yale ya kuvaa nguo nzuri yamepatikana wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kuwataka maderera na makonda kufaa fomu huu unatokana na sheria mama Nam. 7 ya mwaka 2003 chini ya kanuni zake. Katika kanuni zinazosimamia sheria ile ndizo zinazotaka kwamba mamlaka husika iwatake maderera na makonda kuvaa fomu ili kuweza kuwatambua na kuondoa usumbufu kwa wananchi wetu na wengine wapatao huduma katika magari hayo.

Nam. 65
Upandaji holela wa Bei za Vyakula

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya saba (7) yenye Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa imekuwa inajitahidi kutekeleza malengo yake yakuwaletea neema wananchi wa Zanzibar, hata hivyo bado kuna kilio kikubwa cha wananchi kutokana na upandaji holela wa bei za vyakula.

(a) Kwa kuwa wananchi wengi wa Zanzibar kipato chao ni kidogo. Serikali inachukua hatua gani za kukabiliana na upandaji huo wa bei za vyakula.

(b) Je, Mhe. Waziri unaweza kuliambia Baraza hili tofauti ya bei za vyakula vya mchele, sukari na unga wa ngano za mwezi wa Oktoba 2010 kabla ya Uchaguzi Mkuu na bei ya bidhaa hizo za mwezi wa Oktoba 2011 na Je, bidhaa hizo zimepanda bei kwa asilimia ngapi.

(c) Kwanini serikali haiweki utaratibu wa kila miezi mitatu wa kutoa bei elekezi kwa bidhaa hizo muhimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 65 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi kutekeleza malengo yake ya kuwapunguzia makali ya maisha wananchi wake. Pia ni kweli kwamba kuna kilio cha wananchi kuhusiana na upandaji wa bei za bidhaa na zaidi bidhaa za chakula.

(a) Ili kukabiliana na upandaji holela wa bei za vyakula, serikali imechukuwa hatua kadhaa za usimamizi wa bei za vyakula muhimu kama ifuatavyo:-

- Kuandaa kanuni mpya za usimamizi wa bidhaa kwa kushirikiana na wafanyabiashara. Kanuni ambazo zinasimamia pamoja na mambo mengine uagiziaji bidhaa za mchele, unga wa ngano, sukari na utaratibu wa uwekaji wa bei za bidhaa hizo.

- Kupanga bei za bidhaa hizo kwa mashirikiano baina ya serikali na wafanyabiashara baada ya kuzingatia gharama zote za bidhaa husika zinapofika hapa nchini. Baada ya kufikia makubaliano hayo serikali hutangaza bei elekezi za bidhaa hizo kwa wananchi. Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla serikali imeanza kuona manufaa ya ushirikiano huo kwani bei za bidhaa hizo zimeanza kutulia na hupanda pale tu inapolazimika chupando, tena ni baada ya kuthibitshwa na pande zote mbili.

(b) Mhe. Mwenyekiti, tofauti ya bei za Mchele, Unga wa ngano na Sukari kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 na Oktoba, 2011 ni kama ifuatavyo:-

BIDHAA	**BEI ZA OKTOBA, 2010**	**BEI ZA OKTOBA, 2011**	**ONGEZEKO %**
MCHELE	1,000/=	1,200/=	20
U/NGANO	900/=	1,000/=	11.1
SUKARI	1,200/=	1,800/=	50

(c) Serikali imeweka utaratibu wa kufanya mapitio ya be iza bidhaa kila wakati panapotokezea mabadiliko ya moja ya sababu nilizozitaja wakati nikijibu swali mama ikiwemo pia taratibu za kuongezeka au kubadilika kwa bei katiak soko la dunia. Kupanda na kushuka kwa pesa ya Kitanzania kulingana na dola na baada ya mapitio ya bei mpya elekezi Mhe. Mwenyekiti inatangazwa kwa biombo vyetu vya habarí na habarí hizo hupelekwa pia kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wafanyabiashara katika ngazi mbali mbali pamoja na masheha ili wananchi wetu wapate taarifa hizo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri naomba niulize swali moja la nyongeza lenye sehemu mbili.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka wakati wa bajeti ya wizara hii mwaka jana wizara kama alivyosema naibu waziri ilitoa bei elekezi. Sasa ningependa kujua serikali sasa inaisimamia vipi hiyo bei elekezi kwa wafanyabiashara.

Lakini swali la pili, tangu bei elekezi ile ilipotolewa hadi sasa imeonekana kwamba kuna upandaji wa bei hizi kinyume na alivyotaja Mhe. Naibu Waziri kwa baadhi ya wafanyabiashara. Naomba nijue tangu ilivyotolewa ni wafanyabiashara wangapi hadi sasa wameonekana kukiuka bei hiyo elekezi na ni hatua gani zilizochukuliwa na serikali dhidi ya hawa ambao wanakiuka utaratibu huu ambao umepangwa baina ya serikali na wafanyabiashara wenyewe.

MHe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikijibu swali mama nilisema kwamba huwa tunakaa na wafanyabiashara kwa kuzingatia masuala yale niliyoyataja. Kuna suala zima la kuongezeka kwa bei katika soko la dunia, kuna suala zima la gharama anazozipata mfanyabiashara toka kununua bidhaa zile mpaka kufika hapa nchini. Lakini pia kumejitokeza suala jipya la ugaidi katika bahari ya Hindi kwenye pembe ya Afrika nalo lilichangia kiasi kikubwa sana cha kuongezeka kwa bei za bidhaa.

Kwa hivyo, tunapokaa na wafanyabiashara tunazingatia masuala yote haya na ndio bei elekezi inapotangazwa kwa makubaliano. Sasa ikishatangazwa Mhe. Mwenyekiti, tunaitoa kwenye vyombo vya habari pamoja na viongozi niliowataja.

Lakini kawaida kwa wafanyabiashara wetu wengine wadogo wadogo kukiuka taratibu zinapowekwa. Sasa kuna utaratibu ndani ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko wa Maafisa wa Biashara kupita na kukagua kila pale inapohitajika kufanya hivyo, wanapogundulikana huwa wanachukuliwa hatua kama sheria inavyoelekeza.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali mama

alisema kwamba serikali imo katika kuandaa kanuni mpya zitakazoweza kusimamia upandaji wa bidhaa kiholela. Kwa kuwa wananchi wetu wametaabanika sana na upandaji wa bidhaa kiholela. Je, Mhe. Waziri ni lini kanuni hizi zitakamilika na ziweze kutumika ili kuwasaidia wananchi wetu kupanda kiholela kwa bidhaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nimesema kwamba tayari tuna utaratibu wa kukabiliana na ongezeko hili la bidhaa na hasa za vyakula. Utaratibu huu ndio tunaoufanyia kazi kila panapotokea haja ya kufanya hivyo kutokana na sababu mbali mbali basi tunatoa bei elekezi kwa mashirikiano ya pamoja na wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa hizo na ndipo tunapozitangaza.
Kwa hivyo, nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba tayari zoezi hili tunalifanyia kazi na ndio maana utakuta bei hazipandi kwa kasi kama ilivyokuwa huko nyuma kwa sababu kabla ya kupanda kwa bei za vyakula lazima kwanza wizara na wafanyabiashara wanakaa pamoja kukubaliana.

Nam. 61

Upandaji wa Bei za Bidhaa

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza:

Wazanzibari wote kupitia kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa walijenga imani ya kupata unafuu wa bei za bidhaa muhimu hasa chakula na vifaa vya ujenzi. Lakini kila siku zinavyozidi kwenda mbele ndio bei za bidhaa hizo zinavyozidi kupanda na kuwaongezea ukali wa maisha wananchi.

(a) Je, Mhe. Waziri anawaeleza nini Wazanzibari kuhusu mustakbali wa bei za chakula na maisha yao kwa ujumla.

(b) Je, Tume ya Kusimamia Bei inashirikishwa vipi katika suala la upandishaji wa bei za bidhaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwaelezea wananchi wote kwa jumla kwamba serikali kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inafanya juhudi kubwa sana kusimamia suala zima la uwekaji wa bei hasa bidhaa muhimu ikiwemo mchele, unga wa ngano na sukari ili kuhakikisha hakutokei upandaji wa bei usio wa lazima.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuwaelezea wananchi kuwa Zanzibar kwa kiasi kikubwa bidhaa hizi zinategemea uagiziaji kutoka nchi za nje. Udhibiti wa bei za bidhaa hizi utaendelea kuathirika kutokana na hali ya soko ya dunia yaani *world market* na mabadiliko ya thamani ya sarafu ya Tanzania kulingana na dola ya Marekani kama nilivyosema wakati najibu swali Nam. 65.

Aidha, naomba nishauri kwamba tuongeze juhudi za kutoa kipaumbele zaidi katika sekta ya kilimo ili zile bidhaa ambazo tunaweza kuzizalisha hapa nchini basi tuzizalishe kwa wingi ili kupunguza kutegemea bidhaa hizo kuagizwa kutoka nje.

(b) Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kuwa Tume ya Kusimamia Bei kwa hivi sasa haipo. Tume hiyo ilifutwa mara tu Serikali ilipopitisha Sera ya Biashara Huria mwaka 1999 ambapo sasa bei hupangwa kutokana na nguvu ya soko.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kushirikiana na wafanyabiashara kwa kupitia utaratibu tuliojiwekea mwaka 2011 huwa tunasimamia bidhaa za huduma za biashara. Pia serikali husimamia upandaji wa bei wa bidhaa hizo kwa mashirikiano na wafanyabiashara hao kulingana na thamani ya bidhaa hizo kutoka katika soko hadi hapa nchini ili kuhakikisha bei za bidhaa hizo hazimuathiri sana mtumiaji.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kuna wafanyabiashara wangapi ambao wamewahi kuchukuliwa hatua kwa kukiuka agizo la tume kwa kuuza bidhaa kwa bei ya juu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, tokea tumepitisha utaratibu huu wa kukaa na wafanyabiashara na kuelewana nao katika kuzingatia bei za bidhaa hakuna mfanyabiashara hata mmoja aliyeshtakiwa. Kwa sababu mpaka sasa wote tunakubaliana katika kuzingatia bei zile na kuzifanyia kazi haziendi nje na utaratibu tunaokubaliana.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hakuna bodi ya kushughulikia bei je, Mhe. Waziri haoni kwamba kuna udhaifu mkubwa kwa wananchi kuhusu kupangiwa bei zao. Kama hakuna bodi haoni kwamba kuna sababu ngumu ya kupanda vitu kiholela kila siku bila ya kufuata sheria.

Mhe. Naibu Waziri wa wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikijibu swali Nam. 65 nilisema kwamba suala la biashara na hasa bidhaa za chakula limeachwa huria kwa wafanyabiashara. Kutokana na sababu hiyo, toka mwaka 1999 nilivyotamka katika jibu la swali hili la 61

Tume ya Kusimamia Bei imekuwa haipo. Lakini kwa mashirikiano mazuri tuliyonayo wizara na wafanyabiashara tumeweka utaratibu wa kukaa nao na kukubaliana kwa sababu wao ndio wanaoagiza na kuingia katika gharama mpaka kuzifikisha bidhaa hapa nchini kwa hivyo si rahisi kuwawekea tume.
Lakini kwa makubaliano ya pamoja Mhe. Mwenyekiti, tumeweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kuweka bei ambayo inakidhi haja kwa mtumiaji lakini na mfanyabiashara nae hapati hasara.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake ya swali la msingi alitaja moja ya sababu zinazopelekea kupanda kwa kasi kwa bei za bidhaa ni suala la kushuka kwa thamani ya shilingi ukilinganisha na dola ya Kimarekani.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha kama miezi mitatu hadi minne iliyopita dola ya Kimarekani thamani yake ambayo ilikuwa kama shilingi 1,550 ilikuja ikapanda hadi kufikia shilingi 1,800. Lakini baada ya hatua za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Benki Kuu kuingilia kati thamani hii imerudi na kufikia kiwango kile kile ambacho kilikuwa kama miezi minne iliyopita. Lakini kwa wafanyabiashara ambao wametumia hii kuwa ni moja ya sababu za kupandisha bei za vyakula haijapelekea kushuka tena kwa bei za vyakula ambazo zilipanda kipindi kile.

Sasa wizara inachukua hatua gani kwa wafanyabiashara kama hawa ambao wanatumia vibaya fursa kama zile na kuendelea kuwakandamiza walaji ambao ni maskini raia wa nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana nae kwamba shilingi ya Tanzania katika miezi mitatu iliyopita ilipanda kutoka shilingi 1,550 mpaka karibu shilingi 1,800. Pia ni kweli wafanyabiashara walipandisha bei za

bidhaa za vyakula lakini baada ya kukaa kwa pamoja kufuatana na kupanda kwa thamani ya pesa ya Tanzania ikilinganishwa na dola.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba hii ni moja ya sababu inayotufanya tukae nao sana wafanyabiashara na katika mazingatio tunayoyazingatia hili zaidi. Kwa sababu inajitokeza kwamba pale bidhaa zinapopanda kufuatana na kupanda au kushuka kwa pesa ya Tanzania ikilinganishwa na dola lakini inapoteremka huwa hawashushi bei za vyakula.

Tunapojadiliana nao kuhusu suala hili Mhe. Mwenyekiti, wanasema kwamba bei ya vyakula inapokuja inakuwa tayari imekuja kwa bei ile wakati shilingi thamani yake ikilinganishwa na dola ya Kimarekani ilikuwa iko juu. Kwa hivyo, wanasema kwamba ni bora waendelee kuuza kwa bei hiyo hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kwa kuwa suala hili sote tunalifahamu na tumeanza kulifanyia kazi basi atuachie tuendelee kulifanyia kazi sisi na wafanyabiashara. Pia nimhakikishie kwamba mwelekeo mzuri upo kwa sababu wafanyabiashara wetu si wakaidi hata hivyo.

Nam. 35

Ujenzi wa Studio ya Kurekodi Muziki

Mhe. Hamza Hassan Juma – Aliuliza:

Hivi karibuni tumesikia kwenye vyombo vya habari kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar ameagiza kuanzishwa kwa ujenzi mpya wa Studio ya Kurekodia Muziki. Wazo hili ni zuri na litaleta faraja kwa wasanii wetu wa hapa Zanzibar na Tanzania nzima kupata kitu kilicho bora.

(a) Je, Mhe. Waziri, suala hilo ni kweli.
(b) Kama kweli Wizara yako imechukua hatua gani.
(c) Ujenzi huo tuutarajie kuanza lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:
Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba Rais wa Zanzibar ameagiza kujengwa studio mpya ya muziki.
(b) Katika kutekeleza agizo hilo, Wizara yangu imechukua hatua ya kuliingiza suala hilo katika miradi itakayotekelezwa katika mwaka huu wa fedha na hivi sasa tunasubiri kupatiwa kiwanja kutoka Idara ya Majenzi ili kutimiza azma hiyo.
(c) Ujenzi huo utaanza mara tu tutakapofanikiwa kupata kiwanja cha kujenga studio hiyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri akijibu kwamba ni kweli Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliagiza kwamba ijengwe studio ya kisasa itakayoweza kukidhi mahitaji hasa ya wanamuziki wetu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimuulize Mhe. Waziri. Kama alivyosema kwamba wameshaingiza katika mchakato wa bajeti inayokuja. Je, wametenga kiasi gani katika bajeti hiyo, lakini vile vile studio hiyo itajengwa katika eneo gani.

Lakini swali (c) kuna mtaalam alitoka Uingereza alikuwa akifanya *research* ya studio zilizokuwepo Afrika kwa ajili ya kurekodia muziki. Miongoni mwa studio ambazo alizigundua kwamba ni bora katika bara la Afrika ni mbili, moja iko Ghana na moja ni

studio ya Zanzibar. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kujenga studio nyengine kutazidi kuigharimu serikali kuliko kukarabati studio tuliyokuwanayo ambayo katika muziki alizorekodi huyo mtaalam alipata *CD* yenye sauti nzuri sawa sawa na hizi zinazorekodiwa Ufaransa, Ujerumani na Uingereza.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Rais mwenyewe aliahidi na hatuwezi kumkiuka tukafanya vyenginevyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuhusu tathmini ya pesa siwezi nikamwambia Mhe. Mwakilishi ni kiasi gani.

Hoja za Serikali

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe katika orodha niliyonayo hapa nina jumla ya watu watatu. Wa kwanza ni Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, wa pili ni Mhe. Hamza Hassan Juma na wa tatu ni Mhe. Hassan Hamad Omar. Bado nafasi iko wazi kwa wajumbe ambao wanataka kuendelea kuchangia tunawaomba watumie fursa hii. Tutaanza basi na Mhe. Hamza Hassan Juma ili tuendelee na utaratibu wa kuchangia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nikushukuru kunipa nafasi hii nikazungumza machache katika mswada huu wa Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ulipokuwa ukitaja orodha ya majina ulimtaja Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa sasa nilidhani labda ungelivua joho ukaanza kuchangia. Lakini kwa bahati nzuri umeamua kuacha hiyo nafasi na kunipa mimi. Nakushukuru kwa

hilo. Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nataka nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kusikia kilio cha wananchi, kilio cha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi cha muda mrefu kwa kutaka kuwepo sheria hii hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kupitia Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora waliweza kutufanyia semina kwa ajili ya kutu-*alert* kwa hii sheria inayokuja. Katika semina ile tulitoa changamoto nyingi sana kwa upande wa serikali. Sasa tunashukuru Mhe. Waziri alifanya jitihada tulisikia katika vyombo vya habari alikwenda kwa wadau mbali mbali kwenda kupeleka sheria hii ili kuweza kutolewa maoni mbali mbali. Tunashukuru sasa hivi leo umewasilishwa Mswada huu wa Sheria hapa Baraza la Wawakilishi na sisi tuweze kutoa maoni yetu ili uweze kuwa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuona haja kwamba sasa wakati umefika kutuletea mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niende moja kwa moja katika hoja na kimsingi ni kwamba naipongeza sana Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa sababu ukiangalia katika lile *document* lao la marekebisho kwa kweli lilikuwa pengine kubwa kuliko hata huo mswada wenyewe. Kwa hivyo, hii inaonesha kwamba Kamati zetu za Baraza sasa hivi ziko makini katika kuichambua Miswada ya Serikali pale inapokuja ili kuweza kutoa maoni yetu na tunashukuru kwa sehemu kubwa serikali inatusikiliza. Kwa hivyo, naipongeza kamati na vile vile nampongeza waziri kwa kuweza kuona yale maeneo ambayo kamati ilishauri na mengi ambayo wameweza kuridhiana pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala la rushwa. Mhe. Mwenyekiti, rushwa ni adui wa haki na katika vitabu vya dini imeelezewa wazi wazi, tena katika kitu kilichokemewa ni suala zima la rushwa. Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu kuleta mswada huu wameonesha uadilifu mkubwa sana.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, sheria ni nzuri lakini bado wananchi wengi nikiwemo mimi tunajiuliza je, itatekelezeka. Mhe. Mwenyekiti, mswada mzuri sana, vipengele vizuri sana vilivyokuwemo, lakini bado suala linarudi lile lile. Je, sheria hii kwa mazingira yetu Wazanzibari itatekelezeka. Sasa hili ni suala ambalo tunalibakisha kwa ile mamlaka ambayo itakuwa kupewa mamlaka ya kusimamia uzuiaji na utoaji wa rushwa.

Kwa nini nikasema ni ngumu sana. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuweza kuigundua rushwa panataka kazi kubwa sana. Kwa sababu kwanza sheria ya rushwa inavyosema mtoaji na mpokeaji wote wakosa sasa hapo ndio kwenye kishindo. Hao wenzetu watakapotaka sasa kwenda kutafuta huo ushahidi wa nani katoa na nani kapokea sasa hapo ndio kwenye mtihani. Kwa sababu yule aliyetoa anajua akisema mimi nimetoa atachezea pingu, na yule aliyepokea akisema na mimi nimepokea atachezea pingu. Sasa sijui nani katika mazingira yetu ya sasa hivi ataweza kukubali kusema kwamba mimi nimetoa na mimi nimepokea. Bado ni suala ambalo lina kitendawili kirefu sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi naomba mamlaka itakayohusika ambayo Mamlaka ya Uteuzi naomba sana hichi kitengo Mkurugenzi atafutwe mtu ambaye mwenye taaluma ambayo kama ilivyotajwa kwa sababu uteuzi umetajwa katika kifungu cha 4 cha sheria hii. Ateuliwe mtu mwenye hizo sifa zilizotajwa lakini vile vile mwenye uwezo, lakini vile vile ambaye hana hofu ya kufanya kazi yake pale yanapotokezea matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka hii ni nzito naweza nikasema nguvu yake inakaribiana kusema huu ni mhimili wa nne wa dola. Nchi inaongozwa na mihimili mitatu, kuna Serikali, kuna Chombo cha Kutunga Sheria, kuna Mahakama. Lakini nguvu ya Taasisi hii ya Kupambana na Kuzuia Rushwa inaweza ikakaribiana nguvu yake na hii mihimili mitatu. Kwa hivyo, hii Mamlaka ya Kupambana na Kuzuia Rushwa tunaweza tukasema kwamba ni mhimili wa nne katika dola. Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii ikipewa mamlaka yake kamili, ikiachiwa ifanye shughuli zake kwa uhuru, basi nchi itapiga hatua kubwa sana za maendeleo tena katika kipindi kifupi.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia nchi nyingi ambazo zina utajiri mkubwa lakini wananchi wake wana umaskini mkubwa kutokana na tatizo la rushwa. Zimo nchi katika dunia yetu wana mafuta, wana madini na vitu mbali mbali, lakini ukiangalia hali ya umaskini iliyokuwepo katika nchi ile ni kubwa iliyokithiri. Lakini ukiangalia utajiri mkubwa sana waliokuwanao watu ndani ya nchi ile ile kwa kweli unakuwa mkubwa sana. Hii yote inatokanana rushwa kwa sababu rushwa ni adui wa haki, mapato ambayo yalikuwa yaende serikalini yanavuja mifukoni mwa watu wachache na hiyo ndio rushwa yenyewe.

Kwa hivyo, nchi baada ya kukusanya mapato kwa ajili ya maendeleo ya nchi matokeo yake nchi inakusanya mapato kwa ajili ya maendeleo ya watu wachache. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema rushwa ni adui wa haki.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hii mamlaka itakayoteuliwa na wajumbe nadhani kwenye kamati walishauri kwamba huyu Mkurugenzi ambaye atakayekabidhiwa hii mamlaka ya kudhibiti au kuzuia rushwa basi Mkurugenzi yule aje athibitishwe na Baraza la Wawakilishi. Sasa ingawa katiba yetu inasema kwamba Rais halazimiki kufuata ushauri wa mtu. Sasa mimi nadhani itabidi katika sheria zetu sijui pengine baadae katika ufafanuzi tunaweza tukaja tukafafanuliwa labda itabidi pengine kuundwe

kanuni ambayo itakayoelekeza hivyo. Lakini kwa kweli tunaomba sana katika hili tuondoe muhali, tuondoe undugu, tumtafute mtu atakayekuwa na uwezo wa kuweza kukabidhiwa hichi chombo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali yenyewe ndio iliyoleta mswada huu tunaamini wataweza kuwa makini katika kumtafuta mtu ambaye ataweza kukabidhiwa hiki chombo. Kwa sababu chombo hiki kikifanya kazi vizuri basi serikali itafanya mambo yake kwa utulivu bila matatizo yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nitaje baadhi ya aina za rushwa, ambapo kuna baadhi yake zimetajwa. Kuna rushwa za kisiasa. Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii itapata tabu sana hasa wakati unapokaribia uchaguzi. Chaguzi zetu za kiafrika zinatawaliwa na rushwa tena kwa kiasi kikubwa. Sasa hiki chombo kama hakikuwa makini wakati huo basi wananchi watakuja kukidharau, kwa sababu wananchi wataona rushwa zinatolewa nap engine wanaotoa rushwa ni wakubwa na wao wananchi pengine watasema fulani anafanya hivi na wao watakuwa wanaogopa sasa kufanya hiyo kazi. Ndio maana tukasema hiki chombo nguvu zake zinakaribiana na muhimili wa dola.

Je, tujiulize sisi ambao tunaitunga hii sheria tuna usafi kwa kiasi gani. Tumeingia katika mlango wa aina gani mpaka kufika ndani ya hiki chombo cha kutunga sheria, hatukutoa rushwa na kama tulitoa rushwa tuna uhalali wa kuipitisha hii sheria.

Mhe. Mwenyekiti, sisi baada ya kuingia hapa Baraza tulikabidhiwa msahafu na kwa wale wakristo walikabidhiwa biblia, hivyo hapa tunatakiwa tuseme maneno ya ukweli. Wasi wasi wangu hasa katika masuala ya siasa, hivyo hii sheria nadhani ingekuja katika kikao cha mwezi wa Oktoba kabla ya kuingia uchaguzi unaokuja ili hii sheria inapokuja kufanya kazi mtu ajipime huko huko anakotoka. Je, hii sheria mimi haitonikamata. Kwa sababu kuna watu wengine sheria ukishaipitisha basi fomu

mwenyewe haitaki, lakini unapitisha sheria umo ndani ya chombo cha sheria, halafu sheria ile iko nyuma inataka kukutafuna. Mhe. Mwenyekiti, sitaki niseme labda kwamba labda walioingia humu wameingia kwa njia ya rushwa hapana. Lakini nilikuwa nataka kutoa angalizo hilo ili Mhe. Waziri akija basi hebu aniambie ni wakati muafaka wa kuileta hii sheria au tusubiri mwezi Oktoba mwaka 2015 tupitishe sheria ili kila mtu anayetaka kuchukua fomu, kwa sababu ukishachukua fomu hujijui ukishafika huku utakuja kuwa vipi, unaweza ukajakupewa dhamana kubwa katika nchi, unamaliza tu kuapa tayari TAKUKURU anakuja na pingu.

Mhe. Mwenyekiti, hayo tu nilikuwa najaribu kutoa changamoto kwa Mhe. Waziri ili aje kunisaidia mimi nafiri yake maelezo ya kwamba atajiridhishaje kuileta sheria hii ambapo na sisi wenyewe tuna uhakika gani kuwa tuko wasafi kiasi gani. Mhe. Mwenyekiti, kama utaratibu unavyosema kwamba sheria unatakiwa usimtungie mtu. Sheria unaitungia nchi nzima ili kila mtu awajibike katika sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna rushwa za ngono. Rushwa za ngono mara nyingi zimo katika maeneo ya kutafuta ajira, kuna malalamiko mengi ambayo yanajitokeza, lakini hasa katika *private sector*, hasa katika ukanda wa maeneo ya utalii. Mhe. Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi na hii taasisi ambayo itakuja kupewa kazi, kuna baadhi ya kazi tunaanza kuwapa sasa hivi. Taasisi hii nadhani kazi yao ya mwanzo waje waangalie Hansard za waheshimiwa. Mhe. Mwenyekiti, katika maeneo ya ajira hasa katika mahoteli haya ya kitalii kuna tatizo la rushwa za ngono, wengine wanatujia kutulalamikia, tunawaambia nendeni Kamisheni ya Kazi, nendeni polisi na kwengineko kunakohusika. Lakini kutokana na mazingira ya rushwa kama nilivyosema, sio rahisi kwa mtu kusema nimetoa au nimepokea au nimedai rushwa kwa kweli hukumu zake zinakuwa ni ngumu kiasi hicho.

Mhe. Mwenyekiti, kuna rushwa ya kutumia mamlaka vibaya. Mhe. Mwenyekiti, hapa ndipo pale ambapo panatugusa zaidi sisi viongozi, aidha wanasiasa au watendaji wakuu katika serikali ambao wamepewa dhamana ya kusimamia mamlaka fulani. Mhe. Mwenyekiti, suala la kutumia madaraka vibaya kwa kweli ni tatizo. Moja katika kero kubwa ya Zanzibar ambayo ina harufu ya rushwa ni katika maeneo ya ardhi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amezungumza katika ziara zake mbali mbali matatizo ya ardhi yaliyokuwepo katika maeneo yetu na kutokana na uzito wa maeneo haya anawaagiza viongozi washughulikieni wenyewe, kwa sababu anajua na wao wanahusika.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tumekusikiliza sana katika hotuba zako, mara nyingi unapofunga vikao vya Baraza unaeleza migogoro ya ardhi iliyokuwepo Zanzibar, ukiangalia chanzo chake ni rushwa, utumiaji mbaya wa madaraka. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, suala hili nilikuwa naomba sana serikali yetu iliangalie kwa umakini mkubwa. Tunajua serikali watatujibu kwamba umakini wetu ndio tumeleta hii sheria ije ifanye kazi, mamlaka itakayokuja kupewa hiki chombo wao ndio watasema kwamba hapa madaraka yalitumiwa vibaya, hapa watu walikula rushwa na mengineyo. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, malalamiko yapo makubwa sana katika maeneo ya ardhi hasa katika maeneo ya uwekezaji kwenye utoaji wa *lease* na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wenzangu walizungumza kwamba kuwe na tume nyengine ya maadili ya viongozi. Hili ni jambo zuri tena kubwa, nadhani hili ndio litatusaidia zaidi kuweza kutusafisha ili wananchi wetu watuamini kwamba sisi tuko wasafi.

Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru Mhe. Rais wetu, Makamu wetu wao tayari katika suala la kutangaza mali zao wako safi hawana matatizo. Kwa sababu sheria ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kwamba kiongozi yeyote anatakiwa atangaze

mali zake. Lakini sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, watendaji wakuu wa ndani ya serikali na wasaidizi wao, watendaji waandamizi na wao vile vile walikuwa wanapaswa watangaze mali zao ili kutathmini uwezo wa mali ambao zanazimiliki kama zinalingana na ule uwezo wao.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuna rushwa katika mikataba. Ukiangalia hapa hapa kwetu Zanzibar tayari kuna miradi mikubwa lakini upatikanaji wake wa ile miradi basi hata tenda zimeshindwa kuitishwa na wakati mwengine hizo tenda zilizoitishwa basi zimeitishwa katika mazingira ya utatanishi na matokeo yake kuna miradi mingi mikubwa hapa kwetu ambayo mpaka sasa hivi inasuasua na mingine imeanguka kabisa. Kwa hivyo, haya ni matatizo ya dalili na harufu ya hizo rushwa. Kwa hivyo, hii ndio tunaonesha ni namna gani rushwa ilivyokuwa ni adui wa haki.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme rushwa imechangia sana uharibifu wa mazingira. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia mahoteli yetu mengi ya utalii yamejengwa kwa kukiuka sheria ya mazingira. Sheria ya mazingira inasemaje. Sheria ya mazingira inasema kwamba ujenzi katika mahoteli kwenye yale maeneo ya mchanga basi inatakiwa iwe mita 30 kutoka katika fukwe ya bahari. Katika yale maeneo ambayo ni ya mawe ujenzi unatakiwa uwe ni mita 10 kutoka usawa wa bahari.

Mhe. Mwenyekiti, nakuthibitishia na nitaleta ripoti yangu wakati wa mwezi wa April tutakapowasilisha ripoti za kamati. Kamati yangu inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, hili tumelishuhudia ujenzi mwingi wa mahoteli umejengwa kwa kukiuka sheria ya mazingira. Sasa aidha watu kutumia mamlaka vibaya au watu kutumia rushwa kwa ajili ya uharibifu wa mazingira. Mhe. Mwenyekiti, uharibifu wa mazingira unapotokea unaathiri visiwa.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu walizungumza. Leo Kisiwa Panza kule tayari kinaanza kuliwa na maji, kuna makaburi ambayo yalikuwepo miaka zaidi ya 40 au 50 yamo ndani ya bahari sasa hivi. Kuna minazi sasa hivi iliyokuwa wananchi wa kule Kisiwa Panza wanakwenda kuangua nazi basi imo ndani ya bahari, hii inatokana na nini, inatokana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira watu kutumia fukwe vibaya, bahari inahama upande mmoja inaelemea upande mwengine. Kwa hivyo, haya yote yanatokana na harufu ya rushwa. Kwa sababu kama tulivyosema rushwa ziko za aina nyingi. Kuna rushwa za fedha na kuna rushwa za kutumia mamlaka vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna rushwa ya ku-*forge document* za serikali. Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo humu ndani ya serikali yetu huwezi ukaamini kwamba wamefanya watu wenye akili zao. Lakini tusubiri kuna muda utafika tutakuja kuona ni namna gani watu wanavyo- *forge* mpaka *document* za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ukiangalia katika suala la zima la ajira tena namuomba sana Mhe. Waziri wa utumishi wa umma, tuna tatizo kubwa sana la ajira sasa hivi, katika watu kuajiriwa basi watu wengi wana- *forge* vyeti, umakini unakuwa mdogo. Sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, hata unapo-*forge document* ya serikali. Maana yake cheti cha skuli ni *document* ya serikali, sasa unapo-*forge* ili uweze kupata ajira, mheshimiwa hiyo nisehemu ya rushwa.

Kwa hivyo, ukiangalia rushwa Mhe. Mwenyekiti, ina maeneo mengi, ina njia pana na uwanja mkubwa kama hatukuwa makini kwa kweli rushwa itatumaliza. Kwa sababu leo mtu anapopewa dhamana, kama mtu anatakiwa awe na sifa fulani leo mtu ame-*forge* cheti ina maana mtu yule atapewa dhamana ile na atakuwa hana uwezo nayo, matokeo yake badala ya kujenga nchi atakuwa anabomoa nchi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani mambo haya kwa kweli yanahitaji kuangaliwa kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa, naomba sana sheria tunazozipitisha zile *condition* tunazoziweka, basi mimi naomba Baraza la Wawakilishi tusizipinge, hasa katika hawa watu wa ngazi za kuongoza taasisi. Mhe Mwenyekiti, tunasema kwamba mtu ili awe na sifa ya kukabidhiwa dhamana hii, basi awe na elimu ya kiwango fulani. Lakini wakati mwengine kwa ile rushwa ya fikra. Maana Mhe. Mwenyekiti, kuna rushwa ya fikra vile vile. Kuna watu ambao wana sifa ambazo zimetajwa ndani ya sheria wengi na wapo hawana madaraka, lakini matokeo yake tunapokuwa tumemlenga mtu wetu basi tunaanza kuwacha sifa zilizotajwa katika sheria, tunakuja sasa katika uzoefu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano unaweza ukaambiwa kuna takiwa pengine Mkurugenzi wa Usafiri na Leseni anatakiwa awe na shahada ya kwanza. Sio kama hapana watu wenye shahada ya kwanza wenye taaluma ile, lakini utaambiwa kwamba haa! Huyu dereva aliyeendesha gari kwa muda wa miaka 40 atakuwa na uzoefu. Sasa jamani kama tulikuwa tunataka uzoefu wa kufanya ile kazi, kwa nini tukasema awe na shahada ya kwanza katika fani ya Usafiri na Leseni.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kikao kile cha Baraza kilichopita tayari tumeshampa mtu cheo kwa sifa aliyokuwa hana. Sasa hii ndio inayoitwa rushwa ya fikra. Ile kazi inatangazwa mtu mwenye *degree* ya kwanza au mtu mwenye *degree* ya pili, unasahau kwa kuwa una mtu wako unakuja kusema hapana huyu alikuwa anaendesha gari kwa muda wa miaka 30 unampa nafasi ile. Matokeo yake badala ya kufanya kazi nzuri pale anakwenda anaboronga.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nataka niseme kwamba mimi sikutaka kwenda moja kwa moja katika mswada, isipokuwa nilikwenda tu katika kile kifungu cha 4 kuangalia zaidi sifa ya uteuzi. Vile vile kutafuta mtu makini ambaye ataweza

kusimamia hiki chombo chetu. Mhe. Mwenyekiti, tunaamini kikipewa mamlaka yake huru hakiingiliwi na mtu basi naamini nchi yetu itapiga hatua kubwa sana ya maendeleo, kwa sababu kila mmoja ambaye atapewa dhamana ataogopa kufanya vitendo ambavyo ni vya uvunjifu wa sheria.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, hasa Mhe. Waziri atakapokuja kuniambia kuwa sheria hii tunaweza tukaipitisha sasa hivi au tusubiri mwezi Oktoba, mwaka 2015 basi nitamuunga mkono bila ya matatizo yoyote. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi).*

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia mswada wa sheria uliopo mbele yetu wa kuzuwia rushwa na kuhujumu uchumi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nizipongeze juhudi za serikali katika kuwafikishia wananchi wake mema na kutaka kuwasimamia katika mambo yanayohusu haki zao. Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo nashauri turekebishe neno "kuzuwia" na tuweke neno "kupambana". Kwa sababu uwezo wa moja kwa moja kuzuwia ni tatizo, lakini uwezo wa kupambana na rushwa upo.

Mhe. Mwenyekiti, tukizungumza neno "rushwa" ambayo ipo tangu enzi za Mitume, kwa hivyo hapa tukisema katika nchi zetu za Afrika zimejaa rushwa. Mhe. Mwenyekiti, itakumbukwa kwenye mwezi wa 8 na wa 9 tulipata semina ya kuweza kupata uelewa wa sheria hii ya rushwa. Nafikiri wajumbe wako wote walipata semina hii na tulipata kuelewa vizuri na ndio maana leo tuko hapa tunachangia mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, itakumbukwa, naomba nimnukuu Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mhe. Nassor Ahmed Mazrui pale tulipokuwa tukichangia mambo ya semina, akasema je,

viongozi tumeshakuwa tayari na mswada huu kupelekwa katika vyombo vya sheria na akaomba kwanza tujifikirie. Akaomba vile vile magereza yarekebishwe yatiwe *tiles*, kwa sababu ipo siku kiongozi na yeye atalala jela ile.

Kwa hivyo, aliomba katika sehemu za mahabusu zitengenezwe na ziwekwe *tiles.* Ile habari ya kulala mkageuka nyote kwa pamoja iepukwe. Mhe. Mwenyekiti, rushwa ina maana pana sana na kama ina maana pana sana basi imegusa katika sehemu zote. Lakini kama alivyotangulia kusema mwenzangu, huyu mtu wa mamlaka au Mkurugenzi atakayepewa Mamlaka ya usimamiziwa rushwa ni lazima awe makini sana, isiwe ni chanzo cha kujipatia mapato, kwa sababu mswada huu umekuja kuwakomboa wanyonge na isiwe sababu ya kutaka kuwakandamiza zaidi wanyonge wa nchi hii, kwa sababu sehemu zetu zote zimetawaliwa na rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu kifungu cha 53 ukurasa wa 228, naomba nikinukuu. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinasema;

Kifungu cha 53

> "Mtu yeyote ambaye kwa makusudi atakwenda kinyume na nafasi yake ya kazi katika kutekeleza au kushindwa kutekeleza jambo lolote kwa mujibu wa sheria ikiwa ni miongoni mwa utendaji wake wa kazi, au atatumia nafasi yake kwa lengo la kujipatia faida isiyohalali yeye mwenyewe au kwa mtu mwengine au taasisi atakuwa amefanya kosa".

Mhe. Mwenyekiti, tukizingatia kifungu hicho basi inasemekana mtu anakosa haki yake mwenyewe ya kimsingi, basi haki yake mwenyewe anainunua kwa sababu ya rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia sehemu zetu za huduma. Kwa mfano kama barabarani, hospitalini, michezo, bandarini na hata

Misikitini sehemu zote hizo zimetawaliwa na rushwa. Tukija barabarani askari wetu hawa wanaweza kuwacha jambo ambalo linasababisha ajali, lakini akaweza kupiga mkono gari ambayo anaweza kupata maslahi yake tu, hili ni tatizo.

Sasa tunamuomba Mhe. Waziri awe makini na jambo hili, sio jambo la mchezo. Nilisema pale mwanzo kama tubadilishe kipengele hiki, hatuna uwezo wa kuzuwia rushwa, lakini tuna uwezo wa kupambana na rushwa, kwa sababu rushwa ni jambo gumu sana na sisi viongozi nasema tunashiriki katika mambo haya. Tujiweze kwanza sisi viongozi ndio tutaweza kufanikiwa katika hii rushwa, la kama hatujajiweza sisi basi hatuwezi kufanikiwa katika hii rushwa. Kwa sababu sisi viongozi Mhe. Mwenyekiti, tunalindana na kama tunalindana basi hatuwezi kufanikiwa na jambo hili hata siku moja. Itakuwa tumo kutunga sheria hapa na hatimae hazifanyikazi vizuri. Maana ya sheria ni kupata usimamizi mzuri ndio sheria hiyo inakuwa kali na inatisha na itafanyiwa kazi, bila ya hivyo hatuwezi kufika popote. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri awe makini na jambo hili, tumefika katika sehemu ambayo sasa tunakwenda kuwatafutia wananchi wetu haki.

Mhe. Mwenyekiti, mfano hospitalini mtu anaweza kwenda na mgonjwa yuko mahututi na akawa yuko kwenye foleni na akakosa haki yake ya kuhudumiwa, lakini mtu mwenye uwezo akahudumiwa na akamuacha mtu aliyekuwa hana uwezo pale pale, hiyo ndio rushwa hakuna sababu ya msingi ni rushwa imetawala kabisa. Maskini ya Mungu mtu anaweza kutoka alfajiri anakwenda hospitali akapanga foleni akawa mtu wa mwanzo, kwa bahati mbaya anaweza kuwa mtu wa mwisho hajapata huduma, hiyo ni rushwa. Lakini wenye uwezo wakifika pale hawachukuwi hata dakika mbili wanahudumiwa, hili ni tatizo na ni rushwa kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, hata tukija katika upande wa michezo basi pia kuna rushwa, ndio maana Zanzibar hii vipaji vyetu vya michezo havikui kwa sababu ya rushwa. Sasa ikiwa tumekusudia kufanya kweli basi tusimame tufanye kweli tusidanganyane.

Mhe. Mwenyekiti, nitowe mfano wa ndani ya Jimbo langu la Kisiwani Kojani, kuna timu inaitwa *shamba sports club*, hii timu ina mpira mzuri tu na wenzangu waliokuwa katika kamati walihudhuria, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alikuwepo na aliiona ile timu uwezo wake. Mwaka jana katika kombe la maridhiano walipambana na timu ya jamhuri katika *final* na kiliputwa vizuri sana pale, lakini kwa sababu ya rushwa timu ile mara hii haikushiriki kwa kufanyiwa maonevu. Basi kama Mhe. Waziri tumejipanga vizuri tunaomba na sehemu hiyo ifikiriwe kweli kweli. Maana timu ile ilizuiwa kushiriki michezo kwa sababu ya rushwa, mpaka wanapambana na polisi hivi hawakubali ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, hata tukija katika sehemu za bandarini, huko ndio hasa kumekomaa kwa rushwa. Mhe. Mwenyekiti, jana tiketi zinalanguliwa na jambo hili tumelipitia kelele katika chombo hiki cha kutunga sheria sana. Lakini mpaka leo tiketi zinaonekana mikononi zinalanguliwa, hapo tunapata haki. Tunapozungumza neno rushwa lina maana pana sana kama nilivyoelezea. Kwa hivyo, kuna vitengo mbali mbali vya huduma kama halikufanyiwa mpango hili basi tutakuwa tuna-*fail* siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hata Misikitini watu wanagombana na hata viongozi wa serikali wanafika Misikitini kusuluhisha mambo ya mizozo ndani ya Misikiti. Watu wanagombania nafasi hizo ili tu wakipata misaada Msikitini, mfano kama ng'ombe wametoka Makka wakija hapa, basi ndio wameshajipatia kipato, au mambo mengine mengi. Kuna mizozo mpaka Misikitini ni rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niende mbali sana, nafikiri haya maneno niliyoeleza ni mafupi lakini ya msingi kama yatafuatiliwa na yatafanyiwa kazi basi *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nchi yetu itakuwa nchi ya kupigwa mfano. Lakini nataka nishauri tu, katika kufikia huduma hizi na kuboresha basi ziboreshwe huduma hizi kwa kuwalipa watu mishahara yao vizuri ili waepukane na hili tatizo la rushwa. Maana kama mtu kipato chake ni kidogo basi tutatwanga maji katika kinu hatufiki hata siku moja rushwa haimaliziki. Lakini kama huduma itakuwa ni nzuri na watu wanapata nafasi basi anaweza kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria zilizowekwa. Lakini kama mtu hamiliki hata kumiliki ndani ya nyumba yake katika mlo basi rushwa haiondoki. Ni kweli kama alivyosema Mhe. Mazrui kwamba jela na itiwe *tiles* watakwenda wengi mara hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuboresha mambo haya, mtu anayetenda kosa tusimuonee aibu awajibishwe kabisa, kama tutamuonea aibu itakuwa hatufiki kwa kulindana tu itakuwa hatufiki popote. Mtu yeyote mwenye kujulikana na kosa la rushwa na akapatikana na kutiwa hatiani basi na awajibishwe moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika kulipatia ulinzi suala hili na kulifanikisha, basi hata ulinziwa polisi jamii wana haki ya kufuatilia mambo kama haya. Tunaweza kupata mambo ya kufanikiwa na wakakamatwa wala rushwa moja kwa moja. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huu mfupi, mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kojani naunga mkono mswada huu mia juu ya mia, ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza na mimi niungane kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika hapa tukiwa na afya njema kwa ajili yalengo la kupanga mambo ambayo yataendesha nchi yetu vizuri.

Pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza na mimi kutia baraka zangu katika jambo hili muhimu ambalo liko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niipongeze sana serikali kwa kuleta mswada huu ambao nadhani niseme kwamba pamoja na kuwekwa sheria sasa tutakuwa tuna silaha mkononi ya kupambana na kilema, maana yake rushwa ni kilema kilichozoweleka muda mrefu sana. Kwa hivyo, pamoja na hii sheria lakini nitowe angalizo kwamba sasa serikali inatangaza vita vikubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi labda nijiulize kama ambavyo wenzangu wamejiuliza, sijui kama tutaweza. Maana yake tumetunga sheria hapa Mhe. Mwenyekiti, ni ya jambo rahisi sana lakini limetushinda, mpaka leo mimi hukaa nikawa nauliza jamani serikali mnafanya nini.

Mhe. Mwenyekiti, tulitunga sheria ya kuwalinda wanyama hapa, lakini hakuna mtu ambaye hashuhudii wanyama wakiadhibiwa mbele ya macho yetu na macho ya serikali

Siku moja nilimuuliza Mhe. Waziri hapa ni watu wangapi wameshtakiwa kwa kuadhibu wanyama, hana hata mmoja. Sasa ikiwa jambo lile dogo limetushinda sijui kama hili tutaliweza. Lakini kutunga sheria ni hatua moja na kuifuata ni hatua ya pili. Kwa hivyo, tuendelee kutunga.

Mhe. Mwenyekiti, rushwa ni adui wa haki, watu wengi wanakosa haki kwa sababu ya rushwa. Kwa hivyo, nadhani nia ya serikali kwa sheria hii ni kufanya wale waliokuwa wakikosa haki zao kwa sababu ya rushwa, basi ikiwa sheria hii itatekelezwa watu watapata haki zao.

Kwa kweli jambo hili la rushwa Mhe. Mwenyekiti, hata Dini yetu ya Kiislamu imelitaja sana nakumbuka maneno ya Mwanafalsafa mmoja Mashuhuri sana katika Dunia Muhammad Bin Abdillah aliwahi kusema "*Laana llwahu Raashi walmurtashi*" tafsiri yake siijui vizuri, lakini mashehe wanaweza kunikosoa.

Lakini nafikiri alikusudia kusema kwamba Mwenyezi Mungu amewalaani wanaokula rushwa na wale watoaji rushwa, yaani wote wawili. Sasa mtu kama huyu akitamka jambo kama hili basi jambo hilo ni baya sana, ndio maana nikasema naipongeza serikali sana kwa kuliona hili.

Mhe. Mwenyekiti, mambo kama haya yakiendelea kuwepo katika nchi mara nyengine yanaweza kutusababishia matatizo makubwa, hata wakati mwengine huwa ile amani ya Mwenyezi Mungu inapungua katika nchi. Kwa mfano, masuala ya rushwa, riba ambayo tumeyazoea sana, lakini ni mambo mabaya kweli, shirki, ufuska pamoja na mambo mengine.

Sasa mambo kama haya yakichanganyika Mhe. Mwenyekiti, basi wakati wowote nchi itarajie kukumbwa na mabalaa na tayari yameshatokea katika nchi za wenzetu na tumuombe Mwenyezi Mungu atusaidie yasitokezee kwetu, lakini ni hatari sana.

Mhe. Mwenyekiti, rushwa imeenea katika maeneo mengine, nafikiri Mamlaka itakayoundwa kwa ajili ya kudhibiti haya mambo ya rushwa, basi iangalie maeneo mengi. Kwa mfano, katika maeneo ya kutoa ajira kwa kweli imezoeleka sana hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, yaani ajira ni tabu sana kupatiakana kama mtu hajapita mlango wa nyuma, wakati mwengine kama mtu anaomba cheo.

Lakini nimefurahi sana kuona kifungu cha 56 ambacho kinazungumzia rushwa kuhusu masuala ya uchaguzi. Mhe. Mwenyekiti, ni hatari sana. Kwa kweli hivi sasa imezoeleka sio

mtu anatoa rushwa, isipokuwa anadaiwa hasa rushwa, yaani hivi sasa kama mgombea hajanyosha mkono wake, basi ni tabu sana kupata kura kwa wananchi. Kutokana na hali hiyo, ndio nimefurahi kwamba adhabu sasa itawakuja wale wanaotoa pamoja na wale wanaopokea rushwa, yaani wote wawili.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine tunaweza kufika pahala tukapata kiongozi si kwa sababu ya sifa zake, isipokuwa ni kwa fedha zake, yaani amemudu kuwa na fedha nyingi za kuwapa watu na kuweza kupata kura nyingi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia sana watu kunyimwa haki Mahakamani kwa sababu ya rushwa, hili ni jambo baya sana. Kwa kweli hakuna chombo ambacho tulikitarajia kiwe kinatafsiri ni yupi mwenye haki kama Mahakama, sasa tumefika pahala Mahakamani nako rushwa inatembea, hivyo mtu anafika pahala anakata tamaa kabisa na mambo haya yapo.

Mhe. Mwenyekiti, rushwa inatumika sana katika masuala ya kukwepa kodi. Kwa mfano, Bandarini kule pengine kontena ambalo lilitakiwa lilipiwe shilingi milioni 100, basi kuna *negotiations* zinafanywa na mtu analipa shilingi milioni 20 na kutoa kontena lake, tayari ameshatia hasara watu. Kwa hivyo, nchi hii katika misingi kama hiyo itakuwa haiwezi kufika kwenye hatua za maendeleo. Sasa hayo ni mambo ya jumla.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye kifungu cha 4 ambacho wenzangu wengi wamekigusia. Kifungu hiki kinatengeneza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa.

Lakini ukienda kwenye kifungu cha 7(1) na (2) vinataja sifa za mtu anayefaa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa pamoja na Naibu wake, yaani pale kuna sifa mbili tena wote wawili wawe na sifa hizo.

(a) Mzanzibari, mwenye taaluma angalau shahada ya kwanza ya sheria.

(b) Uzoefu kwa kipindi kisichopungua miaka saba katika fani hiyo".

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wengi wametoa mawazo yao, lakini na mimi nataka niongeze kidogo pamoja na sifa hizi, pia huyo atakayechaguliwa basi iwekwe hasa kwenye sheria asiwe mtu mwenye tama.

Mhe. Mwenyekiti, usijekushangaa hata kidogo kama atapatikana mtu mwenye tamaa ya mambo makubwa ameyaweka mbele, akachaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kudhibiti Rushwa na Kuhujumu Uchumi, lakini akawa yeye ndio chemchem ya rushwa na kuhujumu, kwa sababu ya tamaa yake. Kwa hivyo, kiwekwe wazi wazi na watu wamo wasiokuwa na tamaa wanajulikana.

Kwa mfano, unaweza kumkuta mtu amekaa madarakani muda mrefu kweli sana, lakini hamiliki zaidi ya ile nyumba yake mmoja ya kuishi na pengine hiyo nyumba ukiangalia amefadhiliwa na mtu. Mhe. Mwenyekiti, unaweza kumkuta mtu amechaguliwa kuongoza idara au taasisi fulani haijafika miezi sita ukimuhesabia anazo nyumba 6 au 7 ama 8, huyu hafai ni mtu wa tamaa.

Kwa maana hiyo, lazima sheria hii iweke wazi wazi ni mtu anafaa kuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa asiwe mtu wa tamaa namuomba sana Mhe. Waziri alizingatie hili.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 10(1) naomba kunukuu.

Kifungu cha 10(1) cha mswada kinaeleza hivi:-

> “Mamlaka itaweka au itaagiza kuwekwa vitabu na kumbukumbu sahihi za hesabu kwa mujibu wa mapato, matumizi, mali na madeni yake”.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nimefanya wasi wasi kidogo kwamba Mamlaka itaweka au itaagiza kuwekwa, hili neno itaagiza kuwekwa ndilo ninalowasi wasi nalo, kwa sababu Mamlaka yenyewe itamuagiza nani aweze zaidi ya kuweka yenyewe.

Kwa hivyo, ninaomba hili neno “au itaagiza kuwekwa” litolewe na kubakia na ibakie Mamlaka itaweka vitabu na kumbukumbu sahihi za hesabu, kwa sababu mapato na matumizi yamo kwenye hii mamlaka. Kwa hivyo, kama ni hivyo, taasisi yoyote ambayo inayo mapato na matumizi ndiyo yenye wajibu wa kuweka kumbukumbu, sasa hii itaagiza imuagize nani?

Kifungu cha 12 cha mswada pia kidogo nina tatizo labda hakijaandikika vizuri naomba kinachozungumzia masuala ya Hesabu za mwaka za Mamlaka zitatayarishwa na kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo langu lipo hapa “zitatayarishwa na kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali”. Kwa hivyo, nasema kwamba huyu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali sio kazi yake kutayarisha hesabu za mamlaka hii.

Sasa inawezekana hivi inavyosomeka sivyo ilivyokusudiwa, lakini ni tatizo la kiuandishi. Kwa hiyo, mimi niliandika vyengine na kusema nipendekeze hivi na kama itakubalika, basi Mhe. Waziri abadilishe hiki kifungu kidogo, ili kiweze kusomeka vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba kifungu cha 10(2) cha mswada kisomeke hivi "Mamlaka itatayarisha hesabu za mwaka na hesabu hizo zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au Mkaguzi mwengine ambaye atathbitishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali".

Kwa hivyo, hapo itaondosha ile wasi wasi wa kuja kutakiwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yeye mwenyewe atayarishe hizi hesabu hizi, ambazo hatimaye anatakiwa yeye mwenyewe azikague, kwa sababu hiki kifungu hakina hata koma, kwani ile koma inaweza kubadilisha maana sana. Hivyo, naomba Mhe. Waziri azingatie hayo marekebisho kidogo.

Vile vile kifungu cha 12(1) kuna jambo niliona ni tofauti kidogo na *system* za kimahesabu, kifungu hiki kina mambo mawili Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Kifungu cha 12(1) cha mswada kinaeleza hivi:-

"Mkurugenzi Mkuu atatayarisha au ataagiza kutayarishwa …"

Mhe. Mwenyekiti, nadhani yeye *Accountant Officer* wa Mamlaka hii, haidhuru sheria haijamtaja moja kwa moja. Lakini tulivyozoea Mkuu wa Taasisi hii mara nyingi ndio anayekuwa *Accounting Officer*, kwa hivyo yeye mwenyewe ndiye atakayekuwa *Accounting Officer*. Sasa kama ni hivyo, basi asiagize isipokuwa atayarishe mwenyewe, yaani yeye na watu wake wa ndani pale. Kwa maana hiyo, hii "au ataagiza kutayarisha" pia itoke.

Suala jengine ambalo nimeliona kwenye kifungu hiki cha 12(1), Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

> "Mkurugenzi Mkuu atatayarisha au ataagiza kutayarishwa ripoti ya mwaka kwa kila mwaka wa fedha na kuiwasilisha kwa Waziri ndani ya kipindi miezi minne baada ya mwisho wa mwaka wa fedha".

Mhe. Mwenyekiti, tatizo langu lipo hapa chini ndani ya kipindi cha miezi minne baada ya mwisho wa mwaka wa fedha. Kwa kweli tulivyozoea hapa Zanzibar taasisi zote zinataarisha mahesabu yao miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha na wala sio miezi minne.

Vile vile kuna *queer* ambazo ameziandika *CAG* kwa wale ambao wamekiuka ile miezi mitatu. Mara nyengine tumekuwa tukipata matatizo sana katika mashirika ya serikali ambayo hawafuati *system* hii ya miezi mitatu.

Kwa hivyo, ninaomba kwa sababu tunaandaa sheria hii na kuunda Mamlaka, basi tusiiunde na utata nayo iambiwe baada ya miezi mitatu, yaani baada ya mwisho wa mwaka wa fedha mahesabu yake yako tayari, tofauti yangu isiwe miezi minne na badala yake iwe mitatu, ndivyo nilivyokusudia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo sasa niende kwenye kifungu cha 17(2) naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 17(2) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mkurugenzi Mkuu angalau kila baada ya miaka miwili anatakiwa kuteua mtu au taasisi yenye sifa kufanya tathmini ya utendaji kazi, ili kujua kama viwango vya utendaji kazi vimefikiwa na kama viwango hivyo vinatosheleza".

Mhe. Mwenyekiti, wasi wasi wangu ni kwamba hii dhamana ya kuteua mtu au taasisi itakayofanya tathmini akiachiwa yeye

mwenyewe Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka, nafikiri hwenda haki isitendeke. Hofu yangu siku moja Mkurugenzi asijeakawa amefanya manyago katika mamlaka yake, halafu akamtafuta mtathmini ambaye ni rafiki yake na kumwambia afanye tathmini, ili amfichie yale mambo ambayo yamo mule ndani ya taasisi.

Sasa naomba sana kazi hii asipewe Mkurugenzi, isipokuwa kazi hii apewe mtu mwengine yeyote au kama itakuwa Mamlaka iliyomteua Mkurugenzi, basi mamlaka hiyo ndio iteue mtathmini wa kuifanyia tathmini hii mamlaka. Lakini akiachiwa yeye kwa kweli ikiwa hana nia njema na hayo ni mambo ya kawaida Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu siku nyengine mtu anakuwa na nia njema na mara nyengine hana.

Kwa hiyo, akiachiwa mwenyewe na ikiwa hana nia njema, basi hwenda ukweli wa utendaji wa ndani ya mamlaka hauwezi kufanyiwa tathmini vizuri. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri ikiwezekana kama atakubaliana na mawazo yangu.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii nami nikaweza kuchangia mawili matatu juu ya Mswada huu wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa leo katika Baraza la Wawakilishi, kwa ajili ya kuchangia mswada huu muhimu sana katika nchi yetu.

Kwa kweli mswada huu tulikuwa tukiusubiri kwa hamu sana tokea hata katika Baraza lile lililopita, kila wakati tulikuwa tukimuuliza Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban utatuletea lini

mswada unaohusiana na masuala ya rushwa. Mhe. Mwenyekiti, hii inatokana na kwamba suala hili lilikuwa likitukera.

Lakini tunashukuru kwamba Serikali hii ya Awamu ya Saba mara baada ya kuingia madarakani imeweza kusimamia jambo hili na leo tunashukuru *Alhamdulillah* Mhe. Waziri anayehusika na masuala haya ameweza kutuwasilishia mbele ya Baraza lako tukufu. Kwa hivyo, tunawashukuru na kuwapongeza wote.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu ni muhimu sana na kama wenzangu walivyotangulia kusema kwamba ni mswada ambao unahitaji kuangaliwa kwa umakini sana.

Rushwa ni adui wa haki na hata wakati mmoja Mwalimu Julius Kambarage Nyerere muasisi wa Taifa hili alisema katika hotuba yake, kwamba nchi yoyote ikiwa inaongozwa kwa misingi ya rushwa au viongozi wake wanaongoza kwa misingi ya rushwa, basi nchi hiyo haiwezi kupata maendeleo hata siku moja. Kwa hivyo, hiyo inaonesha kuwa rushwa ni kitu kibaya.

Mhe. Mwenyekiti, tokea nilipopata mswada huu nimekuwa nikiupitia baadhi ya vifungu na kuona jinsi gani serikali ilivyoweza kujipanga katika kuona kwamba inapambana na rushwa kupitia taasisi yake hii, ambayo tunakusudia kuianzisha.

Kwa kweli moja ya jambo ambalo nimeliona kwenye mswada huu ni kwamba vifungu hivi vya sheria ambavyo kama mswada huu tutaweza kuupitisha, basi ni vyepesi mno, yaani havioneshi kwamba kweli tunayo nia ya dhati ya kupambana na rushwa. Pamoja na Mhe. Waziri madhumuni aliyotueleza hapa ya mswada huu naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Madhumuni ya Mswada huu ni kutunga sheria itakayoanzisha Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar. Mamlaka ambayo itakuwa ni taasisi inayojitegemea

yenye mamlaka ya kupokea na kuchunguza vitendo vyote vinavyoshukiwa kuwa ni vya rushwa. Vile vile ametuelezea Maazimio mbali mbali ambayo yamepitishwa na Umoja wa Mataifa juu ya jambo hili. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sheria ya Mhe. Waziri imekuwa nyepesi mno na wala haiendani na hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, unapokusudia kuondosha jambo au unapolichukia jambo, basi unatakiwa uoneshe hasa kwamba jambo hili nalichukia. Sasa kama unatunga sheria basi ioneshe hasa kuwa sheria hii inakusudia kuondosha jambo hili. Kwa hivyo, kuonesha maana yake ni kuona zile adhabu ambazo zimetolewa katika kuondosha jambo hili.

Kwa mfano, leo kama umekusudia kuondosha jambo kubwa ambalo maelezo yake yameelezwa humu mengi kama vile kuhujumu uchumi, kukwepa kulipa kodi pamoja na mambo mengine. Mhe. Mwenyekiti, ni vyema tuangalie zaidi wafanyaji wa mambo haya wanao uwezo wa kiasi gani? Hivi sheria hii itawaathiri? Hawa nadhani watalipa na baadaye kuondoka kwa ajili ya kuendelea na shughuli zao.

Kwa hivyo, adhabu zilizotolewa humu katika sheria hii haziendani na hali halisi ya makosa yenyewe. Kutokana na hali hiyo, tunasema kwamba adhabu zilizotolewa hazikidhi haja ya jambo lenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, rushwa ni adui wa maendeleo, tumeshuhudia rushwa nyingi sana za aina mbali mbali zikiwemo za ardhi, mali za serikali zinazouzwa ovyo kwa njia ya rushwa, vile vile zimezungumziwa rushwa za ngono pamoja na mambo mengine. *(Makofi)*

Sasa kama kweli Mhe. Waziri tunakusudia kupambana na mambo haya, kama hatukusudii kuondosha njiani kuonekana kwamba

tunayo Sheria au Taasisi ya Kupambana na Rushwa kama Maazimio mbali mbali ya Umoja wa Mataifa yanavyosema, basi kweli tudhamirie kuondosha jambo hili na kila mmoja aogope kufanya jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii imebeba mambo mawili makubwa, ambayo ni unakusudia kuondosha rushwa pamoja na kupambana na wahujumu uchumi. Mamlaka hii ambayo tunakusudia kuianzisha inakusudia kufanya mambo hayo.

Lakini kwenye mswada kifungu cha 2(1) naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 2(1) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Kosa la kuhujumu uchumi" maana yake ni kosa linaloelezwa kuanzia kifungu cha 43 hadi 52 ya sheria hii".

Mhe. Mwenyekiti, naomba tukiangalia kifungu cha 43 cha sheria hii ambacho kinazungumzia masuala ya uhujumu uchumi. Kwa kweli tunashukuru kwamba mswada umeeleza huo uhujumu uchumi maana yake nini. Naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 43 cha mswada kinaeleza:-

Kutumia vibaya mali.

> "Mtu yeyote ambaye kwa kitendo au kuacha kutenda kitendo visivyohalali akajipatia ama yote au hata sehemu huduma ya Serikali, faida au mali ya Shirika la Umma au Kampuni Binafsi iwe ameajiriwa katika taasisi hiyo au vyenginevyo, atakuwa ametenda kosa la uhujumu uchumi chini ya Sheria hii".

Mhe. Mwenyekiti, tuangalie uzito wa haya matendo ambayo huyu mtu ambaye ameambiwa hapa, kwamba atakuwa ametenda kosa la kuhujumu uchumi.

Lakini tukiangalia kuanzia kifungu cha 43 cha mswada tukienda mpaka 52 iliyozungumzwa imeeleza mambo mengi. Kwa mfano, usafishaji wa fedha haramu kifungu cha 49, naomba kunukuu.

Kifungu cha 49 cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mtu yeyote anayejihusisha au kufanya jambo linalopelekea kosa la usafishaji wa fedha haramu chini ya Sheria ya Kuzuia Usafishaji wa Fedha Haramu Nam. 10 ya mwaka 2009, atakuwa ametenda kosa la kuhujumu uchumi chini ya Sheria hii".

Vile vile kuhusu usafirishaji dawa haramu kwenye kifungu cha 50, naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 50 cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mtu yeyote ambaye kwa njia yoyote ambayo ni kinyume na sheria akaingiza, akasafirisha, akatengeneza, akanunua, akauza, akasambaza, akahifadhi, akasimamia, akapeleka au akagawa kwa kutumia mtu mwengine dawa ya nakotiki au saikotropiki au akaahidi kutoa dawa ya nakotiki au saikotropiki, atakuwa amefanya kosa la kuhujumu uchumi chini ya Sheria hii".

Kwa hivyo, ukiangalia takriban vifungu vyote kama ilivyoelezwa humu vinazungumzia kosa la kuhujumu uchumi wa nchi.

Lakini tuiangalie adhabu na nimejaribu kupitia hapa vifungu vyote, kwa kweli hakuna adhabu iliyowazi juu ya vitendo vya wahujumu uchumi, yaani hamna adhabu iliyowazi, isipokuwa kifungu cha 61 cha sheria hii, naomba kunukuu.

Kifungu cha 61 cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mtu aliyepatikana na hatia kwa kosa lolote chini ya sheria hii, ambalo adhabu yake haikuelezwa, basi atalipa faini isiyopuungua shilingi milioni moja au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili au adhabu zote mbili, ya faini na kifungo".

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wa Kamati wao wamejaribu kufanya iwe bora zaidi na wao wameongeza neno "isiyozidi shilingi milioni 5", lakini ile isiyopungua shilingi milioni moja wao wameona ni *reasonable* au kifungo cha kipindi kilichopungua miaka miwli na kisichozidi miaka mitano, yaani wao wamepunguza ile kwamba Hakimu asije kwenda mbali zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, adhabu hizi hazilingani na kosa lenyewe la uhujumu uchumi. Kwa sababu hapa tumeshapitisha sheria mbali mbali ambazo zinazungumzia baadhi ya makosa kama haya, usafirishaji wa fedha haramu, usafirishaji wa dawa haramu. Sasa sijui Mhe. Waziri Sheria hii au vifungu hivi vimezingatiaje sheria zile ambazo tulizokuwa tumeshazipitisha, adhabu zake.

Mimi nakumbuka Mhe. Mwenyekiti, wakati wa Mwalimu Nyerere kulikuwa kuna *operation* ya uhujumu uchumi na ulikuwa unaongozwa kwa wakati ule na hayati Moringe Sokoine. Ukipatikana na hatia ya uhujumu uchumi adhabu yake kwa wakati ule ilikuwa ni miaka mitano. Sembuse sasa hivi tunavyokwenda miaka miwili halafu unakusudia kuondosha tatizo la uhujumu uchumi katika nchi.

Hapa panahitaji marekebisho na mazingatio juu ya kosa la uhujumu uchumi katika nchi. Ambapo kuna baadhi ya mambo mengine ya msingi yamehusishwa humu kama haya niliyoyazungumza madawa haramu na mambo mengine, kwamba ni kosa la uhujumu uchumi na adhabu ndio kama tunavyoona. Hili linahitaji kuzingatiwa. Kama hiki kifungu cha 43 kilivyoeleza hapa, humu mnahusisha maana yake ni suala la kutumia vibaya mali za umma au mtu kujipatia mali kwa njia isiyo halali. Ni kosa na haya ni matatizo ambayo tunayo sasa hivi. Kuna watu wanafanya kazi katika taasisi za fedha mwaka mmoja tu unamkuta ana kila kitu, ana nyumba tatu, ana magari, ana kila kitu. Hii ni kutumia vibaya mali za umma yakiwemo madaraka yenyewe.

Kwa hivyo Mhe. Waziri sheria ni nzuri na kwa sababu imetoa *definition* kila mmoja anajua ala kumbe nikifanya hivi maana yake nahujumu uchumi, lakini adhabu zilizotolewa hazilingani na kosa lenyewe. Kwa hivyo kama kweli tumekusudia kupambana na wahujumu uchumi katika nchi hii ili nchi yetu iweze kupata maendeleo basi naomba uzitizame hizi adhabu ambazo zipo zimetolewa.
Mhe. Mwenyekiti, suala la rushwa kwenye *interpretation* rushwa hapa imesemwa maana yake ni:-

(a) Kosa lililoelezwa kuanzia kifungu cha 36 mpaka 42 na vifungu cha 53 mpaka 58 vya sheria hii.

Sehemu ya Tano ya sheria hii ambapo ndio kifungu hichi cha 36, kilichoanza kuelezea kinazungumzia makosa. Rushwa katika uwakala, tatizo, kushawishi katika kutoa ushauri, tatizo, mgongano wa maslahi hilo nalo ni tatizo katika nchi yetu hii, kukwepa kulipa kodi hilo nalo ndio tatizo hasa, na mambo mengine.

Sheria kweli imetueleza nini rushwa, kwa sababu tafsiri mara nyingi tulikuwa tunashindwa kutoa tafsiri lakini sheria *Alhamdulillah* tunashukuru imeeleza ni nini rushwa kwa mujibu wa sheria hii. Lakini tatizo bado lipo kwenye adhabu ya makosa haya kwa mfano kifungu cha 44 cha sheria kinasema:

> "Kinasema kwamba mtu yeyote ambaye kwa kitendo au kuwacha kutenda anakusudia kukwepa kulipa kodi au anasaidia katika kukwepa kulipa kodi kwa njia yoyote kati ya hizi zifuatazo"

Zimetajwa hapa kwamba atakuwa ametenda kosa. Hii bado itakuwa tunakwenda katika hali ya uhujumu uchumi. Lakini nilikuwa nataka kulizungumzia zaidi *specific* hili suala la kukwepa kulipa kodi. Nakumbuka Mhe. Mwenyekiti, Sheria tuliyoipitisha ya ZRB, mtu anaekwenda kodi au mfanyabiashara anayefanya mipango ya kukwepa kulipa kodi au akibainika kwamba halipi kodi basi analipa faini ya dola milioni mbili. Hebu tuziangalie kiasi gani hizi za fedha. ZRB wakikubaini kwamba umefanya ujanja katika kulipa kodi ya serikali, adhabu yako ni dola milioni mbili. Sasa hebu tuziangalie na hizi adhabu zilizokuwepo. Maana badala ya kwenda mbele sasa tunarudi nyuma.

Mheshimiwa mimi nakubaliana na sheria, maelezo yaliyotolewa, muundo, lakini nahitilafiana katika suala zima la adhabu ambazo zimetolewa. Kwa mfano tunapozungumzia rushwa ya ngono. Adhabu iliyotolewa juu ya rushwa ya ngono, ukiangalia sheria ya rushwa ya ngono kwa tafsiri ya hii, athabu yake ni miaka 30 jela. Mtu akitiwa hatiani kwa rushwa ya ngono anatakiwa aende jela si chini ya miaka 30. Hetu tuiangalie hii sheria yetu ambayo imeweka ngono kwamba sehemu ya rushwa na adhabu ambazo zimetolewa. Sasa tunakusudia kuondosha rushwa ya ngono au tunataka kuimarisha rushwa ya ngono. Kwa sababu tunatoka kule ambapo tulipofika halafu tunarudi chini.

Mhe. Waziri nadhani ukajipange vizuri katika kuangalia adhabu ambazo tayari zimeshatolewa katika sheria zilizokuwa zimepita. Hii sheria ambayo unatuletea sasa ambayo imetoa tafsiri ya makosa yenyewe na umeeleza chini ya sheria hii. Sasa sijui kama sheria hii imezifuta zile sheria nyengine hatujui. Lakini umeeleza kwamba sheria hii ukifanya hivi ukifanya hivi ni kosa kwa mujibu wa sheria hii. Kwa hivyo adhabu zinahitaji kuangaliwa kwa umakini sana, ili tuone kwamba lile lengo lilokusudiwa na serikali la kupambana na rushwa linafikiwa. Sote tunakubaliana kwamba rushwa ni adui wa haki, rushwa inadumaza maendeleo ya nchi. Sote hapa ni mashahidi juu ya matendo ambayo yanafanyika. Ni lazima tukusudie kwea makusudi.

Lakini mbali ya hiyo pia sheria hizi zifanye kazi, isiwe tunakaa hapa tunatunga sheria lakini utekelezaji wa sheria wenyewe hauonekani. Mhe. Waziri tutakuja kukuuliza hapa tokea tumepitisha sheria hii ya kupambana na rushwa ni watu wangapi wamepelekwa Mahakamani na adhabu zilizokuwa zimetolewa. Kwa sababu haya matendo yapo mengi tu. La kama tunakusudia kufanya tu kwamba na sisi tuonekane tumefanya, sheria tunayo, lakini hakuna sheria zinazochukuliwa haya basi twendeni. Lakini kama kweli tupo *serious* katika kupambana na masuala haya, basi ni lazima sheria hizi tunazozipitisha tuhakikishe taasisi zinazosimamia basi sheria iwe inachukua mkondo wake.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengi yapo wazi, humu yametajwa mambo mengi ambayo yamezungumziwa kwamba mtu akipatikana na mali ambayo haina maelezo, juu ya upatikanaji wake, na ukiangalia kipato chake, basi mali hiyo kwa mujibu wa sheria hiyo ni kosa. Mali haijulikani umeipataje na zipo mali nyingi tu hapa, naamini ukimuuliza mtu mali hii umeipataje atashinda kuitolea maelezo. Sasa tunataka taasisi hii kitengo chake cha uchunguzi kifanye kazi na hatua ziweze kuchukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikubaliane na mawazo ya wenzangu waliotangulia mwanzo. Nilikuwa namsikiliza Mhe. Jussa kwa umakini sana wakati akichangia, nikubaliane na mawazo kwamba sasa tubadilike ili twende kwa wakati, wala tusione tabu, wala tusione kwamba tunaingilia uhuru wa Mhe. Raisi, ndio hali ilivyo ndio dunia inavyokwenda. Wenzetu Tanganyika wameshaanza kuna baadhi ya uteuzi wa Rais unathibitishwa na Bunge. Ile kwanza inasaidia au inamsaidia yule mtu aliyepewa madaraka yale kujua kwamba kwa kuwa nimethibitishwa na chombo hiki nikifanya vyenginevyo vyovyote chombo hiki kinaweza kupiga kura kutokuwa na imani naye. Na kwa sababu tutakuwa tunamuangalia utendaji wake.

Kwa hivyo Mhe. Waziri nadhani ushauri huu uukubali, wala usione tabu kwamba mkurugenzi Mkuu huyu wa kupambana na rushwa akiteuliwa na Rais aje athibitishwe na chombo hiki. Tuanze katika hili na kwa sababu lina umuhimu na ni lazima tuige kutokana na wenzetu na kwa kweli lina umuhimu. Kwa hivyo mimi naungana na wenzangu kwamba Mhe. Rais akifanya uteuzi juu mtu kama huyu basi aje athibitishwe na chombo hiki cha wananchi. Kwa kuwa atasimamia mambo makubwa, mapapa makubwa, mazito mazito, atapambana na mawimbi makubwa, kwa hivyo ni lazima aangaliwe kwa makini, vyenginevyo tunaweza kuanzisha taasisi ya kupambana na rushwa kumbe tukaongeza rushwa zaidi. Badala ya kupambana na rushwa tukamuweka mtu tukamuongezea zaidi.

Siku moja nilikuwa nazungumza na mtu mmoja wa Polisi, nikamwambia mbona wenzetu nyie mmekuwa wepesi sana wa kupata vishawishi vya rushwa, mtu anakamatwa na ushahidi na kila kitu lakini utakapokwenda utaambiwa hakuna ushahidi, hakuna nini. Kumbe watu wanazunguka mlango wa nyuma wanatoa rushwa, mkisha mnashtukia mtu unaambiwa hakuna ushahidi, hakuna nini.

Akasema sisi tunalazimika kufanya hivyo kwa maana tunapomchukua mtu kumpeleka Mahakamani tayari tumeshawatayarishia mazingira ya mlo watu wa Mahakama. Kwa sababu wao wakishakufika kule wanahukumu wanaachia kwa sababu ya rushwa. Kwa hivyo na sisi tunaanza kushika kabisa chetu huku.

Sasa na sisi isije ikawa tunakwenda kwenye utaratibu huo, tunaandaa taasisi ya kupambana na rushwa lakini kumbe tunaongeza rushwa zaidi, tunawayarishia watu mlo. Badala ya kuona rushwa inapungua matokeo yake inaongezeka, hakuna kesi inayokwenda, hakuna ushahidi unaopelekwa Mahakamani, hakuna lolote linaloendelea. Sheria inakuwa ipo pale lakini inalegalega. Kwa hivyo ili tuhakikishe kwamba tunaunda taasisi hii ya kupambana na rushwa kwa makusudi ili tuone kwamba suala la rushwa linapungua.

Mwenzangu hapa Mhe. Hamza amezungumza kwamba rushwa inaharibu mazingira. Na huu ni ushahidi kwamba mazingira yetu yanaharibika kutokana na rushwa. Sheria hazifuatwi kwa sababu ya rushwa. Watu wanajenga mahoteli ovyo kwa sababu ya rushwa. Kama kungekuwa hakuna rushwa, nawahakikishia waheshimiwa wajumbe hoteli zile zisingejengwa kinyume na sheria. Kwa sababu sheria za mazingira zipo, sheria za ardhi zipo, lakini wale wanaosimamia utawakuta wanaanza kusukumiana mpira. Ukija ukimkamata mtu wa mazingira anakwambia huyo aliyefanya hivyo mtu wa ardhi, ukija ukimshika mtu wa ardhi, anakwambia sheria iko hapa huyo kibali cha mazingira. Mazingira yanachafuka kutokana na rushwa
.
Mhe. Mwenyekiti, vyombo au vitu vya serikali vinauzwa ovyo, mali za serikali zinauzwa ovyo kwa sababu ya rushwa. Unapouliza unazungushwa huku, ukipitishwa huku, ukaletwa hivi, unaambiwa maana yake sheria ya kuuza mali ya umma ipo hivi, maana hivi. Maneno meeengi yasiyokuwa na mpango, wakati

sheria zinaeleza wazi. Unapotaka kuuza mali ya serikali yenye thamani fulani unatakiwa utangaze tenda. Unapotaka kukodi, unapotaka kununua, tangaza tenda. Ndiyo sheria ya procurement inavyosema. Leo kumekuwa na maneno mengi, mali za serikali zinauzwa ovyo zenye thamani kubwa, zinauzwa kwa thamani ndogo. Sababu ya rushwa, " rushwa ni adui wa haki". Mali hizi za serikali ni mali za umma, serikali haina mali yake, umma maana yake ni watu wa Zanzibar ndio wenye mali. Sasa ukisema aaah!, maanaake hii ni mali ya serikali. Serikali inahaki ya kiiyuza. Serikali ina mali? Mali zote ni mali za umma.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, sheria hii kama kweli kuna niya iliyokuwa thabiti ya kupambana na rushwa na uhujumu uchumi ifanyiwe marekebisho kwenye adhabu zake. Adhabu zilizokuwemo haziendani na makosa yenyewe. Tunataka ziwe wazi.

Lakini pia katika sheria za nyuma makosa ya Mahakama, makosa ya rushwa na uhujumu uchumi kesi zake mara nyingi zilikuwa zinapelekwa Mahakama Kuu, humu hatujaona. Sasa Mhe. Waziri hebu utakapokuja kufanya majumuisho sheria hii inasemaje juu ya kesi za aina hii. Humu kuna adhabu mbali mbali zilizokuwa zimepangwa.

Kuna adhabu ambazo ziko kwenye Mamlaka ya Mahakama za mwanzo, Wilaya, Mkoa. Kwa mfano adhabu ya milioni mbili, si dhani kama adhabu ya milioni mbili kesi hiyo utaipeleka Mahakama Kuu, sijui mtiririko wa sheria za mahakama, hii ni adhabu ndogo hata Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya wanaweza wakaitoa na humu kwenye sheria imo. Lakini huko nyuma tunakotokea kwamba uzito wa masuala haya ya rushwa na uhujumu uchumi kesi zake zilikuwa zinasikilizwa na Mahakama Kuu. Sasa hebu wakati utakapokuja hapa Mhe. Waziri hebu tupe ufafanuzi juu ya mambo haya, ili tuone sheria yetu inakuwa nzuri.

Serikali inakusudia kweli kupambana na rushwa, sio kuwaridhisha wafadhili au kutekeleza yale maazimio yaliyozungumzwa humo, tupambane na rushwa kweli kweli ili tuweze kupata maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakubaliana na naunga mkono Mswada kwa asilimia kubwa. Mhe.Waziri afanye marekebisho Ishaallah wakati wa majumuisho ili Mswada huu wa Sheria na Sheria iendani na wakati ambao tunao sasa hivi. Ahsante.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nishukuru kwa dhati kunipa fursa hii kuweza kuchangia Mswada huu wa rushwa. Nikushukuru wewe binafsi, nimshukuru Mhe. Waziri, kwa kutuletea Mswada huu pamoja na Kamati yake kwa michango mikubwa ambayo wameiwezesha kuweza kutufikishia suala ambalo ni muhimu katika nchi yetu kwa wakati huu tuliokuwa nao.

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyotangulia kuzungumza wenzangu umuhimu wa sheria hii. Sheria ambayo watu wangi walikuwa wakiisubiri kwa hamu. Wale wenzetu waliokuwepo tangu miaka mitano iliyopita jinsi walivyokuwa wakiupigia kelele miaka mitano iliyopita hadi hivi sasa Mhe. Waziri kaweza kiileta mbele yetu na kuweza kuichangia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kuzungumzia mambo kama mawili matatu. Imani yangi ni kwamba muda mfupi Mswada huu tutaupitisha na tutaunga mkono. Lakini uzito wa suala hili ningeomba kwa dhati kabisa taaluma ya kutosha ikaweza kutolewa kwa wananchi wetu ili mtu kujifahamu kabla ya kuja kutenda kosa pasi na kujielewa. Wizara ifanye jitihada za kutosha ili taaluma ya rushwa na uhujumu uchumi iweze kueleweka ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine tumezungumzia suala la rushwa pamoja na suala la uhujumu uchumi. Lakini kuna tendo ambalo

linaweza likafanyika kabla ya hiyo rushwa yenyewe haijafanyika nayo ni mazingira ya rushwa. Kuna mazingira ambayo yanapelekea kutendeka hilo kosa la rushwa. Kwa sababu lengo la sheria ni kuweza kuwabaini wala rushwa na kuweza kuwachukulia hatua. Lakini yanaweza yakatendeka mazingira ambayo huyo ambaye anatenda kosa la rushwa ukamtia hatiyani. Sasa mazingira ya kuweza kumtia mtu hatiani mtu ambaye anatengeneza mazingira ya rushwa, hili nafikiri Mhe. Waziri angalijaribu kuliangalia kwa makini na kulitafutia mbinu.

Mhe. Mwenyekiti naweza kulitolea mfano suala dogo tu. Kuna masingira mengi ambayo yanaonekana lakini hususan kwa ndugu zetu jeshi la Polisi na hususan *Traffic*. Anaweza akaikamata gari, gari tayari inaonekana kwamba imeshakuwa na kosa kwa mfano imezidisha abiria, lakini baada ya kumtia hatiani dereva anatengeneza mazingira anamwambia akateremshe abiria halafu nifuate kituoni. Sasa kituoni ndio kituoni, wanaingia chumbani, au wanakaa peke yao. Sasa haya ni mazingira ya kutengeneza kosa la rushwa. Sasa suala la kutengeneza mazingira ningeomba likaangaliwa kwa upana zaidi ili baadaye tukaona tunalichukulia hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, chengine ambacho nilikuwa napenda kukichangia katika Mswada huu wa rushwa. Njia za watu wetu kuweza kukwepa hii hatia. Tulipoanzisha sheria ya helment basi watu walitafuta njia ya kukwepa sheria ile. Watu walikwenda kwa madaktari wakatafuta vyeti ambavyo vinathibitisha kwamba mtu yule ana matatizo ya kichwa na hastahiki kuvaa helment. Kumbe ni njia ya kukwepa sheria ili atende kosa pasipo na sababu. Nalo hili katika suala la rushwa kuna vitu tunataka tuviangalie kwa makini, kuna suala la takrima au ahsante. Hili sijui tumeliweka katika pahala gani. Anaweza kukwambia kwamba kafanyiwa kitu mtu basi akasema kampa takrima au kampa ahsante. Hivi vitu tayari vinaanza kutumika kwa kuipindisha hii sheria au kuifunga hii sheria isionekane uzito wake.

Mimi yangu yalikuwa ni hayo, lakini ningemuomba Mhe. Mwenyekiti, uniruhusu nipitie kwenye vifungu viwili vitatu vya sheria hii ili kutoa mawazo yangu katika hii sheria.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 7(a),(b) sifa za Mkurugenzi. Zimetajwa sifa za mkurugenzi anazohitajika kuwa nazo. Mimi nilikuwa na mchango wa kuongeza kifungu (c) hapa kitachosomeka kwamba ili mtu katika sifa zake za kuwa mkurugenzi basi awe muadilifu ambaye hakuwahi kushtakiwa kwa kosa lolote ndani ya nchi au nje ya nchi. Hii ni kutokana na umuhimu wa mamlaka yenyewe vile ilivyo uzito wake.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilikuwa naomba nikipitie kifungu cha 13(1) kazi za Mamlaka. Katika kipengele (a) Mhe. Mwenyekiti naomba yaongezeke maneno 'viongozi wa kiserikali na wakisiasa'. Kifungu hiki ningeomba kisomeke, 'kupokea na kuchunguza malalamiko kuhusu vitendo vya rushwa kwa viongozi wa serikali na wa kisiasa, taasisi za serikali au za binafsi.' Kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti, kitaweka wazi moja ya kazi za Mamlaka ya Mkurugenzi.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba nipitie katika kifungu cha 13 Kazi za Mamlaka. Kipengele cha b(i), ningeomba yaongezwe maneno 'mazingira ya rushwa' hivyo kipengele b(i) kisomeke, Kitendo kinachopelekea kuwepo kwa mazingira ya rushwa, kosa la rushwa au kosa la kuhujumu uchumi.'

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba nimalizie katika kifungu cha 14(3) na (6) maneno chombo ningependekeza yaondoshwe au yafutwe na badala yake ningeomba yasomeke maneno 'usafiri, jengo la taasisi au nyumba' Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kwahani naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika hoja hii ya Mhe. Waziri. Pili niungane na wajumbe wenzangu kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri kwa kuleta Mswada huu, maana umezungumzwa siku nyingi, wale waliotangulia kwenye Wizara ya Utawala Bora, tunasema labda ni mfupa uliokuwa umewashinda. Sasa Mhe. Waziri naona yeye ameuwezo na leo upo mbele yetu tunaujadili na naamini tutaupitisha.

Jengine labda nisema katika hoja zilizotolewa kuhusiana na marekebisho, inaonekana mara hii waraka umekuwa mkubwa sana wa marekebisho. Kweli mimi naomba niipongeze kamati wamefanya kazi kubwa sana katika suala hili.

Lakini pia naomba niwakumbushe Waheshimiwa wajumbe kwamba katika kikao kilichopita hasa Mhe. Rashid Seif aliomba haya marekebisho badala ya kuyaorodhesha tu tuyalete katika mfumo huu ambao utarahisisha mtu kuweza kufuatilia, badala ya yeye mwenyewe kutia irabu basi tumtilie kabisa ili aweze kuusoma vizuri. Kwa hivyo kilichofanyika ndio mara hii tumetia irabu kabisa ili iwe rahisi kuusoma na umesababisha huu waraka wa marekebisho uwe mkubwa sana.

Lakini jengine nirudi kwa Mheshimiwa sahibu wangu ingawa mwenyewe simuoni Mhe. Mshimba , kwanza mimi numuombee aende hija badala ya kwenda Makka *(Kicheko)* maana Maka ni mji lakini hija ndio ibada na wako waliokwenda Maka pengine wamerudi ndio maana tatizo mambo hayakuwa mazuri sana kurekebishika, lakini nadhani waliokwenda hija yamefanikishika. Basi kwa hivyo na mimi naomba nimuombee na yeye aende hija badala ya kwenda Maka.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk yeye aliuliza kuhusu historia ya rushwa, ni kweli tuna historia kubwa sana katika nchi yetu ya sheria ya rushwa ilianza kwa sheria ile Na. 4 ya mwaka 1975 kwa

mara ya mwanzo baada ya Mapinduzi, lakini kabla ya Mapinduzi ukiangalia kwenye sheria yetu ya jinai ile sehemu ya kumi na sehemu ya arubaini ilikuwa inazungumzia masuala ya rushwa. Lakini sheria mahususi ilianza kwa sheria Nam. 4 ya mwaka 1975 ikaja ikarekebishwa na sheria ya Nam. 1 ya mwaka 1976 Nam. 2 ya mwaka 1980 na pia Nam. 2 ya mwaka 1991. Ukweli sheria hii ilikuwa ni kali na iliunda mamlaka lakini baadae mamlaka ile ikafutwa na tukaendelea na utaratibu ambao mpaka leo tunaendelea nao ambao una mapungufu mengi kidogo.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla aliuliza kwa nini chombo kipo tunarekebisha ni kwa sababu kina mapungufu mengi, sheria yenyewe ina mapungufu mfumo wenyewe wa usimamizi pia una mapungufu, kwa hivyo ndio maana sheria hii imekuja kuyaondoa mapungufu hayo katika mfumo wenyewe wa sheria lakini pia katika usimamizi wa sheria yenyewe. Kwa sababu sasa hivi polisi wanachotumia zaidi wanasubiri waambiwe kuna rushwa pahala hasa katika taasisi za serikali, wakati mwengine wanakwenda kila kitu hakipo tena kwa sababu wanasubiri waambiwe ama na taasisi yenyewe ama na waziri. Lakini wenyewe kwa kwenda tu kwa mamlaka yale ya kwenda wakachunguza yamekuwa magumu kidogo au hayako wazi katika sheria au katika mfumo wetu wa sheria uliopo sasa hivi.

Kwa hivyo hayo ni mapungufu makubwa lakini na pia ukiangalia hiyo sheria yetu tunayotumia sasa hivi kuna mapungufu mengi sana, kwa hivyo mimi nadhani hii ni hatua nzuri kwamba tumekuja na sheria ambayo inaweka sawa yale mapungufu ambayo yapo katika mfumo wetu wa sheria sasa hivi.

Lakini jengine ambalo limezungumzwa sana na ambalo naomba waheshimiwa ni vyema tukasikilizana vuziri katika hili, ni suala la uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka na Naibu wake kuthibitishwa na Baraza, dhana yenyewe ni dhana nzuri kwa sababu inaongeza kitu kinachoitwa *cheque and balance* katiba

yetu imetambuwa kuna na *separation of powers* chini ya kifungu cha 5 (a) lakini misingi yake ya *cheque and balance* haikuwekwa bayana katika katiba sasa moja katika jambo ambalo pengine lingeliweza kusaidia kuweka hiyo *cheque and balance* yaani vyombo hivi vyenye madaraka tofauti kuchungana basi wenzetu moja wanalolifanya ni hivi kwamba kuna baadhi ya maamuzi ni vyema yakaidhinishwa na chombo chengine. Suala sasa ni kwamba utekelezaji wake uwe namna gani.

Mhe. Mwenyekiti kama nilivyotangulia kusema kwamba kanuni ya msingi ni kwamba uteuzi wa watendaji katika kazi za utendaji ni mamlaka ya Rais kama kiongozi wa *executive* kwa upande mwengine, hayo yameelezwa wazi kwenye kifungu cha 53 cha katiba. Lakini kifungu cha 5 (a) cha katiba kimeeleza wazi ule mgawanyo wa madaraka, suala ni kujiuliza tu je uteuzi ni mamlaka ya Rais au mamlaka ya *executive* na uteuzi katika *executive position* ni mamlaka ya kiutendaji na sio mamlaka ya *legislature* kwa sababu hayakuelezwa popote katika katiba kwamba hayo ni katika mamlaka yake, unaweza kusema labda ile ya kuchunga lakini hili limeelezwa wazi kwenye katiba.

Mhe. Mwenyekiti wenzetu wanafanya hivyo lakini ndio maana kwa sababu wanajua kanuni hii ni kanuni ya kikatiba ndio maana wanapotaka kulifanya hilo basi hufanywa kwa kupitia katiba yenyewe, yaani huu uteuzi wa watendaji kuthibitishwa na Baraza au na chombo cha sheria katika nchi zote wanazofanya basi utendaji au utekelezaji wa jambo hilo basi hufanywa kwa kupitia katiba.

Kwa mfano mzuri walioanza mtindo huu ni wamarekani tana waliuanza zamani sana tokea walipotunga katiba yao, ukisoma katika *article* kifungu cha pili katika katiba ya Marekani kinachohusu uteuzi wa mabalozi, mawaziri na majaji wale wa Mahakama Kuu yao , Rais kapewa uwezo tena wametumia maneno mazuri tu ku-*nominate and ku-point.* Ku-*nominate*

anafanya yeye mwenyewe lakini katiba yao imeeleza vizuri sana kwamba anapofanya. *appointment* sasa ni lazima apate *approval* ya seneti, lakini hilo limeelezwa kwenye katiba na wameelezwa kwamba ni wepi ambao wapate idhini ya *cement* kwa nini imeelezwa ni kwa sababu yale bado yanabakia ni bado mamlaka yake kama katiba haijaeleza basi Rais hawezi kuingiliwa katika utekelezaji wa mamlaka hayo.

Nchi nyengine ambayo ni mfano wamefanya haya ni nchi ya Uganda kwenye katiba yao ya Mwaka 1995 uteuzi wa *IGP* Mkuu wa Polisi, ukiangalia Mhe. Mwenyekiti uteuzi wa *IGP* huu unafanywa na Rais kifungu chao cha mia mbili na kumi na tatu cha katiba au ibara ya 213 Ibara ndogo ya pili ya katiba ya Uganda ya mwaka 1995 inasema uteuzi ule lazima uizinishwe na Bunge. Lakini hata uteuzi wa Kamishna wa Magereza ukisoma kwa mujibu wa ibara ya 216 ibara ndogo ya kwanza ya katiba ya Uganda ya mwaka 1995 lazima uizinishwe na Bunge, hali kadhalika yule *Inspector General of Government* nae uteuzi wake lazima uidhinishwe na bunge na katiba yao kifungu cha 223 ibara ndogo ya 4 imeeleza wazi kwamba uteuzi huo lazima uidhinishwe na Bunge.

Hata Tanzania Bara kwa huo uteuzi unaosemwa wa Waziri Mkuu ambao unaidhinishwa na Bunge basi uteuzi ule umeelezwa uidhinishwaji wake ndani ya katiba ya Muungano.

Kwa hivyo mimi ninachosema ni kwamba hii nidhana nzuri lakini utekelezaji wake lazima utekelezwe kwa kufuaa misingi ya katiba na mimi nadhani ni jambo zuri kulichukua huko tunakokwenda tunapotaka kufanya marekebisho ya katiba yetu na isiwe kwa nafasi hii tu , lakini tuichukue kama ni sera tuamue tuseme kwamba nafasi zipi zitahitaji kufanyiwa utaratibu wa namna hii kama ambavyo wenzetu wamefanya.

Nadhani sasa hivi tukaanza kuchomoa tukasema kwamba nafasi ya *DG* kwanza kunaweza kuwa na masuali mengi, maana kuna watu wengi ambao wana nafasi nyeti sana na ambao haufanywi uizinishwaji wao na baraza. Kwa hivyo mimi nadhani kwamba hii tuichukue kama ni sera ambayo tutaifanyia kazi katika kuleta mfanikio, kwanza sio nafasi tu ya *DG,* lakini kwa nafasi nyengine za utenaji ambazo tunaziona ni za msingi au za nyeti ziidhinishwe na baraza mimi nadhani hilo kama tunataka kulifanya basi mimi naamini litaimarisha *cheque and balance* lakini naamini na ndio ilivyo lakini naamini kwamba ni lazima lifanywe katika misingi ya kufuata katiba kama nilivyoeleza wenzetu wamefanya hivyo lakini wamefanya kwa misingi ambayo imewekwa chini ya katiba zao.

Jengine lilizungumzwa ni sifa ambalo lilizungumzwa na Mhe. Hijja Hassan Hija kwamba iwekwe angalau awe na shahada ya pili, ni vuziri lakini nadhani kwenye uteuzi wa nafasi hizi tunaangalia sera ya msingi ambayo tumeiweka. Katika nafasi za kisheria *the high court* ni nafasi ya Jaji Mkuu ndio maana ukakuta wale wengine wote vile vigezo vinafanana. Jaji Mkuu katiba inasema awe na shahada ya kwanza angalau na uzoefu usiopungua miaka saba na huyo ndio jaji Mkuu wa Nchi, anayeongoza moja katika mihimili ya nchi .

Lakini pia ukiangalia Mwanasheria Mkuu katiba inasema vigezo na sifa ni hiyo hiyo na pia hata Mkurugenzi wa Mashitaka sifa ni hiyo hiyo, sasa na hili limefuata msingi huo kwa sababu hiyo ndio tuliyoweka sasa hivi kikatiba kwamba ni *minimum* ya *qualification* ya hiyo lakini hiyo tunasema ni *minimum qualification* haina maana kwamba mtu anateuliwa kwa sababu ya kuwa na shahada ya pili, lakini anawezakuwa asiwe na sifa za kuteuliwa katika nafasi hii, na kukawa na mtu mwenye shahada ya kwanza ana sifa zote lakini kwa sababu hana *academic qualification* na hii maana yake nini nadhani zote tunafahamu, kwamba ili kupata shahada ya pili inawezekana umekwenda

kusoma kitu kidogo ambacho wala hakihusiani na rushwa. Isipokuwa ni sifa za kielimu za kukuongeongezea lakini tuliweka msingi wa kikatiba ni kwamba makisio ni shahada ya kwanza kwa nafasi za Jaji Mkuu, Mwanasheria Mkuu na *DPP* sasa mimi nadhani wakati tunafuma huu mfumo wetu basi ni vyema tusitie nyiza ambayo itaonekana kwamba hii mbona tofauti ili iende vizuri, maana hata wale wanaopaka ukili basi wanatia ili lile jambo lionekane kwamba hili ni kitu kimoja sio kitu cha kigeni.

Sasa nadhani tusiingize *genetics modification* kwenye mfumo wetu ya kwamba itaonekana kwamba ni tofauti sana na ule ambao tumeuanzisha, lakini nadhani tumeona kwamba katika uteuzi zinatizamwa sifa nyingi, zinatizamwa sababu nyingi mpaka huo uteuzi unafanywa, naamini Mhe. Hija Hassan Hija atakubaliana na mimi kwamba mfumo tuliokuwa nao unasaidia kupata watu waliokuwa na uwezo huu.

Lakini pia lilitaja suala la sifa ya umri na Mhe. Rashid Seif alisema asipungue angalau miaka arubaini. Mhe. Mwenyekiti mimi naamini kwamba sifa ya umri ina uzuri wake lakibi bado inabaki kama *subjects*, mimi mwenyewe niliteuliwa nikiwa *DPP* nikiwa miaka 39 lakini niliteuliwa nikiwa *DPP*, (*AG*) nikiwa na miaka 30, *assessment* namuachia Mhe. Rashid Seif sijui angesema huyu hafai kwamba angesubiri miaka arubaini inawezekana kayasikia yangu mabaya tu kwa sababu ya umri naomba asiyaseme hapa aniambie mimi mwenyewe. Lakini ninachosema ni kwamba sifa za umri unakuwa *subjective* lakini tutizame nchi za wenzetu Urais Uganda ni miaka 35, Wamarekani na nguvu zao na taifa lao kuwa kubwa Urais ni miaka 35.

Lakini mimi wakati fulani Mhe. Mwenyekiti nilitembelea Iran wakati wa uchaguzi na kule nikakuta malalamiko wanawake wanalalamika kweli kweli kuhusiana na hili hili la umri, malalamiko yao ni kwamba kwa nini mtu asubiri miaka 18 ndio apige kura wakati huo pengine mwanamke ana umri wa miaka 16

au 17 anaweza kufanya makubwa zaidi kuliko kupiga kura na wenyewe walikuwa wakali kweli kweli Mhe. Mwenyekiti. Wakasema unamkuta mtu pengine miaka 17 huyo mgombea yeye anaweza kumtengeneza mambo yote pengine kaondoka nyumbani kwenda kwenye kampeni za mkutano ndio aliyemvisha shati ndio aliyempa sauti, aliyempa nguvu nadhani mnanifahamu akamtayarisha kwa ajili ya kwenda kupiga kampeni. Lakini unamwambia yote aliyomfanyia hawezi kupiga kura sasa hili wenyewe walikuwa wanasema tu kwamba umri ni *subjective* lakini ni kitu kizuri lazima uwe na pahala kusema hapa ndio iwe kigezo chetu.

Lakini mimi nadhani kwenye hili kwa kukuwa hatujaweka ukiachia nafasi ya Urais na Muwakilishi hatujaweka labda chini ya miaka 21 nalo linaleta tatizo, sasa ikiwa kutunga sheria miaka 21 lakini kwenye kutekeleza sijui ndio unahitaji busara zaidi au kwenye kuitunga. Lakini bado tunasema kwamba hoja ninayoiona ni kwamba kusema sifa za umri ingekuwa na uzuri wake lakini nadhani ingekuwa ni *subjective* kwa sababu ya tofauti mbali mbali ambazo zipo sasa hivi katika mfumo wetu wa sheria.

Lakini jengine alizungumza kwamba sifa nyengine awe na makazi ya kudumu mimi nasema kwa mtu msafi si lazima awe na makazi ya kudumu, na anawezekana hajayapata kwa sababu ya uwo usafi wake na ukawa na mtu ambae hafai ikawa sifa yake ana makazi ya kudumu, sasa mimi nadhani kuyaweka kwenye sheria itakuwa sio vizuri kwa sababu ya mazingira hayo ambayo yanaweza kutokea, niwakumbushe tu katika *process* hizi za uteuzi kunakuwa na *vetting back round cheque* ambayo inaangalia na mambo mengine yote hayo kabla ya kufanyika uteuzi.

Mhe. Mwenyekiti jengine ambalo nilisema nizungumzie kidogo ni kwamba Mhe. Jaku Hashim aliuliza kwamba hivi mtu kukoseshwa ya kuchaguliwa wakati huko ameshapewa adhabu sio kumhukumu mara mbili, alichokuwa anakizungumzia Mhe. Jaku

Hashim ni kitu ambacho tunakiita mtu kupewa adhabu mara mbili, lakini sifa ya kimsingi ya kisheria ni kwamba mtu kupewa adhabu katika jambo lile lile basi inahitaji lazima awe kafunguliwa mashitaka mara mbili. Sasa hii sheria yetu haisemi suala hilo la kufunguliwa mashitaka mara mbili inasema katika kesi ile ile anaweza kupewa adhabu hizo mbili, ambalo halijafikia lile kosa linalokatazwa la kumpa adhabu mara mbili. Kwa hiyo hapa sioni kama kuna tatizo la msingi.

Lakini jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo nilisema ni vizuri nilizungumze ni lile ambalo alizungumzia Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba kwa nini makosa au baada ya upelelezi lazima *IG* apate idhini au mamlaka ipate idhini ya *DPP* kwa ajili ya kufungua kesi ya jinai. Mimi naomba nikumbushe tu kwamba tujiulize kwa nini tulianzisha ofisi ya *DPP* tulianzisha kwa sababu ya kutenganisha upelelezi na uendeshaji wa mashitaka, katika huu uendeshaji wa mashitaka sio kuendesha tu mashitaka lakini ile kuamua nani ashitakiwe na nani asishitakiwe vigezo vilivyotimia ndio ambacho kimetenganishwa na huo sasa ndio muelekeo wa dunia kwamba kutenganisha mashitaka na upelelezi ili kuleta kuondoa huu wasi wasi.

Mhe. Jaku Hasshim tulimsikia jana na malalamiko yake lakini ili kumsaidia kuondoa wasi wasi ni kwamba hili jambo linakwenda sehemu mbili, kuna upelelezi halafu kuna na kuamua je, upelelezi huu ushahidi uliokusanywa unatosha katika kufungua haya mashitaka na hawa watu wanafunzwa vitu viwili tofauti. Kuamua kwamba upelelezi unatosha basi kunahitaji umakini wa hali ya juu na mimi nimefanya kazi hiyo zaidi ya miaka kumi na tano, tokea nikiwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu na nikiwa *DPP* na mara nyingi unagundua kuna makosa ambayo mtu unaweza kumtia akashitakiwa, ukisha kushtakiwa Mheshimiwa wewe ni jina tu lakini wewe si mtuhumiwa lakini ni mfungwa kwa sababu ukipelekwa pale Mahakamani ndio maana ukiondoka pale huondoki hivi hivi unaambiwa kwamba madam umeshitakiwa

basi lazima utoe dhamana na ikikushinda unakwenda ndani kama mfungwa, tofauti yako inakuwa ndogo wapo waliyoyaona hayo wamekaa ndani zaidi ya miaka miwili mitatu baadae unakuja kukuta mtu unaambiwa hana kosa.

Sasa hili linahitaji umakini na mimi nakwambia kesi nyingi zinatokea upelelezi unafanywa unakuwa hafifu hautoshi, wakati mwengine uamuzi au maoni ya upelelezi upo ushahidi lakini unakuja kukuta na mwenyewe unamwambia, hapa kosa linatakiwa kuwe na hiki na hiki na hili halijatimia, hili halijafanyiwa upelelezi nendeni kafanyeni tena na wanakuja wakati mwengine mnakubaliana kwamba hapa hapajatimia, lakini kubwa ni kwamba katiba yetu yenyewe kifungu cha 56 (a) kifungu kidogo cha 3 kimetoa wazi kwamba uwezo wa kushitaki ni ya mkurugenzi wa mashitaka. Kwa hivyo sheria hii haiwezi kumega yale mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashitaka isipokuwa inaweza Mkurugenzi wa Mashitaka akaidhinisha au *ku-delegate* mamlaka yale kama katiba yenyewe ilivyosema kwamba mamlaka yale anaweza kuya-*delegate* au kuyakasimu kwa watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwamba muda hauotoshi lakini bado nina *point* kama tatu za muhimu kufafanua kwa hivyo kama itakuwa muda umemalizika nitaomba nije nimalizie kidogo kwa wakati wa jioni kutoa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria upo muda bado endelea.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, akilini mwangu ilikuwa naona ni saa saba kasorobo.

Kwa hivyo huo ndio mdingi wa kutofauitisha mambo haya.
Lakini jenine mimi nadhani madam tumeanzisha mamlaka ya kuendesha Mashtaka na tunazo hizi taasisi za upelelezi na taasisi ya upelelezi haitokuwa hii tu, taasisi ya upelelezi ipo polisi, uhamiaji, hata *ZSSF* na kuna taasisi nyengine kama Manispaa,

lakini hizi tuzikuze na tuziimarishe wafikie ile hali ambayo wanatakiwa wafanyie kazi ya upelelezi. Lakini katika suala la kuendesha mashitaka basi tukuze nako badala ya kuanza kumega basi tukuze ule uwezo wa ile taasisi ya kuendesha mashitaka ili iweze kuendesha mashitaka katika taasisi.

Mhe. Mwenyekiti kumpata mtu mpaka akaweza kuendesha mashitaka sio jambo rahisi, kwa sababu mtu anapotoka chuo kikuu alichofunzwa ni sheria za jumla tunamuita ni *GP*, ili aweze kuwa na uwezo sasa wa kuweza kutumia elimu yake ya sheria kuendesha mashitaka ni lazima umpe mafunzo maalum ndio maana tumeanzisha Ofisi ya *DPP* watu wote tuliowaajiri ni lazima aende mafunzo ya miezi mitatu ya msingi ya kuendesha mashitaka, lazima aende tena mafunzo ya miezi mitatu katika ngazi ya *international* katika masuala haya na pia kumpatia mafunzo mbali mbali ikiwemo ya fani nyengine ambayo yatamuwezesha kuendesha mashitaka.

Kwa mfano kuwaita madaktari wakaja kuwafunza mambo *basic ya forestic medicine,* kuwaita watu wa uchunguzi wa madawa watu wa *bal static fact* ili kumpa kwasababu hii ni taaluma yote ambayo anaihitajia, sasa ikishakuwa wewe ni mpelelezi tu chini ya haya mamlaka haina maana kwamba utakuwa na uwezo wa kuendesha mashataka, kuendesha mashtaka kama unataka ya ufanisi ni lazima mtu yenyewe uwe umemuandaa kwa ajili ya kuendesha mashtaka vile vile. Kwa hivyo, mimi nadhani katika hili huu mfumo ambao tumeuweka basi unapendekezwa kwenye mswada nadhani ni sahihi kabisa.

Jambo jengine ambalo lilizungumzwa ni kuhusiana na adhabu alizungumza sana Mhe. Salmin Awadha Salmin kwamba adhabu zinaonyesha hazitoshi ni ndogo, mimi labda niseme mambo mawili kuhusiana na hili. Mhe. Mwenyekiti kwanza nadhani makamo Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa anawasilisha ripoti alieleza tatizo la msingi ambalo tunalo, tuna tatizo la msingi

kwamba hatuna wao wameita *punish policy* lakini kitaalam inaitwa ni *sentensing policy* yaani sera ya utoaji wa adhabu. Hii sera inasaidia kuweka haya yote tunayozungumza adhabu hii inatosha au haitoshi, lakini kuna adhabu nyengine ambazo ni kubwa zaidi lakini hazitambuliwi katika mfumo wetu wa kutoa adhabu, maana wakati mwengine unafanya kosa unapewa karatasi tu ukae barabarani useme mimi mwizi kwa wenzetu wanasema hivyo, unapewa bango unakaa Darajani unasema mimi mwizi au kibaka maarufu. Mengine ndio hayo *community service* ziko adhabu za namna nyingi kwa kweli nyengine ni *reformatory* mtu unamwambia tu kwamba ndio kile kinaitwa *suspendent sentence*. Sasa haya ni mambo ambayo mpaka tutakapokuwa na *sentensing policy* itatusaidia kuweka ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, la pili kwenye mfumo wa sheria hii kuna mambo mawili, kuna makosa ambayo yako chini ya sheria hii yenyewe na adhabu zake zimetolewa wazi wazi. Lakini kuna makosa ambayo yametambuliwa tu na sheria hii ndio hayo ya kuhujumu uchumi. Kwa sababu haya makosa haya yote yanasheria zake na adhabu zake, yametambuliwa chini ya sheria hii ili kuiwezesha hii mamlaka ndio isimamie upelelezi, lakini mtu akaposhtakiwa atashtakiwa kwa sheria ile inayohusika. Kwa mfano, magendo hatoshtakiwa chini ya sheria hii ingawa kuwa uzito wa kosa mwendeshaji mashtaka hakatazwi kutumia sheria hii, lakini yale yametambuliwa na sheria hii ili kuiwezesha ile mamlaka maana yake bila ya kuyatambua kwamba haya ni makosa ya kuhujumu uchumi chini ya sheria hii, basi huyu Mkurugenzi Mkuu hatokuwa na mamlaka ya kuyapeleleza, itakuwa mwenye mamlaka ni polisi.

Kwa hivyo, linalofanywa hapa ni kwamba kuyaingiza huku kuyatambua ili kuiwezesha hii mamlaka kuwa ndio taasisi ya kupepeleza kwa sababu haya makosa ya kuhujumu uchumi tumeona hayasimamiwi ipasavyo. Kwa hivyo, anaweza akashtakiwa kwa sheria ile pia anaweza akashtakiwa kwa sheria

hii. Kwa hivyo, adhabu zilizowekwa kule kwa mfano sheria za kodi zinabaki kule kule, lakini pia kwenye sheria zetu tumegundua kuna mapungufu kwamba kuna baadhi ya *incidence* hazitambuliwi ndio maana hii ikaja sheria kwamba ukifanya jambo la namna hii basi wewe utakuwa ni kosa la kuhujumu uchumi. Lakini kwa yale makosa mahsusi ambayo ni nyeti bado yanabaki katika sheria zake, kwa mfano Sheria ya Madawa ya Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mimi hili nadhani hata hapa tunaweza iwe tukabisha iwe milioni 5 au milioni 20 au milioni 100 bado hatutokuwa na kigezo, sheria zile tulizozipitisha bado zitaendelea kutumika kwa makosa haya, lakini mpelelezi sasa atakuwa ni *Director General* wa hii taasisi badala ya kuwa polisi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu sheria ya rushwa ya ngono miaka 30 nadhani kilichoelezwa miaka 30 ni *rape* yenyewe na hiyo ina matawi mengi. Kwa hivyo, mtu kama atakuwa amefanywa jambo hilo kwanza taasisi hii inaweza ikachunguza kama linaingia huku basi watamshitaki kwa sheria ambayo inahusika. Lakini kama haiingii huku basi huyo atakuwa kafanya ubakaji wa kawaida ataendelea polisi kuweza kumchunguza. Kwa hivyo, kwa ufupi nimalizie la mwisho lile alilozungumza Mhe. Abdalla Juma Abdalla kwamba kwa nini *DG* ateuwe mtu wa kufanya tathmini.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba huyo anayemteuwa *DG* sio mtu wa kuchunguza kama katekeleza kazi zake sawa sawa, hiyo kuna kamati, kuna taasisi nyengine za serikali hapa inaitwa ni *performance management* yaani anaweka vigezo kwamba zitakiwa *standard* zifikie hapa na ndio wenzetu wanavyofanya kwamba ili hii taasisi ionekane kwamba ni *efficient* ifikie vile vigezo ambavyo duniani vinatambuliwa basi anatakiwa kuwe na hiki na hiki, *efficient* iweje, *file* likitoka au kesi ikiwa *reported* inachukua muda gani. Hii ni ripoti ya kumsaidia mwenyewe Mkurugenzi kuweza kuona kwamba kazi zinakwenda kwa mujibu inavyotakiwa.

Kwa hivyo, hii hawezi kufanya mwenyewe, ndio maana inatakiwa ateuwe mtu kama vile *internal auditor* wa kuweza kuja kuangalia kwamba je maana *internal auditor* anawajibika kwa yule yule kiongozi lakini bado anatoa taarifa zake na zinafanyiwa kazi. Kwa hivyo, huyu ni kama *internal auditor*, lakini hii haina maana kwamba inazuia taasisi nyengine ambazo zina mamlaka ya kuchunguza mwenendo wa utendaji kazi wa mamlaka ya rushwa basi zisiweze kufanya kazi. Lakini hiki ni kitu tofauti na kinahusiana zaidi na *performance management* ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo mimi nawashukuru sana Wajumbe waliochangia na ninawaomba kwamba tuupitishe mswada huu ili tupate nyenzo ya kufanyia kazi na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kwa mara nyengine kukutana tena katika Baraza lako tukufu jioni hii tukiwa katika hali ya afya njema.

Pia naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao yenye nia ya kufanya mswada huu kuwa bora zaidi. Naomba nichukue nafasi hii kwa Wajumbe ambao walitoa michango yao mbali mbali ambayo itakuwa ni sehemu itakayochangia katika kupambana na rushwa na vitendo vya uhujumu uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wajumbe 17 wamechangia mswada huu mmoja kati yao amechangia kwa maandishi, naomba niwataje kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Panya Ali Abdalla (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala)
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Hija Hassan Hija
4. Mhe. Rashid Seif Suleiman
5. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
6. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
7. Mhe. Ussi Jecha Simai
8. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
9. Mhe. Omar Ali Shehe
10. Mhe. Fatma Mbarouk Said
11. Mhe. Hamza Hassan Juma
12. Mhe. Hassan Hamad Omar
13. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
14. Mhe. Salmin Awadh Salmin
15. Mhe. Ali Salim Haji
16. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na
17. Mhe. Wanu Hafidh Ameir ambaye amechangia kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu kwa uwasilishaji wake mzuri wa michango ya kamati pamoja na marekebisho muhimu waliyoyafanya. Halikadhalika katika kunisaidia kutoa ufafanuzi katika sehemu mbali mbali za mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema kwamba wizara yangu imeyapokea maoni yote yaliyotolewa na kamati na naahidi kwamba maoni yao kwetu sisi ni dira na miongozo ya kuweza kusimamia vyema sheria hii baada ya kupitishwa rasmi.

Miongoni mwa michango yenye uzito mkubwa ni ya serikali kuandaa sera ya adhabu jambo ambalo serikali inaahidi kulifanyia kazi kwa haraka zaidi ili kuweka utaratibu mzuri katika kujenga suala zima la utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kufafanua hoja mbali mbali zilizojitokeza katika mswada huu kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nitafafanua hoja kwa makundi na sio kwa mtu mmoja mmoja, ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili watayapokea au watapokea ufafanuzi huo na nimejitahidi kwa kiasi kikubwa kuweza kuyafafanua.

Hoja zenyewe zitakuwa katika mtiririko ufuatao: kutakuwa na suala la hoja, waliochangia na ufafanuzi.

Hoja ya kwanza: Ilitolewa hoja kwamba sheria iwabane watu wa ngazi zote, aliyetoa hoja hii alikuwa ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Ufafanuzi: Mhe. Mwenyekiti, sheria haikubagua watu wa kuchukuliwa hatua, mtu yeyote atakayefanya kosa chini ya sheria hii atachukuliwa hatua.

Hoja ya pili ilikuwa jina halipendezi lingekuwa kama vile ilivyo TAKUKURU. Hoja hii ilitolewa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Ufafanuzi ni kwamba, naomba kumuarifu Mheshimiwa kuwa TAKUKURU ni ufupisho wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kama ilivyo BLW ikimaanisha Baraza la Wawakilishi. Kwa chombo hiki baada ya kupitishwa kwa sheria na jina rasmi kujulikana tutakuwa na kifupisho chake.

Hoja ya tatu ni kuhusu tusiwe na utaalamu wa kutunga sheria lakini tukashindwa kuitekeleza. Hoja hii ilichangiwa na Mhe.

Makame Mshimba, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Hamza Hassan Juma. Ufafanuzi. Sheria zote huwa zinawekewa utaratibu wa utekelezaji na adhabu kwa wale ambao hawatekelezi. Jukumu letu sote la kuhakikisha kuwa sheria zinatekelezwa hivyo tukishirikiana hakuna sheria ambayo haitatekelezwa. Sheria hii imeweka kinga kwa watendaji wake hasa kiongozi mkuu ambaye hawezi kuingiliwa katika madaraka yake na kuondolewa kwake kumewekewa utaratibu maalum.

Hoja ya nne Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni uhalifu kuchukuliwa hatua na vyombo vya kusimamia sheria. Hoja hii ilitolewa na Mhe. Makame Mshimba na Mhe. Salmin Awadh.

Ufafanuzi wa hoja hii ni kama ifuatavyo: Sheria imeweka adhabu kwa anayetenda kosa na wale watendaji wa taasisi hii watakaobainika kutotenda haki pia watachukuliwa hatua za kisheria na adhabu zao zimetajwa katika mswada huu.

Hoja ya tano Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni sheria ya maadili, Wajumbe walipendekeza ingeletwa mwanzo kabla ya sheria hii. Hoja hii ilichangiwa na Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Mwenyekiti, ufafanuzi ni kwamba mswada wa maadili ya viongozi tayari unaandaliwa na utawasilishwa katika Baraza lako tukufu mud sio mrefu kutoka kikao hiki.

Hoja ya sita Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni Mkurugenzi na Naibu wake kuwa athibitishwe na Baraza la Wawakilishi. Hoja hii ndio hoja iliyochangiwa na wajumbe wengi ambayo imechangiwa na Mhe. Hija Hassan, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Ussi Jecha Simai, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili limetolewa ufafanuzi mzuri sana na Mwanasheria Mkuu na naomba nikubaliane naye na tusubiri hadi hapo baadae taratibu nyengine zitakaporekebishwa.

Hoja ya saba Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa inahusiana na sifa za viongozi wakuu wawe na *degree* ya pili na kuendelea. Hoja hii ilichangiwa na Mhe. Hija Hassan na Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, ufafanuzi ni kwamba kiwango cha *degree* ya kwanza ndicho kiwango cha utaalamu cha utendaji kinachoatambulika katika katika taasisi zetu nyingi. Tunaamini hata kwa nafasi hii kinatosha. Hata hivyo, kiwango cha *degree* ya mwanzo ni kiwango cha chini na hakizuii kuteuliwa mwenye elimu kubwa zaidi kama alivyofafanua Mwanasheria Mkuu mchana huu wa leo.

Hoja ya nane Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa inazungumzia baadhi ya adhabu ni ndogo ziongezwe hasa ya kosa la rushwa ya ngono. Hoja hii ilichangiwa na Mhe. Hija Hassan, Mhe. Ussi Jecha Simai na Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, ufafanuzi ni kwamba, adhabu nyingi zilizowekwa katika sheria hii zinatoa fursa kwa hakimu kupima kiwango cha kosa na kutoa adhabu inayolingana nayo na pale kosa linapokuwa kubwa zaidi itaandaliwa sheria ya mamlaka yenye nguvu kama vile alivyoeleza Mhe. Mwanasheria Mkuu. Naomba niungane naye ni kwamba alivyoeleza ametoa ufafanuzi wa kutosha ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe watakuwa wamesikia na wamefahamu vizuri.

Hoja ya tisa ilikuwa ni viongozi watangaze mali zao na walivyozipata. Hoja hii ilichangiwa na Mhe. Hija Hassan, Mhe. Jaku Hashim, Mhe. Omar Ali Shehe. Mhe. Mwenyekiti, suala hili litawekewa utaratibu na muongozo chini ya sheria ya maadili ya

viongozi ambayo mswada wake tunatarajia kuuwasilisha katika Baraza lako tukufu hivi karibuni.

Hoja ya 10 Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa inazungumzia watumishi wawe na maadili ya kazi na wafanyiwe tathmini ya utendaji wao. Hoja hii ilichangiwa na Mhe. Rashid Seif, Mhe. Abdalla Juma Abdalla na Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Mwenyekiti, ufafanuzi ni kwamba suala hili limewekewa utaratibu chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na mimi naamini ilivyowekwa inatosheleza kabisa.

Hoja ya 11 ilikuwa inazungumzia suala la umri wa kuteuliwa kwa Mkurugenzi usipungue miaka 40. Hoja hii ilitolewa na Mhe. Rashid Seif Suleiman na Mhe. Mwanasheria Mkuu aliichangia kwa kuitolea ufafanuzi. Naomba nieleze kwamba, suala hili litazingatiwa na Mamlaka ya Uteuzi na si vyema kuliweka katika sheria kwani tunaweza tukawa na mtu bora tukakwamishwa na kipengele cha umri. Katika suala hili nakubaliana na ufafanuzi wa mzuri wa Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Hoja ya 12 ilikuwa inazungumzia suala la kuwa atakaeteuliwa awe na mali kama vile nyumba na anayeheshimika katika jamii. Hoja hii imezungumzwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman. Ufafanuzi ni kwamba, uwadilifu hautegemei sana kuwa na mali kwani hata wenye mali pia wameshawahi kukubwa na makosa ya aina hii ya kujilimbikizia mali zaidi.

Hoja ya 13 ilikuwa inazungumzia fedha za mfuko ziwe fungu maalum lililoidhinishwa na Baraza na sio ruzuku au misaada. Hoja hii ilizungumzwa na Mhe. Rashid Seif. Ufafanuzi ni kwamba, fedha zote za ndani na za misaada zinafuata utaratibu wa kibajeti. Hivyo, hakuna haja ya kuwa na wasiwasi, Mkurugenzi hatokuwa na fursa ya kuomba misaada kwa taasisi anazozishughulikia kikazi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya 14 ilikuwa ni suala la kutofautisha kati ya sadaka na rushwa hasa kwa mazingira ya Zanzibar. Hoja hii ilizungumziwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Ufafanuzi ni kwamba, chombo hiki ni kikubwa na kitakuwa na viongozi wenye hekima na wataweza kutofautisha sadaka na rushwa kwa kuzingatia dhamira ya mtoaji na mpokeaji. Chombo kimepewa jukumu kubwa la kuchunguza makosa ya aina hii.

Hoja ya 15 ilikuwa inazungumzia kifungu cha rushwa ya ngono, kimelengwa kwa wanaume peke yao. Hoja hii ilizungumzwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Ufafanuzi ni kwamba kwenye mswada wa sheria hii haikutaja mwanamme au mwanamke, yeyote atakayefanya kosa ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

Hoja ya 16 ilikuwa inazungumzia mamlaka ipewe ruhusa ya kushtaki bila ya kupitia kwa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*). Hoja hii ilizungumziwa na Mhe. Ismail Jussa. Lakini ufafanuzi ni kuwa suala hili limetolewa ufafanuzi mzuri sana na Mwanasheria Mkuu na naomba nikubaliane naye. Ni vyema kutofautisha chombo cha uchunguzi na kushtaki ili kutenda haki zaidi. Tukifanya hivi tutakuwa ndio hasa tutakapopata kile kipimo cha utawala bora.

Hoja ya 18 Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa inazungumzia kwa nini tuanzishe taasisi wakati tulikuwa na kikosi cha kupambana na rushwa kilichokuwa chini ya usimamizi wa polisi. Hoja hii ilizungumzwa na Mhe. Abdalla Mohammed Ali na ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:

Lengo ni kuwa na chombo chenye nguvu zaidi na kinachojitegemea badala ya kutumia chombo ambacho kina majukumu mengine na pia kina majukumu mengi ya kimuungano.

Hoja ya 19 ilikuwa inazungumzia suala la kosa la kusema uongo limewekewa adhabu kubwa kuliko baadhi ya makosa mengine. Hoja hii vile vile ilitolewa na Mhe. Abdalla Mohammed na ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:

Uongo unaweza kuleta madhara makubwa na mara nyengine kuliko hata upotevu wa mali. Hivyo mwenye kosa la aina hiyo anastahiki adhabu kubwa ndio maana wazee wetu wakasema, “bora kujikwaa kidole kuliko kujikwaa ulimi”.

Hoja ya 20 Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa inazungumzia mambo ya kimataifa yanayoridhiwa na Tanzania pia yaridhiwa na Baraza la Wawakilishi. Hoja hii ilitolewa na Mhe. Omar Ali Shehe na ufafanuzi wake ni kwamba. Kwanza ushauri wake tumeupokea na kadri itakavyowezekana mambo yanayoridhiwa na Bunge au Bungeni, serikali itafanya jitihada ya kutoa taarifa katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya 21 ilikuwa inazungumzia suala la adhabu kubwa itolewa kwa wanaoficha bidhaa. Hoja hii ilitolewa na Mhe. Fatma Mbarouk Said na ufafanuzi wake ni kwamba, mswada umeweka adhabu ya kutosha ikiwa ni pamoja na kifungo. Hivyo adhabu hizi zikitumika ipasavyo suala hili litaondoka kabisa hapa nchini kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya 22 ilikuwa inazungumzia Mahkama gani yenye mamlaka ya kusikiliza kesi za rushwa na uhujumu uchumi. Hoja hii ilizungumzwa na Mhe. Salmin Awadh na ufafanuzi wake ni kwamba, kwa mujibu wa aina ya makosa chini ya mswada wa sheria hii ni Mahkama Kuu. Kosa la rushwa hata kama ni dogo lina uzito mkubwa. Kifungu cha 73 cha mswada wa sheria hii kinafafanua zaidi.

Hoja ya 23 Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa inazungumzia adhabu ni kosa kwa mtoaji na mpokeaji. Je, katika hali kama hiyo

watakaotoa taarifa inakuwaje? Hoja hii ilizungumziwa na Mhe. Hamza Hassan Juma. Ufafanuzi wake ni kwamba, kama utatoa taarifa ya rushwa hutakuwa na kosa ndio njia kuu muhimu ya kuondoa tatizo hili.

Pia mamlaka imepewa jukumu la kuchunguza ili kubaini vitendo vya rushwa vilivyojificha. Kwa hivyo nataka niwahakikishie wananchi raia wema kwamba watakaotoa taarifa hawatadhurika kwa sababu tu pengine taarifa hizi zitawafikia walengwa.

Hoja ya 24 ilikuwa inazungumzia suala la uteuzi wa viongozi ufanyike kwa makini. Hoja hii ilizungumzwa na Mhe. Hamza Hassan. Mhe. Mwenyekiti, ufafanuzi ni kwamba, kila kiongozi anayeteuliwa huwa anaangaliwa maadili yake na vyombo vinavyohusika kabla ya kuteuliwa na naamini viongozi wa taasisi hii watateuliwa kwa umakini hasa kutokana na uzito na umuhimu wake kwa maslahi ya wananchi ambao wanakosa hako zao kutokana na vitendo vya rushwa.

Hoja ya 25 Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa inazungumzia watu wasio waaminifu wanaofanya udanganyifu katika hati na nyaraka mbali mbali. Hoja hii ilizungumziwa na Mhe. Hamza Hassan na Mhe. Omar Ali Shehe. Mhe. Mwenyekiti, haya ni makosa chini ya sheria hii na atakayebainika anafanya mambo haya basi atachukuliwa hatua za kisheria.

Hoja ya mwisho Mhe. Mwenyekiti, kwa leo ni hoja ya 26 ambayo ilikuwa inazungumzia wananchi wapewe taaluma. Hoja hii ilizungumzwa na Mhe. Ali Salum Haji ambayo ufafanuzi wake ni kwamba moja katika majukumu ya mamlaka ni kuwaelimisha wananchi kama ilivyo katika kifungu cha 13(1)(h). Kwa hivyo, taaluma itatolewa kwa sababu sheria yenyewe inataka itoe taaluma.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ni imani yangu kwamba wajumbe watakuwa wamenisikiliza kwa makini na vile vile walimsikiliza kwa makini sana Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar alipokuwa akitoa ufafanuzi wake. Ni imani yangu kwamba tunae Mwanasheria Mkuu mahiri, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar na sio Mwanasheria Mkuukuu. Kwa hivyo, ufafanuzi aliyoutoa ulikuwa ni ufafanuzi wa kina na nina imani kwamba Waheshimiwa Wajumbe watakuwa wameusikiliza pamoja na ule ufafanuzi ambao mimi nimepata wasaa wa kuweza kuutoa jioni hii ya leo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri sasa niwahoji Wajumbe.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi huwa nalitahadharisha Baraza lako, Kanuni ya 71 fasili ya pili inasema, ‘mara kabla ya uamuzi wowote kufanyika ikiwa mjumbe yeyote aliyehudhuria atapinga kwa kudai kwamba mbali na Spika Wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya wajumbe wote, basi kama Spika kathibitisha kuwa wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya wajumbe wote atasimamisha shughuli kwa muda wa dakika tano na huku mhudumu kwa maelekezo ya katibu akipiga kengele kwa vituo yaani sio mfululizo”.

Mhe. Mwenyekiti, nina wasi wasi kwamba wajumbe tuliomo ndani tunatimia zaidi ya nusu ya Baraza kuweza kufanya maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, Mjumbe aliyesimama sasa hivi kutoa hoja yake hoja yake ni sahihi na labda basi tuchukua fursa hii kuliahirisha Baraza hili kwa muda

wa dakika tano ili wajumbe wale ambao wako maeneo ya karibu hapa waweze kufika na tuweze kuendelea na utaratibu wetu.

(Saa 11:30 Baraza liliahirishwa kwa muda) kwa ajili ya kuwaita waheshimiwa walioko nje ili kutimiza quorum)

(Saa 11:35 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe baada ya kwisha kukamilika kwa *quorum* sasa tuwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono juu, waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza lako tukufu limeujadili na kuukubali mswada, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ili kupitisha vifungu vya mswada huu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu cha 1 - Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu cha 2 - Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Kifungu cha 3 - Kuanzishwa kwa Mamlaka pamoja na marekebisho yake

Kifungu cha 4 -

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nilipokuwa natoa mchango wangu nilikizungumzia kifungu cha 4 kuhusu Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu. Nilitoa mapendekezo kwamba kifanyiwe marekebisho kuwa kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais na iongezewe na kuthibitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nimepata nafasi ya kumsikiliza Mhe. Mwanasheria Mkuu akitoa mchango wake kuhusiana na suala hili ambapo Mhe. Waziri katika majumuisho yake kwa lugha zetu mimi na Sheikh Othman tunasema *in total* ameyakubali na kwamba hayo ndio maelezo ya ufafanuzi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi bado sijaridhika na nilikuwa nataka nitetee hoja yangu katika suala hili kwa sababu zifuatazo. Katika ufafanuzi alioutoa Mhe. Mwanasheria Mkuu hoja zake zilijikita zaidi kwamba kwa mujibu wa mfumo wa kikatiba tulionao hivi sasa haujaweka utaratibu wa aina hiyo ambao umependekezwa na Wajumbe. Kama Mhe. Waziri alivyokiri kwamba hoja hii ni katika hoja ambazo zimechangiwa na Wajumbe wengi sana wa Baraza hili kuliko pengine kifungu chengine chochote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sikubaliani na rai hii na hoja zangu ni kwamba tukiitazama katiba haijazuia mahala popote Rais kushirikiana na chombo kingine lakini hasa madaraka yake kukipa chombo kingine kabisa seuze kushirikiana kama tulivyopendekeza sisi.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba Wajumbe wakafanya marejeo kwenye ibara ya 53 ya Katiba ya Zanzibar inasema “Kwa mujibu

wa Katiba hii na bila ya kuathiri masharti ya sura ya 8 au sheria nyengine yoyote iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi Mamlaka

(a) ya kuanzisha au kufuta afisi katika Zanzibar
(b) ya kuteua wakuu wa afisi hizo na ya kupandisha cheo kwa muda wa utumishi, kufukuzwa na kushughulikia na hatua za kinidhamu kwa watu walioteuliwa kushika dhamana za afisi hizo yamo mikononi mwa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu iko pale katika maelezo ya ufunguzi anaposema "Kwa mujibu wa Katiba hii na bila ya kuathiri masharti ya sura ya 8 au sheria nyengine yoyote iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi."

Ndio kusema kwamba kwa mujibu wa katiba yetu ikiwa tutapitisha sheria ambayo itaweka masharti tofauti ndani ya katiba hii, katiba hii itakuwa imeruhusu kwa kutumia kifungu hichi cha katiba. Hilo moja.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, jengine katika majibu ya serikali vile vile ilitajwa kwamba kwa nini iwe kwa huyu mmoja tu, kwa nini isiwe kwa watu wengine ama pengine wanaongoza pia na taasisi nyengine ambazo nazo ni nzito na muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, mifano aliyoitoa Mhe. Mwanasheria Mkuu ni mifano ambayo makhsusi imetajwa ndani ya katiba. Kwa mfano, Uteuzi wa Mawaziri, Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili wa Rais, *DPP*, Mwanasheria Mkuu, Majaji, yote haya yamewekewa utaratibu maalum ndani ya katiba. Kwa hivyo, isingekuwa sahihi ije sheria nyengine iweke utaratibu tofauti na ule ambao umetajwa ndani ya katiba.

Lakini Mkurugenzi Mkuu ambaye ikipitishwa sheria hii tunampendekeza atakuwa wa Mamlaka hii huyu hajatajwa ndani ya katiba ametajwa na sheria hii. Ndio maana kuwepo kwake,

namna ya uteuzi wake, namna ya kumpata utategemea sheria hii. Kwa hivyo, sheria hii ikipita ndio itakayoweka utaratibu mzuri.

Sasa sheria hii tukiirekebisha tukasema kwamba atateuliwa na Rais na kuthibitishwa na Baraza la Wawakilishi utakuwa ni utaratibu umewekwa ambao utakuwa umezingatiwa na hichi kifungu cha 53 ambacho kinasema kwamba "Bila ya kuathiri masharti ya sura ya 8 au sheria nyengine yoyote iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi."

Lakini niongezee hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka haraka pia kwa kuwarejesha Wajumbe katika kifungu cha katiba vile vile cha 63. Kifungu cha 63(1) kinasema "Kutakuwa na Baraza la Kutunga Sheria ambalo litajulikana kama Baraza la Wawakilishi litakalokuwa na sehemu mbili, Rais wa Zanzibar kwa upande mmoja na Wawakilishi kwa upande wa pili."

Kifungu cha 63(2) kinasema "Iwapo kwa mujibu wa masharti ya katiba hii au masharti ya sheria nyengine jambo lolote linahitaji kuamuliwa au kutekelezwa na sehemu zote mbili za Baraza la Kutunga Sheria, basi jambo hilo halitakuwa na nguvu za kisheria mpaka liwe limeamuliwa au limetekelezwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na vile vile na Rais."

Mhe. Mwenyekiti, mfano uko hai, tukitunga sheria sisi hapa haiwi sheria mpaka ipate idhini ya Rais kwa kuwa *assented* kuthibitishwa. Sasa ndio nasema hapa pamewekwa kifungu kinachosema "Iwapo kwa mujibu wa masharti ya katiba hii au masharti ya sheria nyengine."

Mhe. Mwenyekiti, napendekeza kwamba jambo likifanywa litekelezwe na sehemu zote mbili litakuwa halijatimia mpaka sehemu zote mbili zitekeleze. Ndio kusema Mhe. Mwenyekiti, kwamba kwa mujibu wa vifungu hivi tukipitisha marekebisho tuliyoyapendekeza sisi na Wajumbe wengine wengi itakuwa

hatujenda kinyume na katiba na katiba itakuwa imetuwezesha kabisa kufanya maamuzi hayo na tutakuwa tunaanzisha zaidi ya uwajibikaji ambao hauhitaji kungojea marekebisho ya katiba. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa mapendekezo hayo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kujaribu kutoa ufafanuzi kwa kadri alivyofahamu yeye tafsiri ya sheria. Nilichosikitika tu ni kwamba kanukuu katika hoja yangu mambo nusu nusu.

La mwanzo Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba mimi kimsingi sioni tatizo juu ya jambo hili kwa sababu litaimarisha utendaji katika nchi yetu, litaimarisha kitu tunachoita *check and balance.* Lakini nilisema ni vizuri tunapolifanya jambo hili tulifanye kwa umakini na tulifanye kwa njia ambayo hatutokuwa tunachanganya mambo. Nimetoa mifano ya nchi ambazo wamefanya jambo hili iwe sisi tusaidie kutafsiri sheria kwa nini wenzetu wamefanya. Wenzetu hawakufanya kwa kubahatisha wamefanya kwa kuelewa kwamba kinahitajika hicho kitu kifanywe *expressly* katika katiba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema tusifanye hili kwa tafsiri ya kubahatisha tufanye kwa tafsiri ambayo ni ya uhakika na tunapolitekeleza lisilete tatizo lolote.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la msingi kama unatafsiri sheria lazima uende kwenye msingi yaani kwenye ile *norm* au ile *basic principle* ya jambo lenyewe halafu uje katika hizo *exceptions*. *Basic principle* ambayo katiba haikuchanganya maneno chini ya kifungu cha 5A ni kwamba tuna mfumo wa *Separation of Powers* ndio kanuni ya msingi kwamba tuna *Separation of Powers* mamlaka tatu ambazo kila moja imeelezwa mamlaka yake.

Suala la uteuzi wa watendaji ni mamlaka ya *executive*, ni mamlaka ya Rais ambayo yameongezwa nguvu na kifungu cha 51

na 53. Sasa tunapo-*introduce approval* ya uteuzi wa watendaji iwe mikononi mwa Baraza maana yake ni kitu gani. Maana yake Rais atafanya uteuzi Baraza likikataa maana yake ni kitu gani, ni kwamba uteuzi huo hauwezi kufanyika. Sasa hapo maana yake ume-*curtail prerogative* ya *executive* chini ya kifungu cha 5A. Sasa kama unataka ku-*curtail prerogative* ya *executive* ambayo *expressly* imekuwa *provided* na katiba huwezi kufanya hivyo kwa kutumia sheria. Ndio maana hao wenzetu waliofanya mambo hayo wameyaweka kwenye katiba ili kusiwe na ubishani kwamba ilikuwa sahihi haikuwa sahihi.

Sasa mimi nasema kwa nini tuwe na haraka kwa jambo hili. Kanuni ni nzuri, hilo jambo ni zuri, lakini tulifanye tusilete mgongano katika utendaji ndio hoja yangu ya msingi. Mimi ninaamini kama tutalifanya hivyo kwenye sheria tutakuwa tuna-*curtail* madaraka ya *executive* yaliyoelezwa chini ya kifungu cha 5A kwa sababu sasa uteuzi utakuwa ni wa Baraza sio wa Rais, Rais atakuwa anapendekeza ndio maana yake. Labda basi Baraza liteue Rais ndio aidhinishe hapo ndio atakuwa amefanya uteuzi.

Lakini kifungu cha 63 anachokizungumzia Mhe. Ismail Jussa Ladhu kinazungumzia jambo ambalo kimsingi linakubalika lifanywe na pande zote mbili ambalo limeelezwa ndani ya katiba kwamba hili lifanywe na pande zote mbili. Hata unaposema kwa mujibu wa sheria hiyo sheria ni lazima itii masharti ya katiba. Sheria yoyote ambayo ina-*curtail provision* madaraka *prerogative* ya Rais au ya *executive* au ya chombo chochote kile hiyo itakwenda kinyume na katiba kwa maoni yangu.

Mimi ushauri wangu ni kwamba tusifanye jambo la kubahatisha. Kama tunataka kulifanya hili ni jambo zuri lakini tulifanye kwa misingi ambayo inakubalika. Hili mimi nasema anaweza akawa na tafsiri yake, mimi naweza kuwa na tafsiri yangu na mwengine anaweza kuwa na tafsiri yake, lakini bado litakuwa ni *subject* na Mahakama. Mimi ninavyoliona ni kwamba hili jambo litakuwa

linavunja katiba au halitokuwa wazi na linaweza likatuletea matatizo hasa ukiangalia uzoefu wa wenzetu ambao wanafanya jambo hili.

Kwa hivyo, mimi nadhani kwamba hoja anayoisema dhamira ni nzuri na tumeikubali wala sioni mimi tatizo lake. Kwa sababu hata kama tutaamua Baraza zima hili iwe sote tupitishe hoja kwamba hili ni sawa, lakini Baraza haliwezi ku-*overright* kupitisha sheria ambayo ina-*overright* katiba. Ni vyema kwanza turekebishe hiyo katiba ili hiyo sheria iruhusike kuweza kutungwa ndio hoja ambayo nimeizungumza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima zote kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu naomba nitofautiane nae. Nafurahi katika maelezo yake kasema kwa tafsiri yake na bahati nzuri katika katiba yetu hakuna pahala popote ambapo panasema kwamba tafsiri itakayosimama ni ya Mhe. Mwanasheria Mkuu. Ndio maana nafurahi kwamba ka-*appreciate* kwamba kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri yake. Lakini chombo ambacho kina mamlaka ya kutafsiri katiba na sheria nyenginezo ni Mahakama.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, sitaki tufike huko, mimi ninachosema hapa hapana kupindisha maneno wala kutoa tafsiri pana wala jambo jengine lolote. Vifungu nilivyovisoma Mhe. Mwenyekiti, viko wazi kwamba vinatoa fursa hiyo na kwa bahati nzuri havijafungwa na vifungu vyengine vyovyote. Maana yake kunakuwa na *cross reference* unajua utaambiwa labda ukiacha kifungu fulani hapajasema pahala popote. Mhe. Mwenyekiti, naomba nirejee tena kidogo halafu niendelee na hoja yangu.

Kwa mujibu wa kifungu cha 53: “Kwa mujibu wa katiba hii na bila ya kuathiri masharti ya sura ya 8 au sheria nyengine yoyote iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi.”

Sasa ukishatoa *room* ya kwamba kuna uwezekano wa kutokea sheria nyengine yoyote iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi ikawekwa kwa utaratibu mwengine ambao tofauti na uliotajwa na ibara ya 53 maana yake utaratibu huo umekubaliwa kikatiba ndio maana yake wala haitaki kutafuna maneno imeelezwa kwa uwazi kabisa. Mimi nadhani *just man* wa katiba hii alikuwa bahati nzuri Mswahili na sisi sote Waswahili humu ndani tunaelewa hii lugha.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 65 ukikisoma katika maelezo yake Mhe. Mwanasheria Mkuu anasema hichi kimekusudiwa kwa wale ambao kimsingi yamekusudiwa kufanywa na pande hizi mbili. Hilo neno kimsingi Mhe. Mwenyekiti, halina tafsiri ndani ya katiba hii, hatujaambiwa kwamba kimsingi ni kwenye kutunga sheria na ku-*assent* tu basi. Ndio maana nikasema katiba ime-*assume* kwamba yanaweza kuwepo mambo mengine.

Kwa nini nasema hivyo. Kwa sababu ukisoma hapa kifungu cha 63(2) kinasema “Iwapo kwa mujibu wa masharti ya katiba hii au masharti ya sheria nyengine jambo lolote linahitaji kuamuliwa.”

Sasa ingelikuwa tunakusudia kwamba hapa ni katika *assenting* tu basi katiba ingefunga hapa kwa sababu mambo ya kutunga sheria yanaweza kufuata taratibu ndani ya katiba hii. Lakini katiba inaweka hiyo *room* kwamba au masharti ya sheria nyengine kwamba kuna uwezekano. Ndio maana nasema tukiirekebisha sheria hii itakuwa imeingia ndani ya vifungu hivyo.

Lakini hoja yake nyengine katika maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu hapa anasema tusifanye mambo kwa kubahatisha. Nataka nimhakikishie kwamba wala hatufanyi kwa mambo ya kubahatisha ndio maana tumechaguliwa kuja humu ili tufanye kazi ya kutunga sheria kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie katika hilo. Mimi naiomba serikali iwe makini wakati inapotafuta hoja gani kujibu hoja za wajumbe wa *backbenchers*. Kwa sababu ikiwa kila siku tunabadilika badilika basi tutakuwa hatuweki ule msingi wa *continuity* ambao ni msingi mmoja wa sheria.

Wakati fulani Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanasheria Mkuu katika majibu yake ametumia msingi wa *separation of powers.* Baraza hili hili nilisema mara moja mimi nilipokuwa nazungumzia nafikiri suala la Sheria ya Utumishi wa Umma, nikazungumzia hilo suala la mgawanyo wa madaraka. Nikajibiwa hapa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwamba katiba yetu haijaweka msingi wa *seekly* kuwa na *separation of powers.* Hoja ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ni kwamba ndio maana Mawaziri ni *executive* lakini ni sehemu ya Baraza. Kwa hivyo, tusiutumie huu mfumo wa *selectively* kwamba tunapotaka kunyamazisha hoja hii tunasema hakuna *strictive separation of powers.* Lakini tunapotaka kunyamazisha hoja nyengine tunasema aaa kuna *separation of powers* tusichanganye, tutakuwa hatuna msingi wa *continuity*.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie hoja yangu ya kuliomba tena Baraza lako lizingatie hili kwa sababu ametoa mfano huu wa kusema kwamba tukiyachanganya haya tutakuwa tunakiuka huo msingi.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna nchi ambayo ni mfano wa separation of powers duniani ni Marekani na yeye mwenyewe Mhe. Mwanasheria Mkuu katika mchango wake asubuhi katwambia kwamba imetoa *room* ya baadhi ya watu majaji na watu wengine kuthibitishwa na *senate*. Hata kama imeandikwa ndani ya katiba yao lakini katiba hiyo hiyo inatambua *separation of powers*, kama *separation of powers* haiwezi kuwa ni hoja.

Mhe. Mwenyekiti, ndio hivyo hivyo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nataka kutoa mfano, Waziri Mkuu ukisoma humu hajaambiwa anapendekezwa na Rais na anateuliwa na Bunge. Ukisoma kifungu cha 51(1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano kinasema "Kutakuwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano atakayeteuliwa na Rais kwa kufuata masharti ya ibara hii na ambaye kabla ya kushika madaraka yake ataapa mbele ya Rais.

Rais anamteua lakini kifungu cha 51(2) hapo kinazungumza kwamba uteuzi huo utathibitishwa na Bunge, haujasema kuwa utathibitishwa na Bunge kwamba Rais hateui Waziri Mkuu. Kwa hivyo, nasema kama kuna hoja nyengine tuambiwe lakini kama hoja ni misingi ya katiba na misingi ya *separation of powers* bado hakujakuwa na hoja za kuridhisha. Labda serikali itwambie tu kwamba yenyewe inaona haijawa tayari juu ya suala hili lakini tusijifiche kwa kichaka cha njugu kusema kwamba katiba hii tunaizuia.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani bado Mhe. Ismail Jussa Ladhu labda nia ni kuonesha nani kashinda hoja. Lakini mimi nadhani tunachozungumza kiko wazi kwa kweli ni kwamba kazi za Baraza la Wawakilishi ambazo zimetokana na kifungu cha 5A cha katiba zimeeleza wazi na kifungu cha 88 cha katiba. Hizo ndio kazi za Baraza la Wawakilishi ambao ndio msingi wa kifungu cha 5A cha katiba, *as legislature* kazi zake ni hizo, sheria nyengine zimefafanua hizo kazi.

Katika hapo hakuna suala la appointment ya executive au suala la uteuzi, ndio maana hata Katibu wa Baraza la Wawakilishi anateuliwa na Rais. Maana kama ni uteuzi basi ungekuwa ni wa Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu ni mtendaji *(executive).* Tunapoleta hoja ya kusema kwamba Baraza hili liidhinishe uteuzi unaofanywa na Rais maana yake ni kwamba

siku linaweza likaidhinishwa linaweza lisiidhinishwe. Kwa hivyo, mamlaka ya uteuzi *indirectly* yatakuwa mikononi mwa Baraza na ambao sio kazi yake kwa mujibu wa kifungu cha 88.

Ndio maana mimi nasema hivi wenzetu waliofanya wamefanya kwa sababu hawajui, hizo katiba zao ziko hivyo hivyo nao. Lakini wamefanya kwa sababu msingi wa utekelezaji wa hivi vyombo uko kwenye kifungu cha 5A cha katiba. Labda atupe tafsiri yake kwamba maana yake ni kitu gani, kwamba kuna *separation of powers.* Bila shaka kanuni yoyote ina *exception* na yeye anajua, lakini *exception* hiyo lazima uiweke kwenye hiyo sehemu ambayo umeandika hiyo principle yenyewe.

Sasa *separation of powers* imekuwa provided kwenye katiba. Unapotaka kuweka *exception* zake unaweka pia kwenye katiba. Ndio maana hawa Wamarekani hizo *exception* kweli wana *classic example* ya *separation of powers.* Hata hicho alichosema Mhe. Abubakar Khamis Bakary sio kupinda maneno, wala sio kubabaika na hoja, wala sio kutafuta hoja.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba katiba yetu imetambua *separation of powers,* lakini katiba hii hii ndio iliyoweka *exception* haikuwekwa kwenye sheria. Hiyo ndio hoja ambayo mimi naiona iko wazi na mimi nasema hata kama Baraza hili zima tutaipitisha hii sheria kwa kauli moja haifanyi kanuni hiyo ikawa imebadilika kwa sababu sheria hii tumeipitisha sote. Hivi tunataka Rais kateua Baraza linasema huyu hatumtaki.
Kama tuntaka kufanya *exception* hiyo suala ni dogo tu kwamba hii document katiba ni yetu, Baraza hili hili ndio linaloipitisha, ndio hoja ambayo tunaizungumza. Lakini hivyo vifungu ninavyovisema vinazungumzia lile jambo ambalo kimsingi linasema *application* ya hiyo kanuni anayotaka yeye maana yake itakuwa Baraza hili ndio lenye mamlaka ya uteuzi kitu ambacho ni kinyume, wazi wazi ni kinyume na kifungu cha 5A cha katiba, vyenginevyo tuweke *exception* kwenye hii katiba yenyewe. Hiyo

ndio hoja ambayo tunaizungumza na mimi ninaamini kama sheria hii tutaipitisha itaweka kifungu hicho, kifungu hicho kitakuwa ni batili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa Ladhu kabla hujaendelea nahisi labda nikushauri. Kutokana na maelekezo ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu ameyatoa tunaomba either uwe umekubaliana na hii hoja au tuingie katika utaratibu wa kupiga kura. Lakini nalo pia inabidi tuliangalie je, iko haja ya kufanya hivyo kwa suala hili. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naona unafanya kazi ambayo kimsingi ningeiomba mimi ya kupendekeza kupiga kura lakini mimi nadhani hatuna haja ya kufika huko. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasimama mara hii nikijua kwamba mujibu wa kanuni ni mara yangu ya tatu na ya mwisho. Kwa hivyo, ningeweza kabisa kusema baada ya maelezo haya tupige kura na mimi ninaamini kabisa tukipiga kura hoja yangu itashinda.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaamini katika msingi mzuri ambao alitwambia Mhe. Mwanasheria Mkuu bahati mbaya kama ninavyosema kuwa wenzetu hawako *consistence* katika yale wanayotuambia humu ndani. Siku tulipojadili sana suala la bajeti ya Wizara Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mhe. Mwanasheria Mkuu alitupa wasia mzuri sana, alisema kwamba ni muhimu sana kwa mambo ambayo yanagusa maslahi ya nchi ikawa serikali, Baraza la Wawakilishi na wananchi tukawa tunakwenda pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa kama ni hivyo basi ni kwamba kila upande uzingatie *concern* yake. Ndio maana katika *legislative process* kuna masuala ya kuzingatia hoja za pande zote mbili. Kama si hivyo, kama chombo hiki kazi yake ni kuja kupitisha mapendekezo yanayoletwa na serikali tu, basi itakuwa Baraza hili limegeuzwa kwenye *rubber stamp* jambo ambalo sisi hatuwezi kulikubali.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuheshimu sana uwezo ambao nataka nikiri kabisa kwa kunizidi Mhe. Mwanasheria Mkuu katika fani hii. Lakini bado nasema katika vifungu nilivyovitaja sitaki kuvisoma tena. Kifungu cha 53 na kifungu cha 63 bado vimetoa *room* hiyo. Yeye Mhe. Waziri katika mifano kwenye mawazo yake ya mwisho kwa mifano ya nchi alizozitoa ni kwamba pale katiba yenyewe imeweka *exception.* Mimi nasema na katiba hii pia imeweka *exception* ndio maana ikasema au masharti ya sheria nyengine. Kwa hivyo, hiyo *exception* hiyo imetolewa. Sasa ni kiasi gani tunaitumia ni jukumu la chombo hicho kwa sababu ndio chombo chenye uwezo wa kutunga sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine kasema, tunarudia katika hoja ile ya *suppression of powers* alivyosema kwamba kama suala la kuteuwa tungeteuwa katibu wa Baraza. Mimi nasema bahati mbaya ndio hizo sheria zilizokuwepo huko nyuma, lakini nadhani tungekuwa tunatunga sheria leo, mimi nilikuwa sipo. Lakini leo ningekuwepo basi ningesema pia hivyo hivyo kwamba aidhinishwe na Baraza la Wawakilishi. Lakini sasa hivi sizungumzii hiyo, nazungumzia sheria ambayo iko mbele yetu Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, ninachosema ni kwamba bado nasisitiza kuwa kama nilivyounga mkono upande wa pili wa bahati tu hapa kwamba uteuzi wa Waziri Mkuu unateuliwa na Bunge, haujamaanisha wala katiba ya Muungano haijasema popote kwamba Bunge ndio linateuwa, Rais ndiye anayeteuwa, na kwa msingi huo huo Baraza hili likiambiwa lithibitishe bado itakuwa ni kuthibitisha sio kuteuwa. Nadhani Kiswahili kinaeleweka kabisa, tofauti ya kuteuwa na kuthibitishwa. Lakini kwa sababu tu ya kujenga *spirit* nzuri, mimi nasema nakubali tuendelee.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nasisitiza sana serikali isilichukulie Baraza hili *for granted* na watambuwe kwamba kutunga sheria ni *process* inayo-*involve* serikali kutoa mapendekezo yake na sisi

kama wawakilishi kuchagua tunaloliona linatufaa, tukiona ambalo lina mawazo tofauti pale tunahaki ya kufanya mabadiliko. Naamini tungefanya ambayo tumependekeza basi hatuvunji katiba Mhe. Mwenyekiti, wala tusitishwe kwa suala la kuwa tunavunja katiba, hatuvunji katiba. Ni kama lile suala la juzi tulivyotishwa hapa kwamba mkifanya hivi Baraza itabidi livunjwe, mambo haya ya kutishwana Mhe. Mwenyekiti, tuyawache twende katika misingi yetu.

Kifungu cha 4 Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Nilipokuwa nikichangia kifungu cha 4 nilitaja pendekezo hilo kwamba huyu mteuzi atakayeteuliwa na Rais athibitishwe na Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina *lament argument*, kwa hivyo naomba mnichukulie hivyo, sitaki kunukuu katiba wala sheria. Mhe. Mwenyekiti, tulisema kiongozi huyu ana mamlaka ya kutizama mihimili yote mitatu, namna inavyotoa huduma zake kwa wananchi bila ya kupata rushwa wala kuhujumu uchumi. Kwa hivyo, huyu kiongozi wa aina hii ana *exceptional characteristic*, ana *exceptional pictures*.

Kwa hivyo, namuomba Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri kwamba pamoja na yote hayo ili kuweka heshima ya yule kiongozi atakayeteuliwa kuwa anawajibika zaidi kwa umma kuliko kwa mtu mmoja aliyemteuwa, ndio tukasema itabidi athibitishwe na Baraza la Wawakilishi.

Sasa kama katiba hairuhusu sasa hivi au haijaruhusu ni masuala ambayo yameshajadiliwa sasa hivi sina haja ya kuyarudia. Lakini kinachonitia wasi wasi ni kwamba sisi tuko *stagnent* katika sheria zetu, hatutaki mabadiliko na wizara yenyewe inaitwa utumishi na utawala bora. Kwa hivyo, moja katika *characteristic* za utawala

bora ni kumpunguzia Rais madaraka, jambo ambalo serikali imelishikilia Rais huyo huyo mmoja kila kitu. Kweli tumempa urais, lakini ndio kila kitu yeye hana haja ya wengine.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka tuendelee, lakini tujuwe kwamba tunaifanya hii nchi yetu idumae, kwamba Rais madaraka yake yako pale pale na yanamegwa kila siku madaraka ya vyombo vyengine kwa sababu ya kumpa Rais. Sasa ikiwa hatutotoka huko basi hatutokwenda katika utawala bora na matokeo yake Rais ukimpa madaraka makubwa basi anageuka mfalme. Naomba nimalizie hapa tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 4	Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu
Kifungu cha 5	Kinga kwa Mkurugenzi Mkuu
Kifungu cha 6	Uteuzi wa Naibu Mkurugenzi Mkuu
Kifungu cha 7	Sifa za Mkurugenzi Mkuu na Naibu Mkurugenzi Mkuu
Kifungu cha 8	Wafanyakazi Wengine pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 9	Fedha za Mamlaka

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nikiri kabisa kwamba sina taaluma yoyote ya sheria, lakini nataka nitolewe wasi wasi zaidi na Mhe. Waziri,

Mhe. Mjumbe Fulani: Lakini una taaluma ya ukaidi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Wala sina taaluma ya ukaidi, nina taaluma ya hoja kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Kiwani. Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 9(3) kuna fedhaza mamlaka.

Nilimfahamu Mhe. Waziri na Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini kwa taaluma hiyo ya wananchi wa Kiwani walionituma naona itakuwa ni vigumu sana kutofautisha baina ya ruzuku, misaada na rushwa. Ukisema mamlaka ya mkurugenzi kwamba awe na ruhusa ya kuchukua ruzuku na misaada, basi nina hakika kwamba wale wala rushwa watatumia kipengele hiki na tutakuwa hatujafanya la maana. Kwa hivyo, nashauri kwamba sentensi hii iongoke na badala yake ikiwa kunahitajika fedha nyengine, basi ziwe fedha zitakazopatikana kutokana na adhabu mbali mbali kwa mujibu wa sheria hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Hija Hassan hayuko mbali sana na kule na kule ambako sheria hii imezungumzia. Ruzuku na rushwa na vitu viwili tofauti. Tulisema kwamba Mkurugenzi ruzuku hii na misaada hii atakayoipokea ni ile ambayo itakuwa katika utaratibu wa kibajeti na sio vyenginevyo. Kwa hivyo, kama Mkurugenzi Mkuu ataamua kwenda kuchukua ruzuku kwa kificho yaani kwa njia ile ya rushwa, hiyo itakuwa sio ruzuku ambayo imekusudiwa hapa. Kwa hivyo, na yeye vile vile atalazimika kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria hii. Lakini ruzuku inayozungumziwa hapa ni suala la ile ruzuku na misaada mingine kutoka nje ambayo itakuwepo katika utaratibu wa kibajeti ya serikali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kama ni ruzuku ambazo zitapatikana kwenye misaada ya kibajeti, naomba maneno haya yaingizwe kwamba ni misaada ya kibajeti, ili hatimaye Baraza liweze kupitia kama tulivyokubaliana, lakini isiwe tu ruzuku wazi wazi, lazima tuongeze maneno kwamba misaada ya kibajeti iwe ya ndani au nje ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, bakubaliana na yeye.

Mhe. Hija Hassan Hija: Tuendelee.

Kifungu cha 9 Fedha za Mamlaka

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu kifungu hiki pamoja na masahihisho aliyoyaomba Mhe. Hija Hassan, lakini huu ni muhimili wa *executive* umetajwa sasa hivi, na muhimili wa *executive* yaani serikali inapata fedha zake kutoka katika bajeti ya serikali kupitia Baraza la Wawakilishi. Sasa mimi sikubaliani na hoja ya kuweka kifungu (b), kwa sababu wizara zote zinapata misaada, zinapata ruzuku kutoka sehemu mbali mbali, lakini fedha zote hizi huletwa katika Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuidhinishwa matumizi. Sasa kuweka kifungu hiki peke yake inaonesha kuwa zitapatikana fedha hizi zitaidhinishwa na nani matumizi yake.

Kwa hivyo, hakuna haja. Madhali imeshatajwa kifungu (a), kiwango cha fedha kitakachoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika kila mwaka wa fedha kwa matumizi ya mamlaka, huwenda fedha ile inatoka katika bajeti ya serikali au ilipatikana katika bajeti ya misaada, lakini itaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi, kuna haja gani ya kuweka kifungu (b). Hilo ndio swali langu. Mhe. Waziri naomba anipe majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Rashid Seif Suleiman angekisoma kwa ukamilifu hiki kifungu kinavyoeleza. Kifungu (b) kinasema, naomba ninukuu;

Kifungu (b)

> "Ruzuku, misaada na fedha zinazopatikana kupitia njia nyengine zitakazopokelewa na mamlaka kutoka vyanzo vyengine vya fedha vinavyokubalika".

Vinavyokubalika maana yake ni kwamba hapa lazima ufuatwe utaratibu wa sheria. Sasa anaposema kwamba hiki kingeondoka, mimi nadhani Mhe. Mjumbe angekiwacha hiki kifungu kikabakia kama kilivyo, kwa sababu kinajitosheleza chenyewe, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki ni cha NGO, ni NGO pekee ndio inayofanya kazi hii. Lakini hii ni *institution* ya serikali, haiwezi ikapokea fedha tu huko. Mimi naona NGO ndio zinazoweza kupokea fedha kwa njia ya utaratibu huu ruzuku na nyenginezo. Lakini *institution* ya serikali haiwezi ikapokea fedha namna hii huko kwa huko, njia gani hizo zinazokubalika, hebu na atueleze hasa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza labda nikubaliane na mawazo ya Mhe. Rashid Seif kuhusu wasi wasi wake, kwamba kwa hadhi ya chombo hiki kisiwe na harufu wala dalili ya kwamba labda kinaweza kikapata fedha kwa njia nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tumepitisha sheria nyingi ambazo zinaunda mamlaka mbali mbali na kwenye sheria hizi tunazozipitisha kifungu kama hiki kipo, kwa sababu mamlaka zote hizo tulizopitisha ya Mkemia Mkuu, ya Bodi ya Viwango ile ya *Bureau Standard* na nyenginezo ukisoma kwenye sheria ya DPP. Kwa mfano sheria namba 2 ya mwaka 2010 kifungu kama hiki kipo.

Kifungu hiki cha (a) na (b) kwa sababu kuna wakati ambapo unapokea ruzuku kwa njia ya vifaa na ambapo vifaa vile pengine wala hujui thamani yake, kwa hivyo havipiti kwenye Baraza la Wawakilishi, lakini ni kitu ambacho umepokea, inawezekana gari. Kilizungumzwa hapa choo kilichoko uwanja wa ndege wa madawa ya kulevya, kimekuja na kimepokewa kama ni msaada, lakini hakikuja kama ni fedha, ndio maana ya kuja kama ni

ruzuku, misaada au fedha. Sasa kama ni fedha bila shaka lazima utaratibu ulioko katika kifungu (a) ni lazima ufuatwe, lakini yako mambo ambayo yanakuja bila ya kwamba ni fedha. Wakati mwengine inakuja misaada ya masomo, lakini ukija ukifanya hesabu baadae nazo zile zina gharama ya kifedha, lakini si fedha kwa maana ya *cash*, ni sehemu ya mambo ambayo wanapata na ni lazima uyazungumze hapa katika suala la fedha, kwa sababu ni *resources.* Bahati mbaya pengine katika Kiswahili fedha maana yake ni pesa, lakini fedha kwa Kiingereza ni zaidi ya pesa kwa maana ya pesa *cash.*

Pia Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinamu-*encourage* yule alioko kwenye ile taaasisi kutafuta taasisi nyengine zikiwemo taasisi zinazofanana na hizi, ambazo zinatoa misaada ili aweze kutafuta misaada kuiendeleza taasisi yake, ndio madhumu ya hii. Lakini mimi sioni kama hii itapelekea basi wapokee misaada kama NGO, kwa sababu hiki kifungu kimo. Mimi naomba Mhe. Rashid Seif Suleiman akaangalie sheria zote tulizopitisha za kuunda hizi mamlaka atakuta kifungu hiki kipo na madhumuni yake ni haya.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu, hususan alipoyatambua mawazo yangu, kwamba hiki ni chombo cha namna nyengine kuliko hivyo, hivyo vyengine vyote ni vya utekelezaji, lakini hiki ni chombo cha ufuatiliaji wa namna gani watu na viongozi mbali mbali wanavyopata fedha zao na matumizi yao kuhusiana na mambo ya rushwa na kuhujumu uchumi.

Kwa hivyo, mimi nasema kwamba pamoja na hali hiyo, lakini tutupie macho kifungu hiki ili wale ambao wataajiriwa wasiwe ndio wapokea rushwa. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 9 Fedha za Mamlaka

Kifungu cha 10 Hesabu na Ukaguzi

Kifungu cha 11 Makisio pamoja na Marekebisho yake

Kifungu cha 12 Ripoti ya Mwaka pamoja na marekebisho yake

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilionesha wasi wasi wangu kuhusu kifungu hiki cha 12 ripoti ya mwaka na nikasema utaratibu tulionao hapa Zanzibar kwa taasisi takriban zote, ukiacha mashirika ya umma ambayo yanaongozwa na sheria nyengine. Lakini taarifa za mahesabu ya mwisho wa mwaka zinapelekwa miezi 3 baada ya mwisho wa mwaka wa fedha. Sasa hapa imewekwa miezi 4, nasema hii italeta tofauti, hata itakuwa ina-*contradict* na ile sheria ya fedha ya mwaka 2005. Kwa hivyo, ni vyema ikawekwa miezi 3 vile vile, lakini Mhe. Waziri ama sikumsikia au hakujibu hii hoja, nilikuwa naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Abdalla Juma Abadalla, ni kweli kipengele hicho sikukijibu. Kwa hivyo, naomba nikubaliane naye kwamba iwe ni ripoti ya miezi 3, ili kupata ile robo ya mwaka, ahsante kwa hiyo nakubaliana naye.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 12 Ripoti ya Mwaka pamoja na marekebisho yake

Kifungu cha 13 Kazi za Mamlaka pamoja na marekebisho yake

Kifungu cha 14	Uwezo wa Mkurugenzi Mkuu pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 15	Uwezo Maalum wa Kuchunguza
Kifungu cha 16	Kushirikiana na Taasisi Nyengine
Kifungu cha 17	Tathmini ya Utendaji Kazi
Kifungu cha 18	Kuendeleza Ufanisi
Kifungu cha 19	Uchunguzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 20	Utambulisho kwa Mchunguzi
Kifungu cha 21	Malalamiko Yaliyokuwa Hayakuchunguzwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 22	Maelezo ya Mali ya Mtu Anayehusishwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 23	Agizo la Kutoa Taarifa pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 24	Kuwasilisha Kumbukumbu na Mali pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 25	Kukagua Eneo
Kifungu cha 26	Kukubalika kwa Kitu Kinachotolewa au Kilichopatikana
Kifungu cha 27	Kuwasilisha Hati ya Kusafiria pamoja na marekebisho yake

Kifungu cha 28	Kumkamata mtu
Kifungu cha 29	Kutoa Maelezo Yatakayoathiri Uchunguzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 30	Kujifananisha na Mkaguzi
Kifungu cha 31	Taasisi ya Uchunguzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 32	Taarifa ya robo mwaka
Kifungu cha 33	Taarifa ya Makosa kwa mwaka
Kifungu cha 34	Uchunguzi Kufanyika kwa Nia Safi
Kifungu cha 35	Mashtaka ya Makosa
Kifungu cha 36	Rushwa Katika Utawala pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 37	Ushawishi Katika Kutoa Ushauri pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 38	Kumdanganya Mwajiri
Kifungu cha 39	Mgongano wa Maslahi
Kifungu cha 40	Kujifananisha Kutokana na Uteuzi wa Mdhamini pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 41	Rushwa Katika Zabuni

Kifungu cha 42	Ubadhirifu wa Mali ya Mapato pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 43	Kutumia Vibaya Mali
Kifungu cha 44	Kukwepa Kodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 45	Kufanya Magendo
Kifungu cha 46	Kuficha Bidhaa
Kifungu cha 47	Kufanya Jambo Kinyume na Ushindani wa Soko
Kifungu cha 48	Kutumia Vibaya Taarifa za Kiofisi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 49	Usafishaji wa Fedha Haramu
Kifungu cha 50	Usafirishaji wa Dawa Haramu pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 51	Kughushi Bidhaa au Fedha pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 52	Mpango wa Kudanganya Kima cha Fedha pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 53	Matumizi Mabaya ya Ofisi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 54	Kuhamisha Manufaa ya Rushwa

Kifungu cha 55	Kushughulikia Mali za Mtuhumiwa pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 56	Rushwa Katika Uchaguzi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kifungu cha 56, nataka kujua ni wakati gani hii adhabu itatumika.

Mhe. Mwenyekiti: Hatujakusikia vizuri, hebu rudia tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kifungu cha 56, nataka kujua ni wakati gani kifungu hiki kitatumika wakati uchaguzi unaendelea jimboni, ikiwa kama mimi ni mgombea.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim Ayoub wakati nilipokuwa nikijibu hakuwepo. Lakini la pili ni kwamba kosa lolote lililoainishwa hapa kwenye sheria hii hatua itachukuliwa pale ambapo muhusika atalifanya lile kosa lenyewe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano, jimbo langu lina matatizo, ikitokezea ajali mtu anataka kusaidiwa, nitasaidika vipi wakati kama ule na uchaguzi unakaribia.

Mhe. Mwenyekiti: Hatujakufahamu bado.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimeshachukua fomu ya uteuzi jimboni na bado shida zinaendelea jimboni na wale wananchi watanihesabu kama ni mwakilishi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Jaku Hashim anaelewa, kwamba kwanza Baraza hili au Bunge au Baraza la

Wawakilishi, linakipindi cha kuzinduliwa na kipindi cha kuvunjwa. Lakini pale ambapo tayari Haji Omar Kheir ametia nia ya kuchukua fomu ya kugombea, basi katika kipindi kile haruhusiwi kutoa huduma yoyote, hiyo ndio maana ya sheria hii.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, labda kwa kumtoa wasi wasi zaidi tu Mhe. Jaku Hashim ni kwamba kwenye makosa ya jinai kuna kitu kinaitwa, ili vitimie ni lazima kuwe na kitu wanaita yaani iwe hicho ulichokifanya ni kiovu na kwa nia ovu. Sasa kutoa msaada kitakachozingatiwa ni mazingira ya huo msaada wenyewe, kwamba je ilikuwa sio sahihi na ilikuwa ni kwa nia ambayo ni ovu kwa mujibu wa sheria hii. Hivyo ndio vigezo ambayo vitatumika, sio kila utakapofanya hivyo wala usifanye wakati mwengine kwa kuwa na wasi wasi, ilimradi kitakachozingatiwa ni mazingira ambayo jambo hilo ulilitenda na nia yako katika kutenda jambo hilo, ndio msingi wa kosa la jidai.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu cha 56	Rushwa Katika Uchaguzi
Kifungu cha 57	Kutoa rushwa kwa Afisa wa Kigeni
Kifungu cha 58	Rushwa ya Ngono pamoja na marekebisho yake

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kidogo nahitaji ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri, juu ya kifungu hiki ambacho kinagongana na vifungu vya sheria nyengine, ambapo kifungu hiki cha rushwa ya ngono kimeeleza faini pamoja na adhabu, yaani faini isiyopungua milioni 3 au kifungo kisichopungua milioni 2. Lakini kuna kifungu cha sheria ya rushwa ya ngono inayohusiana na masuala ya ngono ambapo mtu anapolazimishwa kufanya ngono bila ya ridhaa, kwa idhini yake mwenyewe ni kosa kwa mujibu wa sheria na akipatikana na

hatia huyo mtu atakwenda jela miaka 30. Hii kufanya ngono bila ridhaa yake ni pamoja na hii rushwa kwa sababu anafanya ngono kwa sababu ya kutegemea jambo. Kwa hivyo, hiyo ni bila ya ridhaa yake mwenyewe, yaani amelazimika.

Lakini Mhe. Mwanasheria wakati alipokuwa akitoa ufafanuzi pale alisema inategemea ni sheria ipi itakayotumika ama hii au nyengine. Mimi nahisi kidogo pana utata hapa, hebu atupe ufafanuzi ambao tayari sheria hii imeeleza faini na adhabu iliyowekwa. Lakini kuna Sheria nyengine ya Jinai, ambayo nayo inazungumzia kitu kama hicho na adhabu yake ni miaka 30.

Sasa vipi tunapoweka sheria hizi mbili zinatofautiana, pamoja na kwamba kuna Sera ya Upangaji wa Faini pamoja na mambo mengine ambayo tumeelezwa. Lakini sheria hii ndio tunapitisha, yaani tunaondoka hapa na itakuwa tayari ipo. Kwa hivyo, kidogo tupate ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naamini Mhe. Mjumbe hana wasi wasi na hiki kifungu, lakini anataka awe na hakika wapi mtu anaweza kutekeza, wapi anaweza kuingia hatiani.

Kwa kweli hapa kifungu kiko wazi, kwa sababu kinachozungumzwa hapa ni kudai sio kufanya, hivyo ndivyo kifungu kinavyosema kwamba mtu ambaye atadai au kuomba, yote mawili ndilo ambalo ni kosa. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kudai pengine mtu anaweza kudai katika *central sanction* ukaona labda dalili amekubali, kumbe bado hajakuli, ukaendelea kufanya hilo Kosa jengine la Jinai la *rape*. Sasa utakapofikia hatua hiyo na ushahidi upo kwamba ume-*rape*, sasa itakuwa ni *case* nyengine hiyo sasa ume-*rape*.

Kwa hivyo, hapo ndipo atakaposhtakiwa kwa Kosa la Kubaka na adhabu yake kwenye Sheria ya Jinai imeelezwa vizuri sana. Lakini hapa kinachozungumzwa ni kudai, yaani ile kuanza kudai rushwa ya ngono ndicho kinachozungumzwa hapa.

Sasa ukenda mpaka ukafanya ni kosa jengine la ku-*rape* na inaweza ikatokea hiyo ukadhani kwamba mtu amekubali kumbe vile bado, basi ukawa umefanya kosa jengine, lakini ile kudai yenyewe ni kosa na ndilo linalokusudiwa kwenye sheria hii.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Kicheko/Makofi)*

Kifungu cha 58

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini nilishauri hapa kwamba adhabu hii ni ndogo, kwa sababu hapa kuna mambo manne mazito. Kwanza kuna suala la ajira, kupanda cheo, haki na kufanya upendeleo, mambo haya yote Katiba yetu ya Zanzibar imeyazingatia na kuyakataza, kwamba huwezi kumnyima mtu haki, fursa na wala kupata kazi.

Kwa hivyo, miaka miwili au shilingi milioni tatu kwa mtu anayefanya kosa hili ni ndogo sana. Kutokana na hali hiyo, nilipendekeza kwamba miaka hii isipungue 15 na faini shilingi milioni 10, kwa sababu inawezekana mtu akose haki na haki hiyo itakuwa tayari Katiba yetu imeikataza. Kwa kuwa tu hajatoa rushwa ya ngono na akikamatwa mtu huyo mwenye tabia kama hiyo na akikamatwa mtu huyo mwenye tabia hiyo, basi adhabu yake ni shilingi milioni tatu. Kwa kweli hiyo ni adhabu ndogo sana na tuzingatie.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tulieleza msingi wa hili kosa lenyewe. Kwa hiyo, msingi wa kosa ni

kwamba mtu amefanya kosa la kudai na mpaka ikafika ikawa *reported* na mtu akashtakiwa na kutiwa hatiani, maana yake ushahidi ulikuwepo. Vile vile sidhani kwamba huyo ambaye alikuwa na haki atakuwa amekosa haki, kwa sababu atakuwa ameliripoti na limechukuliwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kifungu hiki kuhusu adhabu, tuangalie kwamba imeweka *minimum* isiyopungua shilingi milioni tatu. Kwa hivyo, ni kazi ya Hakimu kuangalia ukubwa wa lile kosa lenyewe kutokana na mazingira yaliyofanywa, basi anaweza kuweka adhabu ambayo inastahili au kifungo cha miaka miwili.

Sasa tulisema hapa kwamba tatizo kubwa liliopo ni kuwa hatuna hiyo *Sentencing Policy*, kwa hivyo chochote tutakachoamua kitakuwa ni *arbitrary* kwa kiasi fulani.

Lakini jambo jengine la msingi ni kwamba uzoefu unaonesha na hizi hata tafiti nyingi zimefanywa, kuonesha kwamba wakati mwengine ukubwa wa adhabu sio kinachomfanya mtu asifanye lile kosa au kuwazuia wengine, maana yake wanasema sio kitu ambacho ni kizuizi cha kufanya kosa.

Kwa mfano, kama ingekuwa ni kizuizi cha kufanya kosa basi leo nadhani tusingekuwa na UKIMWI kwa baadhi ya nchi, kwa sababu adhabu yake ni kifo au masuala ya madawa ya kulevya kuna nchi hasa zinajulikana kama vile China, Iran adhabu yake ni kifo, lakini bado watu wanakamatwa na kutiwa hatiani.

Vile vile kitaalamu jambo jengine ni kwamba kwa mtu ambaye yuko kwenye wadhifa kushtakiwa peke yake akafikishwa Mahakamani, basi ni adhabu kubwa sana na wengine ndio maana wanaamua hata kutoroka kuliko hata ile adhabu atapewa adhabu gani, wakati mwengine inakuwa sio jambo kubwa la msingi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kosa lenyewe na mazingira yaliopo, nadhani kama walivyokubaliana hata na kamati, basi nafikiri ni kiasi sahihi cha adhabu ambayo imetolewa hasa kwa sababu imetoa uwezo zaidi kwa Hakimu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naona mnapungua na hapa tunataka tupitishe vifungu. Kwa hivyo, naomba mjihimu huko mnakokwenda, ili muweze kurudi haraka.

Kifungu cha 58

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinanipa mashaka, kwa sababu linaweza likatendeka hilo tendo la kudai ngono na watu wakakubaliana na ngono ikafanyika, lakini kwa sababu wamekubaliana, basi hapa pakawa hapana uthibitisho kwa kuwa wamekubaliana.

Vile vile kifungu hiki kinaweza kusababisha mtu kwa sababu tu, ya utashi wake pamoja na kusema uongo akamtaja mtu kwamba amemuomba ngono kumbe si kweli na hayo ushahidi umeshakuwepo. Kwa mfano, kuna hadith moja ambayo niliipata kuhusu Mkurugenzi wa *IMF* Dominic Strauss Kahn alikashfiwa na kwa sababu tu kulikuwa na mtu ambaye alikuwa akigombania na yule anagombania, basi aliichukua kwamba hii ni *issue*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina wasi wasi na kifungu hiki kwamba tutawatia watu ambao hawamo katika hatia na tukamtia hatia kwa kutumia kifungu hiki. Kwa hivyo, naomba kifungu hiki kitizamwe vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, wasi wasi wa Mhe. Mjumbe hasa kwa kuwa ni mwanamke ni wa msingi kwa kweli na mazingira hayo yanaweza kutokea. Lakini huwezi kuacha tuhuma ni jambo ambalo linatokea kila siku.

Kwa bahati mbaya kwenye sheria huwezi ku-*deal* na tuhuma ambazo hazina ushahidi. Kwa hivyo, kinachozungumzwa hapa ni zile tuhuma ambazo zitakuwa na ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, sheria huko nyuma ilikuwa imekwenda mbali zaidi, yaani tafsiri. Kwa mfano, tafsiri ya Majaji kwenye suala hili hasa la Makosa ya Kujamiiana, kwa kweli ni jambo moja ambalo tafsiri pamoja na ushahidi wake unakuwa ni mgumu sana, kwa sababu wakati mwengine hiyo mtu kukataa kumbe amekubali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine mpaka na Jaji. Kwa mfano, kulikuwa na Jaji mmoja ambaye ni maarufu sana Jaji Biron yeye alisema kwamba Mwanamke wa Kiafrika kukataa pia ni sehemu ya kukubali, inabidi utafsiri. Kwa kweli hiyo, ni *statement* ambayo muda mwingi imekuwa ikitumika katika kutafsiri mazingira ya suala hili. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, nadhani sheria au kinachojaribu kuwekwa wazi ni pale ambapo atakuwa na tuhuma na tuhuma zile zitakuwa na ushahidi na hili suala la adhabu limewekwa kwa kuzingatia mazingira ambayo kosa la namna hii linaweza kufanyika.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu cha 58	Rushwa ya ngono pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 59	Kushiriki kosa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 60	Faini ya ziada ya lazima.
Kifungu cha 61	Adhabu ya jumla pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 62	Kulipa fidia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 63	Fidia kwa manufaa yasiyohalali pamoja na marekebisho.
Kifungu cha 64	Fidia nyenginezo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 65	Fidia baada ya kupatikana na hatia.
Kifungu cha 66	Kutaifishwa kwa mali isiyo na maelezo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 67 .	Amri ya kuzuia mali iliyotuhumiwa
Kifungu cha 68	Mali isiyo na maelezo itatilia nguvu ushahidi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 69	Hati ya kuonesha thamani ya mali pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 70	Kanuni kuhusiana na mshirika wa kosa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 71	Hati ya kuonesha wadhifa na manufaa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 72-	Uwezo wa kuagiza uchunguzi pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 73	Makosa kusikilizwa na Mahakama Kuu.
Kifungu cha 74	Kusimamishwa kazi kwa kosa la rushwa na kuhujumu uchumi.
Kifungu cha 75	Kusimamishwa kazi kwa kutiwa hatiani kwa kosa la rushwa au kuhujumu uchumi.
Kifungu cha 76	Kupoteza sifa kwa kutiwa hatiani kwa kosa la rushwa au kuhujumu uchumi.
Kifungu cha 77	Kutangazwa kwa waliopatikana na hatia.
Kifungu cha 78	Kinga kwa watoa taarifa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 79	Kumzuia mtu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 80	Kinga ya jumla.
Kifungu cha 81	Kuchukuliwa kama mshiriki wa kosa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 82	Mila kutokuwa utetezi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 83	Kushindikana au kutokuwa na nia si utetezi pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 84	Ushirikiano na Mamlaka nyengine.
Kifungu cha 85	Ushirikiano na sekta binafsi.
Kifungu cha 86	Msaada kutoka nchi za kigeni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 87	Kubadilishana wahalifu.
Kifungu cha 88	Tendo lililofanywa nje ya Zanzibar pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 89	Kanuni.
Kifungu cha 90	Kufutwa kwa sehemu ya 10 na 14 ya Sheria ya Makosa ya Jinai Nam. 6 mwaka 2004.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar wa waka 2012, usomwe kwa mara ya pili.

Mswada wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ya mwaka 2012
(Kusomwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja iliyotolewa na Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*
(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ya mwaka 2012 kusomwa kwa mara ya pili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar wa mwaka 2012, usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja iliyotolewa na Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo, sasa imepitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kuwa ni sheria. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa nichukue fursa hii kukushukuruni sana, kwa namna ambavyo mumeonesha mashirikiano kuweza kupitisha mswada huu hadi tukafikia mwisho hapa. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kuliahirisha Baraza hili hadi kesho siku ya Jumatano tarehe 25/01/2012 saa 3:00 asubuhi. *(Makofi)*

(Saa 12:50 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 25/01/2012 saa 3:00 asubuhi)